ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge

10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/ Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara

	Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/ Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake

81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Tatu – Tarehe 31 Julai, 2012

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Naibu Spika,(Mhe. Ali Abdalla Ali) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: (Kny: Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Bishara na Kilimo, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya makadirio ya mapato na matumzi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2012. Naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa taarifa aliyonipa Mhe. Spika, ni kwamba hivi asubuhi tutamwita waziri Mhe. Said Ali Mbarouk, ili asaidie na baadae tutamwita mwenyewe Mhe. Waziri kwa kufanya majumuisho. Kwa sababu waziri aliwahi kufanyakazi kwenye wizara hii, kwa hivyo, ameomba amsaidie mwenzake katika kujibu hoja. Mhe. Waziri karibu sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza mchango wangu, naomba niseme kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando, naomba kuunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake na kwa uwasilishaji wa hotuba yenyewe. Hotuba imepangika vizuri na wenzangu wamesema hilo na mimi naomba niseme na nimpongeze. Katika kitabu chake kwenye ukurasa wa 23 naomba nimpongeze kwa kuanzisha kampeni wa unywaji wa maziwa katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo muhimu sana ambalo kwa kweli wafugaji wetu

litawasaidia sana. Wafugaji wetu wamekuwa wakijitahidi, lakini mara nyingi wamekuwa wakilalamika kwamba bidhaa yao inakosa 333soko, na inakosa soko kwa sababu Wazanzibar kwa kiwango kikubwa hawajaharibika na tabia ya unywaji wa maziwa. Sasa kampeni hii ambayo ameianzisha na maonesho ambayo ameyafanya bila shaka kwa kiwango kikubwa itasaidia kuibua hizo tabia za watu wetu kutumia bidhaa hii muhimu kwa afya ya watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, hata katika mkahawa wetu wa hapa Barazani siku zile za kula mchana, ukenda pale sio sana kuwaona hata wajumbe wa Baraza lako tukufu wakiagiza bidhaa ya maziwa, utawaona wengi wanaagizia supu hasa ya pweza, lakini maziwa sio sana humuone swahib yangu hapa *captain*, bahati mbaya amechelewa kuingia. Yeye huyu akiingia pale huuliza vipi supu ya pweza ipo, kama ipo hiyo anataka, lakini maziwa sio jambo ambalo linapendezewa. Kwa hivyo, hili wameanzisha jambo zuri na kwa kweli namuomba sana Mhe. Waziri hili aliendeleze kwa maslahi ya afya za watu wetu, lakini pia kwa uchumi wa ufugaji wetu.

Jambo jengine ambalo naomba nilizungumzie ni sheria ya uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010. Mhe. Naibu Spika, sheria hii tuliitunga sisi Baraza la Wawakilishi, katika sheria ya mwisho mwisho kuitunga kwenye kipindi kile cha awamu ya sita, hii ni sheria moja. Nakumbuka zilitungwa sheria hapa pamoja na marekebisho ya katiba. Kabla ya kutungwa sheria hii yalifanyika mashauriano mengi na wadau wanaohusika, mimi nakumbuka vizuri. Mzee wangu Mhe. Burhan Saadat Haji alikuwa Waziri wa Wizara ya Kilimo ambapo shughuli za uvuvi zilikuwa zinaingia mule. Hata sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi aliatufanyia semina ya sheria hii, ukiachilia mbali kamati mbali mbali za wavuvi wetu ambao mimi katika Jimbo la Gando nakumbuka kamati zangu za uvuvi za Shehia za Fundo, Gando, Ukunjwi pia zilishirikishwa katika kutunga sheria hii. Sasa tukizungumza leo kwamba sheria hii haikuwashirikisha wadau, kwa kweli mimi napata mshangao mkubwa.

Niseme Mhe. Naibu Spika, kwamba hii sheria ni vizuri sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwanza tukaisoma, tukaifahamu na baadae tukaitumia katika kuwaelimisha wananchi wetu, kwa sababu sio vizuri kuizungumza kwa jumla kwamba sheria hii ni mbaya, inawanyanyasa wavuvi. Hii sheria ni moja katika sheria laini sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi mara moja nilipita nchi ya *Maldives*, nilikuwa na swahib wangu mmoja, tulipopita pale tukaonana na waziri wa uvuvi, tulipofika asubuhi ofisini kwake ali- *download* sheria yetu ya uvuvi katika kompyuta yake, kwa sababu sheria hii baada ya kuitunga *World Bank* wanayo kama mfadhili wetu. Kwa hivyo, aliingiza katika mtandao. Alipo *download* sheria yetu, akatuambia waheshimiwa bado hamjawa tayari kuimarisha sekta ya uvuvi katika nchi yetu, kwa sababu sheria hii bado ina mapungufu ambayo, wavuvi wenu wanaweza kutumia katika sheria hii kuharibu mazingira ya bahari.

Kwa hivyo, leo Waheshimiwa Wajumbe wakisema sheria hii inawanyanyasa wavuvi. Labda tukubaliane kwamba sasa tuyawache mazingira yetu ya bahari yawe huru kuharibiwa na wavuvi, matokeo yake baada ya muda wa miaka miwili mitatu tuone taathira yake. Kwa wenzetu Maldives kamati za uvuvi za maeneo ni mahakama za

mwanzo katika sekta ya uvuvi ufukweni. Pale ufukweni mvuvi anapelekwa jela, mfano akija na samaki mdogo ni kosa, akitumia vifaa ambavyo sivyo ni kosa, pale pale hakuna habari ya kwenda huku na huku.

Kwa hivyo, sisi bado tumetoa nafasi kubwa, tunapoteza muda mkubwa na tunapoteza muda mwingi na matokeo yake tunakuwa na tatizo kubwa. Sasa pale *Maldives* nyavu hazitumiki. Walituambia bado mnatumia nyavu. Ndio. Nyavu hasa. Wao wanatumia mshipi tu. Samaki mpaka wa kilo 20 kiwandani hanunuliwi anaambiwa mdogo rudisha. Sasa sisi kama tunataka utaratibu wa kutumia nyavu ambazo zitakokota na kuharibu matumbawe, hili litaatuathiri sana. Kwa hivyo, mimi ningewaomba sana wenzangu tuiangalieni sheria ile katika kipengele baada ya kipengele, tuiangalie ubaya wake iko wapi. Lakini mimi nadhani kuwa ni sheria nzuri, tunahitaji kuisoma vizuri, halafu tuitumie kuwasomesha watoto wetu.

Mimi katika Jimbo la Gando Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuisomesha sheria hii na wavuvi wangu wamenielewa na matokeo yake tumekubaliana kwamba bahari iliopo baina ya kisiwa cha Uvinje mpaka juu Hoteli ya Manta tuhifadhi wenyewe. Wamejikusanya kwa hilo shehia zote, tutashirikiana na shehia za Jimbo la Mtambwe na Jimbo la Wete pamoja na shehia za Jimbo la Gando ili ile bahari kuhifadhi, tutatafuta utaalamu na mashauri kutoka Idara ya Uvuvi ili tuanzishe uhifadhi wa bahari yetu. Hatutaki kuona kwamba bahari ile wanakuja watu wengine kwa nia moja au nyengine katika kuiharibu mazingira yake, kwa sababu athari ya kiuchumi tutapata sisi watu wa Jimbo la Gando na jirani zetu Jimbo la Wete na Jimbo la Mtambwe.

Kwa hivyo, wito wangu Mhe. Naibu Spika, badala ya Waheshimiwa Wawakilishi kuilalamikia ile sheria, basi wangeweza kwanza kujifunza ile sheria, halafu wakapata nafasi ya kukaa na wavuvi wao kuangalia wapi ile sheria ina kasoro. Mimi bado naona ile sheria ni nzuri ambayo kama tutajifunza nayo, kwa kweli itakuwa ni eneo ambalo linaweza kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar, yeye alituambia kwamba kama sheria ile tunaiona ni nyepesi basi tupeleke kwake mapendekezo ya kuitia ukali zaidi ili kuhakikisha kwamba mazingira ya bahari yetu, yamekuwa ni mazingira ambayo yamewezesha uchumi wa nchi yetu kupitia sekta ya uvuvi, ili iweze kukua zaidi. Kwa hivyo, bado niwaombe wenzangu kwamba sheria ile ambayo tumeipitisha sisi Wajumbe wa Baraza hili mwaka 2010 tu. Sasa Mwakilishi kupitisha sheria humu, halafu baada ya siku mbili akasema sheria hii ni mbaya. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, tutakuwa tumepoteza fedha za wananchi bure kukaa hapa kupitisha sheria, halafu baada ya siku mbili tunarudi tunasema aah! Sheria ile sio. Nafikiria hilo sio jambo zuri.

Eneo jengine ambalo naomba sana nimpongeze Mhe. Waziri ni mradi wa uvuvi wa bahari kuu. Hili ni eneo ambalo kwa kweli Mhe. Waziri na watu wake wamefanya jambo la maana sana. Niwapongeze kwa kutafuata dola milioni 22 na zaidi, karibu zaidi ya bilioni 30 kwa ajili ya mradi huu. Ni kweli kwamba watu wetu sasa ni wakati wa kwenda katika bahari kuu. Lakini uvuvi wa bahari kuu Mhe. Naibu Spika, sio suala la kuvamiwa, linahitaji matayarisho. Mhe. Waziri katika kitabu chake amesema

kwamba anaanza na mafunzo, ili uvuvi wa bahari kuu uweze kufanyika maana yake ni kwamba ni kuvua katika maji makubwa na kwa kutumia vyombo maalum. Sasa unakwenda umbali wa maili zaidi ya 150 maeneo ambayo yanahitaji ujuzi mzuri na vifaa vile ambavyo vinakuja, vina mambo mengi ya kutumia, kuna GPS, kuna *navigation* na kuna masuala ya *engine* na mambo mengine. Kwa hivyo, sio suala la kuchukua boti za gharama kubwa leo ukampa mvuvi bila ya kumfundisha. Kwa kweli litakaa pale hilo boti bila ya kuvua. Leo wavuvi wetu hawa ambao wanavua, ukivuma upepo tu hapo samaki hawapatikani. Sasa ni lazima kwanza wapewe mafunzo ya kutosha katika suala hili, ili watakapopewa vifaa waweze kwenda katika uvuvi wa bahari kuu. Ndivyo wenzetu walivyoanza. Sirlanca wameanza hivyo kwanza, walianza kuwafunza wavuvi wao baadae wakawawezesha.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ningeshauri kwamba utaratibu huu aliouanza Mhe. Waziri wa kuona kwamba anaanza na uvuvi wa bahari kuu, ni jambo la kupongezwa na mfumo aliouanzisha wa kuanza na mafunzo ya wavuvi 60 ni jambo zuri. Mimi nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba Jimbo la Gando lina wavuvi wengi, hasa maeneo ya Fundo na Gando. Kwa hivyo, ningeomba katika wavuvi 30 wa Pemba atakaowachukua, basi awaangalie na wavuvi wa Fundo na wavuvi wa Gando, nao pia ni wazuri na wanahitaji mafunzo ili na wao waingie katika mpango huu wa uvuvi wa bahari kuu.

Eneo jengine Mhe Naibu Spika, namalizia ni suala la ufugaji wa mazao ya baharini. Hapa napo naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa jitihada zake ambazo amezianza. Nimeona humu, ana mradi kupitia Korea ni jambo zuri. Kwa kweli hapa ni maeneo ambayo watu wetu wakipewa nafasi au mafunzo zaidi, wenzangu wamesema kwamba wanaanza kufuga lakini hawana ujuzi mzuri. Sasa mradi huu ambao ameuanzisha ni mradi ambao uko katika kiambatanisho nambari 10, kwenye ukurasa wa 76 kuna fedha karibu bilioni moja, yaani milioni 733,000,000 kwa kweli sio pesa kidogo, ningeomba sana Mhe. Waziri auendeleze mradi huu ni muhimu, mafunzo ni muhimu kwa wavuvi hawa wanaofuga samaki. Kama alivyosema Mhe. bi Mwanajuma ni kwamba kuna maeneo mengi Kangani na maeneo mengine ambayo wakipatiwa mafunzo wanaofuga samaki basi tunaweza kufanya tofauti ya masuala haya ya uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, Jimbo la Gando nao wanajitahidi katika ufugaji wa samaki hasa maeneo ya Chozi na Gando kwenyewe. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Waziri, katika mafunzo haya ya ufugaji wa samaki kwa kupitia maradi huu wa Korea, basi aangalie maeneo hayo ili zile jitihada ambazo zimeanzishwa ziende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la mradi wa *MACEMP*. Wenzangu wamelizungumza hili na mimi ningeomba sana nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuuendeleza mradi ule na mpaka unafikia hatima. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, mradi ule umefanya mambo mengi. Ule mradi ulikuwa una-cross kati katika taasisi kama saba au tisa nakumbuka vizuri. Kwa kweli wenyewe watu wa *MACEMP* wanachofanya pale ni kutoa fedha baada ya miradi kuibuliwa katika shehia. Kwa hivyo, sisi katika shehia, majimbo na wilaya ndio wenye miradi, sio idara ya uvuvi au mradi wa *MACEMP*. Kinachokwenda kupatikana katika mradi wa *MACEMP* ni fedha za kutekeleza miradi yenyewe. Kwa

hivyo, kama kuna *performance* nzuri au mbaya, wa kuhojiwa ni shehia, majimbo na wilaya ambako miradi ile ndiko inakoibuliwa na inakosimamiwa.

Kwa hivyo, usije hapa kusimama ukasema watu wa *MACEMP* hakuna wanachokifanya. Hapana. Wamefanyakazi nzuri *MACEMP* wao wametoa fedha baada ya kuombwa na shehia zetu na majimbo yetu. Kwa hivyo, kama mradi wa Jimbo la Gando la uvuvi hawakufanya vizuri, mimi kama mwakilishi nina lawama, sio Mkurugenzi wa Uvuvi au meneja, au waziri. Ni mimi niliokwenda kwa waziri mradi wangu, sasa kama nimeshindwa kuusimamia ni mtihani.

Kuna miradi Mhe. Naibu Spika, boti zake zimeuzwa. Sasa umekuja wizarani, umepita kwa waziri na umekwenda kwa mkurugenzi na umekwenda kwa meneja, wamekupa shilingi milioni 30 umenunua boti. Sasa sisi katika shehia, au sisi katika majimbo tumeshindwa kuisimamia ile miradi tunarudi tena kwa wale waliokupa fedha. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hawa jamaa wanapaswa kupongezwa kwamba miradi yetu katika shehia, walikuja kwetu kutuomba na tumewasaidia. Hili ndio ambalo nitalisema na katika hili ningetaka kuzungumza suala kidogo la mradi huu, hasa katika eneo la Beit el Ajab. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba pale na sisi katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, mradi huu umetusaidia sana katika maeneo mengi hasa katika maeneo ya magofu katika shehia mbali mbali. Lakini kama wizara imetusaidia katika maeneno mawili.

Kwanza eneo la makumbusho *Peace Memorial Museum.* Mnaopita pale karibu na hospitali mtaona matengenezo makubwa ambayo yamefanyika, kwa kweli nawashukuru. Tuliomba shilingi milioni 78,000,000 tunashukuru sana zimetumika mpaka hivi sasa karibu shilingi milioni 52,000,000 wakati wowote akitumalizia, tutawaomba watu wa MACEMP wamalizie zile shilingi milioni 26,000,000, tunashukuru sana.

Jengine ambalo sisi tuliwaomba ni matengenezo ya Beit el Ajab. Kwa kweli walitupa shilingi milioni 249,000,000. Bahati mbaya mkandarasi vifaa alivyoleta mwanzo akatuwezekea bati. Ilikuwa na mambo mawili. La kwanza ilikuwa ni marekebisho ya umeme, lakini la pili ni kuezeka lile jengo. Shughuli za marekebisho ya umeme yanakwenda vizuri, lakini shughuli za uwezekaji kwa kweli hayakwenda vizuri. Juzi Jumapili baada ya kuulizwa swali hapa na Mhe. Mwakilishi wa Mji Mkongwe, namshukuru. Nilikutana na *consultancy* wa ujenzi tukakaguwa na leo mchana tuna ahadi nimemwita mkandarasi wa ujenzi kutoka Dar es Salaam. Kwa hivyo, naamini kwamba hadi mwisho wa mradi kwa kasi ambayo tunakwenda nayo tumembana, tunahakikisha kwamba matengenezo ambayo watu wa MACEMP kwa kupitia Mhe. Waziri hapa ametusaidia basi tunaamini kwamba tutakuwa tumefikia pahala.

Mhe. Naibu Spika, nilisimama kuzungumza hayo. Lakini naomba sana nimalizie kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa bajeti yake na watendaji wake kwa kweli wanafanyakazi nzuri, hasa Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi. Mimi naomba nimpongeze binafsi, anafanyakazi moja nzuri sana. Mhe. Naibu Spika, yule kijana kwa kweli anapaswa kupewa pongezi, kazi aliyonayo ni ngumu. Mimi nimeshamuona mara mbili akizamia katika bahari ya maji makubwa kuibua madema ya macho madogo ambayo

wavuvi wetu wameyaweka. Kwa kawaida Wakurugenzi hukaa ofisini waki-*enjoy air condition*. Yeye ofisi yake ni bahari tena ya kina kikubwa. Kwa hivyo, kazi anayoifanya ni kubwa, anaisimamia sheria ambayo tumeipitisha katika Baraza la Wawakilishi, hivyo badala ya kulaaniwa kijana huyu, nafikiria Baraza lingepata nafasi ya kumshukuru kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa niaba ya Baraza hili, lakini kwa niaba ya serikali kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na kama nilivyosema naomba kuunga mkono hoja. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita waziri kufanya majumuisho, naomba niwatambulishe wajumbe kwamba tumekusudia asubuhi hii mapande ya saa 6:00 tuipitishe bajeti hii na baadae tumwite Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, asome bajeti yake.

Kwa hivyo, naomba *quorum* itimie, musitoke toke sana nje. Mjumbe atoke kwa haja muhimu halafu arudi. Pia akitoka anijulishe mimi. Nadhani tumefahamiana. Sasa tunamwita Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kufanya majumuisho ya bajeti yake. Mhe. Waziri karibu sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha tukiwa wazima na wenye afya nzuri. Pili napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Naibu Spika, pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yenu. Michango yote iliyotolewa ilikuwa na nia ya kunisaidia mimi pamoja na watendaji wa wizara yangu katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nitiwe shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Asha Bakar Makame, kwa ushauri nasaha na maelekezo waliyotoa katika kuielekeza wizara yangu ili kufikia malengo yetu ya kuwahudumia wafugaji, wavuvi na wakulima wa mwani. Wizara yangu itafuta maelezo ya kamati kwa kadiri ya uwezo wetu.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba kutoa shukrani zetu kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, pamoja na Mhe. Viwe Khamis Abdalla ambaye pia hii leo alisalimia kwa niaba ya Mwenyekiti, Mhe. Asha Bakar Makame.

Aidha, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wajumbe wote wa kamati hii kwa kutupatia ushauri na maelekezo ambayo yamechangia sana katika kupatikana kwa ufanisi kwenye yale mambo yaliyofanywa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, michango yote iliyotolewa na kamati hii ni wizara kuitekeleza sera ya mifugo ili sekta hii iweze kutoa mchango mkubwa zaidi kwenye pato la taifa. Wizara isimamie utekelezaji wa mpango mkuu wa sekta ya uvuvi, yaani *fisheries master plan*. Umuhimu wa ufugaji wa samaki na katika bajeti ya mwaka 2012/2013

maeneo ya mfano yamekwisha tengewa fedha na yataanzishwa na yatakuwa mashamba darasa kwa wazalishaji wetu.

Kuuenzi mtambo wa *liquid nitrogen* ili udumu kwa muda mrefu na kujaribu kuuza bidhaa hii kwa taasisi nyengine zaidi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili itumike kikamilifu. Kuweka umuhimu mkubwa juu ya uzalishaji wa mbuzi wa maziwa wenye sifa bora kwani shughuli hii imeonesha kupata mafanikio makubwa hasa kwa wanawake wa Wilaya ya Kusini ambao wanafaidi matunda ya juhudi zao.

Vile vile kuviendeleza vituo vyetu vya mifugo vilioko wilaya mbali mbali za Unguja na Pemba. Kuendelea kutetea haki za mifugo na juu ya hali wizara yangu imekwishaandaa *regulation* ambazo utekelezaji wake utatoa afueni kwa wanyama kwa mateso wanayoyapata. Kutoa kipaumbele kwa wazalishaji wa mwani kwa azma ya kuwaendeleza katika uzalishaji na usarifu wa mwani. Wizara yangu inawafikiria sana wazalishaji wa mwani. Kutoa umuhimu kwa mradi wa uvuvi wa maji ya kina kirefu ambao kwanza utaimarishwa kwa kutoa taaluma kwa vijana juu ya uvuvi huo.

Mhe. Naibu Spika, hotuba ya wizara yangu ilichangiwa na jumla ya wajumbe 24 moja kwa moja na wajumbe kama 5 hivi kwa maandishi. Naomba uniruhusu niwataje wale wote waliochangia hotuba hii moja kwa moja ni:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Hassan Hamad Omar
3. Mhe. Ali Salum Haji
4. Mhe. Hamza Hassan Juma
5. Mhe. Mussa Ali Mussa
6. Mhe. Rufai Said Rufai
7. Mhe. Omar Ali Shehe
8. Mhe. Salmin Awadh Salmin
9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Kazija Khamis Kona
12. Mhe. Abdi Mosi Kombo
13. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa
14. Mhe. Salim Abdalla Hamad
15. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
16. Mhe. Marina Joel Thomas
17. Mhe. Subeit Khamis Faki
18. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
19. Mhe. Mohamed Said Mohamed
20. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
21. Mhe. Nassor Said Salim
22. Mhe. Asha Abdul Haji
23. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
24. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Aidha, wajumbe wafuatao walichangia kwa maandishi nao ni:

25. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo
26. Mhe. Suleiman Hamad Khamis
27. Mhe. Fatma Mbarouk Said
28. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
29. Mhe. Mohamed Haji Khalid

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba michango, maelekezo, maoni na ushauri, mapendekezo waliyotupa tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo, kwani yatatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ili kukidhi matakwa ya wadau wote wa sekta ya mifugo na uvuvi hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako tukufu, sasa naomba niainishe maeneo yaliyochangiwa kwa ujumla kama ifuatavyo:-

1. Kuna maeneo yanayohusu Migogoro ya Wavuvi katika maeneo ya hifadhi,
2. Kuna Uvuvi Haramu,
3. Ukatili wa Wanyama,
4. Sheria ya Uvuvi Nam. 7 mwaka 2010,
5. Mashamba ya Mifugo ya Serikali,
6. Ubora wa Mifugo na Wanyama wanaopewa wafugaji,
7. Upandishaji ng'ombe kwa sindano,
8. Uwekezaji wa Kuku,
9. Kiwanda cha Chakula cha Mifugo,
10. Karantini za Mifugo,
11. Machinjio ya Mifugo,
12. Bei Ndogo ya Mwani,
13. Ufugaji wa Samaki,
14. Uvuvi wa Bahari Kuu kwa kuwawezesha wananchi kuvua katika maeneo ya Bahari Kuu,
15. Wizi wa Mifugo,
16. Taaluma ya Wafanyakazi,
17. Usarifu wa Bidhaa za Mifugo na Mwani,
18. Ziara za Mafunzo kwa watendaji Wakuu wa Wizara,
19. Majosho ya Mifugo,
20. Uvamizi wa Maeneo ya Mifugo,
21. Miradi ya Mifugo na Uvuvi,
22. Sera ya Mifugo,
23. Uimarishaji wa Takwimu na mwisho
24. Taaluma kwa Wafugaji na Wavuvi na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe pamoja na kuwasilisha majibu kwa hoja zilizotolewa kama ifuatavyo:-

Nikianza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, yeye alihoji kwa nini wananchi wa Jimbo la Kitope wamepewa ng'ombe wabovu. Jibu ni kwamba sababu inayopelekea

ng'ombe wanaopewa wananchi kutoka miradi mbali mbali kuwa na uzalishaji mdogo ni kutokana na matunzo dui ikiwemo kutowapatia lishe bora, kinga na tiba.

Hoja yake ya pili wakulima wa mwani wapatiwe vifaa vya kukaushia na mashine za kutengenezea vyakula. Jawabu ni kwamba wizara inafanya juhudi za kupata zana za usarifu, yaani mashine kupitia Washirika wa Maendeleo Korea (*KOICA*), ikiwa pia na kuangalia uwezekano wa kuanzisha Kituo cha Mwani katika eneo la Tumbe Pemba. *(Makofi)*

Aidha Ubalozi Mdogo wa China kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kutoa Mafunzo ya Mapishi ya Mwani, ili kuboresha Soko la Ndani.

Hoja yake ya tatu vijiji vya ***MINAI*** na ***MIMCA*** havijapata faida kutokana na kuwepo kwa maeneo ya hifadhi. Jawabu ni kwamba maeneo ya hifadhi yana faida nyingi miongoni mwa faida hizo ni kama ifuatavyo. Kwanza kuwaweka wavuvi pamoja chini ya utaratibu wa sheria hii, ili kuwawezesha kufanyakazi zao kwa pamoja, jengine kujirudi kwa rasilimali za bahari.

Vile vile kutoa fursa zaidi kwa wageni, utalii kutokana na kuongezeka kwa jamii za samaki, pia kuongezeka kwa kipato cha wananchi kutokana na kazi za uvuvi na shughuli za utalii. Jengine ni kuwapatia mafunzo wavuvi kupitia Kamati zao juu ya mbinu bora za uvuvi na elimu ya mazingira.

Ujenzi wa miundombinu kutokana na mapato yanayopatikana kuyapatikana kusaidia ujenzi wa masoko ya kisasa katika vijiji vya maeneo ya hifadhi na masoko haya yamejengwa Nungwi, Matemwe, Pwani Mchangani, Uroa, Kizimkazi, Kendwa, Mazizini na Fumba.

Mhe. Naibu Spika, mapato hayo pia yanatumika katika ununuzi wa vifaa mbali mbali vya uvuvi na vyombo kama vile *freezers*, *boat*, vyavu, madema pamoja na mitego mingineyo ambayo huwa wanapatiwa bure wavuvi. Fedha hizo pia hutumika kwa ajili ya Mfuko wa Maafa katika kila kijini na wakati wa dharura baharini. *(Makofi)*

Kwa mwaka 2011/2012 Hifadhi ya *MIMCA* imekusanya kiasi cha jumla shilingi 85,854,080/=. Kati ya hiyo, jumla ya shilingi 58,840,230/= zimetumika kwa usimamizi wa eneo na shilingi 27,013,850/= kwa huduma za jamii.

Kwa upande wa *MINAI* jumla ya shilingi bilioni 1,034,818,792/= zimekusanywa. Kati ya hizo shilingi 98,868,042/= zimetumika kwa usimamizi wa eneo na shilingi 35,950,750/= kwa huduma za jamii.

Hoja ya pili litoka kwa Mhe. Hassan Hamad Omar na yeye alihoji ahadi ya Mhe. Waziri kusaidia dume la mbuzi kwa wafugaji wa Kijikani haikutekelezwa.

Jibu ni kwamba ahadi hii, ili kufikia utekelezaji wake ilitakiwa ufanyike kwa mashirikiano baina ya Wizara yangu na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kojani. Juhudi za kumpata dume mwenye sifa bora zitaendelea kwa kuzingatia mashirikiano kati ya

Wizara yangu na Mhe. Mwakilishi. Aidha kwa hatua za dharura wizara yangu imefanikisha kupatikana dume kwa muda mpaka ahadi hii itakapotekelezwa.

Hoja yake ya pili Mhe. Mjumbe kuhusu utekelezaji wa ahadi zilizotolewa ya kumalizia Bwawa la Ufugaji Samaki Kiungoni na Msaada wa Fedha kwa Mfugaji wa Samaki Kojani Pemba. Jawabu ni kwamba ni kweli Mhe. Waziri aliyenitangulia alitoa ahadi hiyo pamoja ahadi mbali mbali kwa wafugaji wa samaki Unguja na Pemba yakiwemo maeneo ya Kiungoni na Kojani.

Wizara yangu imeanza kutekeleza ahadi hizo kwa awamu tofauti, ambapo tayari imeshatoa fedha taslim na vifaa kama vile majembe, saruji, mapauro, shoka katika vijiji vya Pujini, Mwambe, Donge Mchangani, Chambani, Fukuchani na utaratibu huo unaendelea hadi kukamilisha na maeneo mengine kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo. *(Makofi)*

Hoja yake ya tatu wakati wa dharura wavuvi huwa hawaruhusiwi kuingia katika Hifadhi binafsi katika Kisiwa cha Chumbe. Mhe. naibu Spika, naomba kulifahamisha Baraza lako Tukufu kwamba hakuna marufuku kwa mvuvi yeyote kuingia katika Kisiwa cha Chumbe atakapopata matatizo ya dharura baharini. Aidha ni wajibu wa muwekezaji ambaye yupo ndani ya kisiwa hicho kuwapatia msaada unaosatahiki wakati wa dharura. *(Makofi)*

Uharamu wa Zana za Kuzamia (*Diving Equipment*s). Mhe. Naibu Spika, hoja hii pia ilichangiwa na Wajumbe wengine wafuatao sio Mhe. Hamad Hassan Omar tu, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Abdalla Moh'd Ali wote walitoa hoja ya suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, jawabu ni kwamba kifungu 17(1) cha Sheria ya Uvuvi Nam. 7 mwaka 2010 kimepiga marufuku matumizi yafuatayo:-

(i) Uvuvi wa Juya ni haramu na athari yake ni kuvua samaki wachanga, kuharibu matumbawe na kung'oa majani na hatimaye kuharibu mazalia ya samaki.

(ii) Uvuvi wa Mtando ni haramu na athari yake ni kuvua samaki wachanga, samaki ambao hawajafikia ukubwa unaostahiki kuvuliwa.

(iii) Uvuvi wa Kutumia Bunduki ni haramu na huharibu matumbawe na asilimia kubwa ya wavuvi bunduki huharibu matumbawe ikiwa ni pamoja na kuvua samaki wenye mayai. Hali hii huashirikia kwamba unapokuwa chini ya bahari inakuwa rahisi kumpiga samaki mzito, kwa sababu hana kasi ya kukimbia na nilazima awe karibu na tumbawe

(iv) Matumizi ya Kioo, Gesi na Viatu vya Kuogelea Mhe. Naibu Spika hivi havina uharamu wowote kwenye uvuvi, isipokuwa mvuvi anapokuwa navyo baharini huwa ndio chachu yake ya sababu ya kufanya moja kati ya mavuvi niliyoyataka hapo juu.

Kwa mfano, mtalii au rai mwengine yeyote atakayetumia vioo, gesi na viatu pekee bila ya kuwa na dhamira ya kuvua, basi hatokuwa

amekwenda kinyume na sheria hii. aidha vifaa hivi vinatumika zaidi katika shughuli za utafiti na utalii.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine matumizi ya mishipi, nyavu za jarife za mkondoni, madema yenye macho makubwa yanaruhusiwa na wala hayakatazwi kama alivyosema Mhe. Hassan Hamad Omar.

Aidha Mhe. Naibu Spika, ninachoomba kieleweke ni kuwa huwezi kuwa na eneo la hifadhi lenye matunzo yaliyobora ya kimaumbile ikiwa utaruhusu samaki wadogo kama dagaa na jamii kama hiyo ivuliwe. Kwa kweli kuwepo kwa jamii hiyo ndio mvuto wa samaki wengine wakubwa kuingia katika eneo la hifadhi, bila ya kuwepo kwa mfumo huo (*food chain*) eneo hilo haliwezi kuwa hifadhi endelevu.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa hakuna asiyefahamu uharibifu wa mazingira uliosababisha na vifaa hivyo kwa mvuvi ikiwa pamoja na kutoweka kwa makome, majongoo, kamba koche, pweza, ngisi na baadhi ya jamii za samaki zilizozoeleka hapa nchini.

Mhe. Ali Salum Haji na yeye aliuliza kuhusu Shamba la Tunguu karibu ekari 1000 zimechukuliwa. Jibu ni kwamba kutokana na mabadiliko ya Sera ya Serikali kutokujihusisha na uzalishaji moja kwa moja shamba hili lilirejeshwa Wizara ya Ardhi, Makaa, Maji na Nishati. *(Makofi)*

Hoja yake ya pili kuhusu Shamba la Kitumba linavamiwa na wananchi na wizara imechukua hatua gani. Jawabu ni kwamba wizara yangu inayo taarifa ya uvamizi huo na hatua zimechukuliwa za kuwataka wananchi waliovamia kuhama mara moja.

Hoja yake ya tatu mikataba ya Kampuni ya *ZAPOCO*, Kiwanda cha Chakula cha Kuku na Shamba la Kutotolea Vifaranga, hoja hili lichangia pia na Mhe. Mussa Ali Hassan. Jawabu ni kwamba baada ya mabadiliko ya Sera ya Serikali kutokujihusisha na uzalishaji wa moja kwa moja mali za Kampuni hii zilirejeshwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Sasa serikali kwa kupitia Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeingia ubia na wawekezaji binafsi kuendesha kampuni hiyo.

Hoja yake ya nne Uvamizi wa Kituo cha Upandishaji Ngo'mbe kwa Sindano, hoja hii pia ilichangiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma. Jawabu ni kwamba ni kweli kuwa kituo hichi kimevamiwa, lakini kwa sasa wizara imechukua hatua ya kupima na kulizungushia uzio wa matofali kwa lengo la kulinusuru eneo hilo.

Hoja yake ya tano kuhusu Mradi wa Kopa Ng'ombe lipa Ng'ombe, mradi huu ulianzishwa kwa gharama za kiasi gani na umepata mafanikio gani. Jawabu ni kwamba mradi ulianzishwa kwa dola za Kimarekani $150,000 kwa msaada wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za *Atomic* (*IPA*), ili kuendeleza mafanikio ya mradi wa kutokomeza ndorobo.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni jumla ya wafugaji zaidi ya 400 walifaidika na mradi huu. Pili utafiti ulionesha ongezeko la kipato cha familia kwa waliopewa ng'ombe hao. Tatu kuongezeka kwa lishe ya familia kutokana na familia hizi kunywa maziwa yanayozalishwa na familia husika na mwisho kupata taaluma ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuongeza taaluma hiyo kwa wafugaji wengine.

Hoja yake ya sita mbegu zinazotumika hazina ubora. Mhe. Naibu Spika, mbegu zinazotumika kupandishia ng'ombe kwa sindano ni zenye ubora. Changamoto zilizopo mara nyengine ni utunzaji wa ng'ombe chotara kuanzia anapokuwa hajazaliwa, yaani matunzo ya ng'ombe mwenye mamba na baada ya kuzaliwa, ng'ombe bora anapaswa kupata matunzo mazuri, ili aweze kutoa maziwa kama anavyotarajiwa.

Mchangiaji wa nne alikuwa ni Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Naibu Spika, naomba kuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba michango yote aliyoitoa kwa ajili ya kusaidia Wizara yangu nimeichukua na nitaifanyiakazi, kwa sababu yeye zaidi alitoa ushauri, nasaha pamoja na maelekezo na ninamshukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan naye alikuwa na hoja kadhaa. Hoja ya kwanza Wizara itoe nafasi kwa Waheshimiwa Wawakilishi kutafuta Soko la Mwani nje ya nchi. Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu haina pingamizi na hilo na tutashirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu. *(Makofi)*

Hoja yake ya pili wizara iweke mitambo ya barafu katika majimbo na mikoa kwa ajili ya kuhifadhia samaki. Mhe. Naibu Spika, wizara yangu tayari imeshanunua mitambo minne ya kutengenezea barafu, ambayo wavuvi watapatiwa kwa matumizi katika vyombo vyao wakati washughuli zao za uvuvi.

Aidha wizara yangu tayari imeshajenga masoko sita Unguja ikiwemo Uroa, Nungwi, Kizimkazi, Matemwe, Pwani Mchangani na Kendwa na kwa upande wa Pemba ni matano, ambayo ni Mvumoni, Wesha, Kilindi, Mtangani na Mjini Ole ndani ya mwaka huu wa fedha na tayari yameshapatiwa *freezers* na tunatarajia kukamilisha masoko matatu kwa upande wa Unguja.

Hoja yake ya tatu wizara iwapatie wavuvi maboti, zana pamoja na elimu ya kuwawezesha kuvua bahari kuu. Mhe. Naibu Spika, hoja hii pia ilichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe wafuatao, Mhe. Mussa Ali Hassan alichangia hoja hiyo, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Abdi Mosi Kombo, Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mhe. Abdalla Moh'd Ali na Mhe. Omar Ali Shehe wote hao wamechangia hoja hiyo.

Kwa hivyo, jawabu yao ni kama ifuatavyo, kwamba wizara yangu imepanga kutoa mafunzo kwa vijana 60 Unguja na Pemba kuhusu uvuvi wa Bahari Kuu au kina kirefu cha maji. Aidha kwa kuanzia ununuzi wa boti mbili za kisasa kwenda kuvua kwenye bahari hiyo kutafanywa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi, Kiuchumi na Ushirika kupitia Mradi wa Pamoja wa Ajira kwa Vijana.

Kuhusu suala la mundombinu wizara yangu inaendelea kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na kuendeleza mazungumzo na washirika mbali mbali wa maendeleo na wawekezaji na kufikia azma ya kuwa na gati bora pamoja na Viwanda vya Kusindikia Samaki.

Hoja yake ya nne ukarabati wa majosho ya ng'ombe. Wizara yangu kwa kuanzia mwaka huu wa fedha italifanyia matengenezo Josho la Binguni. Aidha itatekeleza mpango wa kupeleka mabomba ya kunyunyizia dawa katika Vituo vya Mifugo, ili wafugaji wapate huduma ya kukogesha mifugo yao kwa yale maeneo ambayo yapo mbali sana na majosho.

Hoja yake ya tano ujenzi wa Kituo cha Mifugo katika Jimbo la Koani. Wizara yangu inafahamu kuwa eneo la Jimbo la Koani ni kubwa sana, hivyo ina mpango wa kujenga kituo cha kutoa huduma za mifugo katika eneo la Unguja Ukuu, ili kiweze kutoa huduma katika eneo la kusini ya jimbo hilo.

Mhe. Mjumbe mwengine ambaye ametoa hoja ni Mhe. Rufai Said Rufai, yeye aliuliza madhumuni ya utafiti ulikuwa ni kwa ajili ya kustawisha Mwani aina ya *Cottonii*. Aidha elimu ya matumizi ya mwani inahitajika na bei ndogo ya mwani ni tatizo. Hoja hii pia ilichangia na Wajumbe kadhaa akiwemo Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba mwani wa *Cottonii* na ule wa aina nyengine ni chakula kwa baadhi ya samaki. Aidha kutokana na utafiti uliofanywa ulihusisha ukuaji wa mwani kutegemea na msimu pamoja na kina cha maji.

Kuhusu elimu ya matumizi ya mwani tayari imeshaanza kutolewa katika vijiji vya Kiuyu Mbuyuni, Wingwi na Tumbe. Wizara yangu inaendelea kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa ajili ya kutafuta makampuni ya kununua mwani kwa bei ya juu zaidi. Vile vile kuhusiana na suala la vipodozi kwa sasa Kidoti, Paje na Bweleo wanasarifu mwani na kutengeneza sabuni na vipodozi.

Hoja yake ya pili Mhe. Mjumbe wafugaji wangapi wanaotesa wanyama wamefikishwa Mahakamani. Mhe. Naibu Spika, hoja hii pia ilichangia na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Panya Ali Abdalla. Jumla ya matukio 78 kwa wanyama yaliripotiwa mwaka jana 2011/2012. Kati ya hayo matukio 15 yalifikishwa Mahakamani kwa mashirikiano na Jeshi la Polisi na Baraza la Manispaa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa jambo hili, kwamba linahitaji mashirikiano makubwa baina ya wizara yangu, Waheshimiwa Wawakilishi, Taasisi Zisizo za Kiserikali na Jamii kwa jumla, ili kuwawezesha wenzetu wa Polisi kuchukua hatua za ziada.

Hoja yake ya tatu Mhe. Mjumbe ni kuondolewa kwa baadhi ya ujenzi wa sehemu za Soko la Tumbe. Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wawakilishi kuwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipata ufadhili wa ujenzi huo kupitia Washirika wa Maendeleo Benki ya Dunia. Ni kweli

hapo awali soko hili katika mipango yake lilikuwa lijengwe kwa kufuata mahitaji yaliyoelezwa, sasa baada ya kuwasilishwa michoro ya ujenzi wa soko hilo kwa Benki ya Dunia kwa hatua ya pili, benki iliondoa baadhi ya ujenzi wa majengo mengine na kuidhinisha yafuatayo:-

(a) Sehemu ya Mnada.
(b) Sehemu ya Mauzo ya Samaki.
(c) Sehemu ya Kukoshea na Kusafisha Samaki.
(d) Vyumba vya Baridi (*Cold Rooms*), kwa ajili ya hifadhi ya samaki.
(e) Afisi nne.
(f) Jiko lenye uwezo wa kuhudumia wapishi wanane na mwisho
(g) Mkahawa wa watu 80.

Hivyo, wizara yangu inaendelea na hatua za kukamilisha ujenzi wa majengo hayo na kama hali itaruhusu basi mengine itabidi yasimamiwe na Serikali.

Mhe. Omar Ali Shehe naye alichangia hoja hii na alisema Wizara ina malengo mawili mapya, hivyo kwa nini inatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo katika vifungu vya Idara ya Uzalishaji Mifugo Pemba, Idara ya Utibabu Pemba na Idara ya Utumishi Unguja.

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba kifungu 0013 jumla ya shilingi milioni 4,000,000/= zimetengwa kwa ukarabati wa ujio katika Shamba la Chamanangwe. Kifungu 014 jumla shilingi milioni 15,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya uanzishaji wa Karantini ya Nzi Wengi na ukarabati wa Josho la Makangale na *Clinic* ya Wete.

Kifungu 0401 zimetengwa shilingi milioni 3,000,000/= kwa ukarabati wa Karakana ya wizara. Kifungu 0601 jumla shilingi milioni 12,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa Vituo vya Tiba vya Mifugo katika vijiji vya Potoa, Dunga pamoja na Binguni.

Hoja yake ya pili Mhe. Mjumbe wizara imetenga fedha hizi kutumika kwa kuzuia Kichaa cha Mbwa, ambacho si muhimu kuliko maradhi mengine. Mhe. Naibu Spika, jawabu ni kwamba Maradhi ya Kichaa cha Mbwa ni ugonjwa unaowapata wanyama na binadamu, hivyo ni vyema Waheshimiwa Wajumbe wakatambua kuwa maradhi haya bado yapo na yanahitaji kudhibitiwa, ili kuondosha madhara kwa binadamu katika nchi yetu.

Kwa mfano, mwaka jana jumla ya watu 59 walitafunwa na mbwa na *sample* 11 za wanyama zilichunguzwa na kuthibitishwa kuwa na maradhi ya Kichaa cha Mbwa, kwa hivyo maradhi haya yapo tena ni hatari.

Mhe. Naibu Spika, njia bora na rahisi zaidi ni kuzuia maambukizi na kutumia chanjo na kufunga uzazi kwa lengo la kupunguza wanyama wazururaji, ndiyo sababu iliyopeleka wizara yangu kutenga fedha, kwa ajili ya kunusuru maisha ya binadamu ambaye akipata maradhi haya, basi hufariki.

Hoja yake ya tatu Mhe. Mjumbe ni kwamba nini hatima ya mashamba ya Mtakata, Chamanangwe, Makurunge, Kipange, Pangeni, Kitumba na Bambi. Mhe. Naibu Spika, Shamba la Mtakata limekabidhiwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko (*ZSTC*) kwa lengo la kuzalisha viungo.

Vile vile Shamba la Makurunge hivi sasa liko chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, Shamba la Bambi wamekabidhiwa JKU, Shamba la Kitumba bado liko chini ya Wizara yangu na linatumika kwa kufanya utafiti wa mbuzi. Mengine mashamba ya Chamanangwe na Pangeni bado yanatumiwa na wizara yangu kwa ajili ya kufanyia utafiti wa mifugo.

Hoja yake ya nne ni kuhusu wizi wa mifugo na hoja hii pia imechangiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Naibu Spika, jawabu ni kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imeanzisha Kamati Maalum ya Ulinzi Shirikishi katika kila shehia, ili kudhibiti tatizo la wizi wa mifugo.

Hoja yake ya tano ni kwamba kuhusu Kesi ya Jinai Nam. 430/2011 na hoja hii pia imechangiwa na Mhe. Subeit Khamis Faki. Mhe. Naibu Spika, jawabu ni kwamba suala la Kesi ya Uvuvi haramu Nambari 430 inayomhusu mshtakiwa Abdalla Mweleza na wenzake 23 iko kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli wizara yangu ilipokea barua tarehe 09/02/2012 kutoka kwa Hakimu wa Wilaya bwana Abdulrazak A. Ali aliyoitaka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi urudishe vifaa kama ilivyosemwa na Mhe. Subeit Khamis Faki.

Aidha tarehe 10/02/2012 Mwanasheria wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi aliomba apewe *proceeding* ya kesi hiyo ya Jinai na kufuatia barua ya tarehe 14/02/2012 Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Uvuvi alipeleka barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na barua hizo zote ninazo, barua inayohusu kutoridhika na maamuzi ya kesi hiyo na hivyo kutaka kukata rufaa, ambapo Ofisi ya *DPP* ndiyo iliyopaswa kukata rufaa hiyo Mahakamani.

Tarehe 10/05/2012 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kwa mara nyengine ilimuandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka na kutaka taarifa juu ya malalamiko ya barua yake ya awali, ambapo hadi leo haijapatiwa jawabu kutoka kwa *DPP*.

Kwa hivyo, ilipofika tarehe 23/05/2012 Mhe. Hakimu wa Mahakama ya Mwera akaeleza juu ya utaratibu wao wa Kimahakama na kuthibitisha kwamba washtakiwa waliachiwa huru, kwani walionekana kwamba hawana kesi ya kujibu kama Mhe. Subeit Khamis Faki alivyoeleza na kurejea tena yeye Mhe. Hakimu kuthibitishwa kuwa maamuzi haya ni yale yatakayoanzia tarehe 23/05/2012, ambapo ndipo mhuri wa Mahakama ulipotiwa.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia barua hiyo Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uvuvi tarehe 03/05/2012 alipeleka barua tena kwa Hakimu wa Mahakama ya Mwera, ambapo Mhe. Mjumbe akihitaji naweza kumsomea.

Kwa hivyo, baada ya barua hiyo wizara yangu haikupokea jibu kutoka Mahakama yenyewe kuonesha utaratibu na miongozo halali wa kukabidhi vifaa hivyo kama barua nilivyoisoma au nitakavyoisoma. Aidha isingekuwa busara kuvikabidhi vifaa hivyo pasi na Mahakama kutoa maelekezo, lazima Mahakama ndio wao watoe maelekezo, wawe ni mashahidi na wahakikishe kwamba vile vifaa vipo.

Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako lifahamu kuhusiana na tatizo lililotokezea juu ya kesi hii ya Jinai.

Mhe. Salmin Awadh Salmin na yeye alihoji suala lake la ukusanyaji wa takwimu. Mhe. Naibu Spika, ukusanyaji wa takwimu unafanyika katika madiko yalioko ndani ya kila wilaya, kwa kawaida siku za ukusanyaji ni 16 kwa mwezi ndani ya Mpango unaofahamika kama ni ***CACH ASSESSMENT SURVEY***, ambao umethibitishwa na *FAO*.

Kwa hiyo, wakusanyaji hao wanapatiwa vitendea kazi pamoja na kupitiwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba takwimu hizo ziko sahihi na zimechukuliwa kutokana na taratibu zilizopangwa. Takwimu hizi zinakusanywa na kufanyiwa uhakiki kupitia katika ngazi ya wilaya na baadaye kuwasilishwa wizarani kwa ajili ya kumajumuisho ya mwisho, kwa kila mwezi takwimu hizo zinawasilishwa wizarani, ili kupelekwa kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuwa na Mpango wa Kitaifa.

Hoja yake ya pili Mhe. Mjumbe, kwa nini kifungu cha mshahara kimeongezeka mara dufu kulinganisha na mwaka wa fedha uliopita. Mhe. Naibu Spika, jawabu ni kwamba Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora umetoa ongezeko la mishahara kwa kada za *science* katika fani za mifugo, hii ndio sababu iliyopelekea kuonekana mshahara wao umeongezeka kwa kasi kubwa.

Hoja yake ya tatu Mhe. Mjumbe, mpanga wa ujenzi wa Chinjio la Kisasa pamoja na matumizi ya Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji. Mhe. Naibu Spika, mradi huu umeombewa shilingi milioni 243,000,000/= na hadi kufikia mwezi wa Juni ilipatiwa shilingi milioni 108,253,750/=, ambazo ni sawa na asilimia 44. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi ajiridhishe na maelezo ya matumizi yaliomo katika kiambatisho Nam. 2 ya kitabu changu cha bajeti.

Hoja yake ya nne Mhe. Mjumbe, kuhusu fedha za Mradi wa *MACEMP* zilizotengwa mwaka huu 2012/2013 zimepungua ukilinganisha na mwaka 2011/2012. Mhe. Naibu Spika, jawabu ni kwamba sababu kubwa iliyopelekea kiwango hicho cha fedha kushuka ni kutokana na kipaumbele cha wizara ilichojiwekea cha kuwaondoa wavuvi wadogo wadogo na kuwapeleka katika uvuvi wa kina kirefu, yaani bahari kuu, ambapo jumla ya shilingi milioni 300,000,000/= zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu na yeye pia alitoa hoja kadhaa pamoja na kutupa ushauri katika maeneo yafuatayo. Kwanza kuhusu wawekezaji wakubwa wawekeze katika kuzalisha vifaranga, ushauri wake tumeuchukua na tutaufanyiakazi, kudhibiti utesaji wa wanyama na hoja hii tayari tumeshajibu wakati nilipokuwa nikijibu hoja za Mhe. Rufai Said Rufai naye alichangia.

Usafi wa masoko hauridhishi, na hili ni jukumu la Bodi ya Chakula na Dawa, Manispaa na Halmashauri za Wilaya.

Hoja yake ya kwanza ameuliza kifungu 0015 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba fungu 220505 vifaa vidogo vidogo ni kumi na moja milioni, laki saba amehoji kifungu hicho. Jawabu ni kwamba mwaka jana fedha hizi zilitumika kwa kununulia vifaa vya usafi wa ofisi. Mwaka huu fedha hizi zimekadiriwa kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vidogo vidogo vya uvuvi 200 yaani kama mishipi na ndoana kwa vikundi 20 vya uvuvi.

Hoja yake ya Sera ni Idara ya Mipango Sera na Utafiti, kifungu 220514 Sera na Sheria kifungu 63166 Huduma za Utafiti. Jawabu ni kwamba vifungu hivi ndivyo vinatekeleza shughuli kuu za Idara. Kifungu 220514 Sera na Sheria, ni milioni ishirini na moja, laki mbili thamanini na sita. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kutoa nakala 500 za sera ya mifugo kwa lugha ya kiingereza na 500 kwa lugha ya Kiswahili. Kutayarisha mpango wa utekelezaji wa Sera Mifugo pamoja na kuupitisha mpango huo katika ngazi ya uongozi wa Wizara na kutayarisha baadhi ya mapendekezo ya mradi wa mifugo inayotokana na sera hiyo.

Kifungu 263166 Huduma za Utafiti nacho utakuta kina jumla ya shilingi milioni kumi na nane laki sita sabini na moja alfu. Kifungu hiki kitatumika kwa shughuli za utafiti ikiwemo kukamilisha taratibu za mapendekezo ya uanzishwaji wa Baraza la utafiti, kufanya ziara katika vituo vya utafiti Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha kazi ya utafiti pamoja na kufanya utafiti wa kijamii unaohusu ufugaji wa kuku wa kienyeji na sio ruzuku kama fungu lilivyo.

Hoja yake ya tatu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mgao wa fedha za Bahari Kuu ukoje kwa mujibu wa fedha zilizopatikana. Mhe. Naibu Spika, jumla ya fedha zilizopatikana tokea mwaka 2010 ni dola milioni tatu laki tatu thamanini na nne elfu, mia tatu hamsini na nane na senti 30. Kwa mgawanyo wa kutumia utaratibu uliowekwa ni kama ifuatavyo. Zanzibar imepata dola elfu sita, sabini na sita elfu mia nane na sabini na moja na senti sitini na sita ambayo ni asilimia 20. Tanzania Bara ni dola elfu moja, kumi na tano elfu mia tatu na saba na senti 49 ambayo ni asilimia 30. Mamlaka ya kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ni dola milioni moja, laki sita sitini na mbili elfu, mia moja tisini na saba na senti kumi na tano.

Hoja yake ya nne Mhe. Ismail Jussa, mapato ya Bahari Kuu mwaka jana 2011/2012 bajeti ilikuwa ni milioni 900 lakini zilizopatikana ni milioni mia moja, thalathini na tatu elfu laki saba, sabini elfu mia mbili na thalathini na nne. Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka huu wa fedha Julai 2011 hadi Aprili 2012 Zanzibar ilipata mgao wa dola thamanini na tano elfu mia saba na saba na senti thamanini na nane sawa na Tanzania shilingi milioni mia moja thalathini na tatu, laki saba sabini elfu , mia mbili thalathini na nne, ambazo ndizo tulizoziripoti. Kati ya dola milioni mia nne ishirini na nane laki tano thalathini na tisa mia nne na ishirini zilizopatikana mwezi wa Mei 2012, Zanzibar ilipata dola laki moja ishirini na tano elfu mia nane na thamanini na nne na senti arobaini na nne, kati ya dola mia sita na ishirini na tisa, mia nne ishirini na mbili na

senti mbili. Juni, ilipata dola arobaini na tatu elfu mia sita na arobaini na tatu na senti ishirini, kati ya dola elfu mbili kumi na nane mia mbili kumi na sita.

Kwa hiyo hadi Juni 30/2012 Zanzibar ilipata jumla ya dola elfu mbili hamsini na tano elfu mia mbili thalathini na tano na senti hamsini na mbili, sawa na shilingi za Kitanzania milioni mia tatu tisini na nane lakini moja tisini na saba na mia nne na kumi na moja na nukta mbili. Sawa na asilimia 44 ya makadirio ya fedha zote.

Hoja yake ya tano Mhe. Jussa soko la samaki Malindi limezidiwa, hivyo nashauri lijengwe soko jipya sehemu ya Kizingo. Mhe. Spika, hoja hii pia imechangiwa na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na jawabu ni kwamba soko la kisasa la samaki litajengwa Malindi kutokana na uzuri wa eneo hilo kitaalamu ikilinganishwa na eneo la Kizingo lenye kina cha maji kidogo na mwamba.

Hoja yake ya sita ujenzi wa makumbusho ya jengo la Beit-el-Ajaib. Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa jengo hili unaendelea naomba kufahamisha kuwa ujenzi huu ulikuwa na maeneo matatu yakiwemo usafishaji wa eneo la wazi la juu, uwekaji njia mpya ya umeme na kubadilisha mabati ya paa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kueleza kuwa kazi ya usafishaji wa sehemu ya juu imeshafanyika na kazi ya uwekaji taa baada ya kumalizika kazi ya *fitting* itaendelea. Mhe. Naibu Spika, kazi ya uwezekaji itaanza mara tu baada ya kuwasili mabati maalum kutoka Mombasa Kenya, tunatarajia mabati hayo kuwasili wakati wowote kuanzia wiki ijayo na mara tu yakifika kazi ya uwezekaji itaanza. Jumla ya fedha za mkataba huu ni shilingi milioni mia mbili arobaini na tisa laki nne na elfu tisa mia nne, na hadi sasa jumla ya shilingi milioni hamsini na nane laki mbili sitini na moja elfu mia sita tisini na tatu nukta saba mbili, zimetumika.

Hoja yake ya tano Mhe. Jussa fungu la safari na mafunzo limekuwa kubwa. Ukweli kwamba kuhusu fungu la safari Mhe. Spika, wizara yangu inahitajika kushiriki katika mikutano mbali mbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi. Mikutano hii huvutia wawekezaji na kuanzisha miradi mbali mbali ya maendeleo ya sekta zetu kama tunavyoshauriwa na Waheshimiwa Wawakilishi kama Mhe. Hamza alisisitiza sana tuwe tunatoka toka sana ili kuhakikisha kwamba sekta hii inasonga mbele.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu fungu la mafunzo wizara yangu ina upungufu mkubwa wa wataalamu wa kada mbali mbali. Hivyo kwa kutumia bajeti yake imeamua kwa makusudi kuwaendeleza wafanyakazi wake kitaaluma. Aidha fedha hizi zitatumika kuwapa taaluma ya ufugaji na uvuvi wadau mbali mbali wa sekta hizi.

Mhe. Panya Abdalla naye alitoa hoja na alichangia bajeti hii, hoja yake inasema kuwajengea jengo maalum waanikaji madagaa. Ni kweli kwamba uanikaji wa dagaa unawapa tabu sana na usumbufu mkubwa wazalishaji wa dagaa hasa wakati wa mvua. Wizara yangu baada ya kuyaona hayo imekaa pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na kutafakari namna ya kuwasaidia wananchi hao.

Mhe. Kazija Khamis Kona, Viti Maalum na yeye alikuwa ana hoja yake anasema madume mawili yanatosheleza. Kwa kweli hayatoshelezi. Wizara ipo katika utaratibu za kununua madume matano madogo ili kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora.
Hoja yake ya pili huwezi kumkamata pweza bila ya kumchokoa. Mhe. Naibu Spika, hoja hii pia imechangiwa na Waheshimiwa wafuatao nao ni Mhe. Kazija Khamis mwenyewe Viti Maalum, Mhe. Subeit Khamis Faki, alichangia hilo, Mhe. Hassan Hamad Omar na yeye alichangia hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli kwamba napenda kumfahamisha Mwakilishi mwenzangu kuwa pweza ana maumbile yake maalum ukiachilia mbali masuala ya kijamii. Kisayansi ya bahari pweza ni kiumbe ambacho hutafuta makaazi yake katika miamba na kujificha kwenye mipasuko ya miamba hiyo yaani mashimo, kulingana na ukubwa wa shimo lenyewe na ukubwa wa pweza mwenyewe. Shimo dogo, pweza mdogo, shimo kubwa hukaa pweza mkubwa.

Matumizi ya Umangu katika eneo la shimo analokuwepo pweza huacha sumu ambayo pweza mwengine haingii. Na matumizi ya kutumia kijiti ni vigumu kumkamata pweza akiwa ndani ya shimo kwa sababu nyama yake inakuwa ngumu na upatikanaji wake unakuwa wa tabu. Kwa kutumia utaratibu maalum wa vikopo ama vya plastiki, vya chuma au vya bati vinavyokwenda sambamba na ukubwa wa pweza unayemuhitaji.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuonesha mfano kupitia Baraza lako tukufu, Wawakilishi tujitolee kuwapatia wavuvi wetu vikopo kama hivi ambavyo thamani yake ni ndogo ili tuweze kuhifadhi mazingira ya bahari, vikopo tunavyo hapa.
Mhe. Abdi Mossi Kombo naye vile vile alitoa hoja zake anasema mfugaji Ame hajapatiwa umeme baada ya Mhe. Rais kutaka asaidiwe kupatiwa umeme. Wizara inaendelea na mchakato wa kumtafutia chombo cha usafiri na sio umeme. Kwa sababu tatizo tulilokuwa nalo ni kumsaidia chombo cha usafiri.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa wa Kikwajuni na yeye vile vile alitoa hoja kadhaa anasema kwamba Wizara iweke umuhimu wa kuwasaidia wafugaji wetu wa kuku wa kitaalamu ili kuweza kuingia katika ushindani wa wewekezaji wanaoleta kuku kutoka nje. Jawabu ni kwamba wizara inachukua ushauri wake na hivi sasa imeshatayarisha mpango maalum wa kuimarisha ufugaji wa kuku nchini ambapo mpango huu unazingatia kuwasili taaluma kwa wafugaji, pembejeo, chanjo na kadhalika.
Hoja yake ya pili Mhe. Mahmoud kufanya mapitio ya Sheria ya Haki za Wanyama na malengo ya haki za wanyama na kwa nini tunafunga uzazi mbwa na paka. Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa 2011/2012 wizara yangu ilifanya mapitio ya Sheria ya Rasilimali ya Mifugo katika vipengele vya ukatili kwa wanyama na kuitungia kanuni. Kanuni hizo tayari zimeshatayarishwa na zipo katika hatua ya kwenda kwa Mwanasheria Mkuu kabla ya kuchapishwa katika gazeti la serikali.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ufungaji wa uzazi wa mbwa na paka, wanyama hawa wana uwezo mkubwa wa kuzaliana. Wanyama wanaozurura tu hufungwa uzazi na kutafutiwa watu ambao wanawahitaji. Mifugo michache hutunzwa vizuri na hupunguza athari za maradhi ya kichaa cha mbwa.

Hoja yake ya tatu vifaa vya maabara vimefungwa. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba vifaa vya maabara vimeshafungwa na vinatumika.

Mhe. Mwengine ni Mhe. Salum Abdalla Hamad na yeye alichangia kwa nini wametumika kuku vishingo tu katika kupandisha na majogoo ili kupata kuku chotara. Mhe. Naibu Spika, tulichokifanya ni kupata aina hizi za kuku chotara. Kuna tafiti nyengine zinazoendelea ambazo zinahusisha aina nyengine za kuku wa kienyeji na kuku wa kisasa ambayo matokeo bado hayajatolewa.

Hata hivyo, mfugaji alitumia kuku vishingo alifuata sifa nne kuu ambazo ni kuhimili magonjwa yaliyopo, utagaji mzuri, uleaji mzuri wa vifaranga na zaidi wanastahamili hali ya joto ambayo nchini kwetu inapatikana sehemu ya shingo isiyo na manyoya na kuwezesha kuondoa au kupunguza joto la mwili ambapo kuku huyo huweza kutumia vinasaba vyake kwa uzalishaji bora.

Kwa upande mwengine kuku wa kisasa wanalitumika ambao ni *leghorns au* ni *Staralop* na *road island* ni kuku bora wenye sifa na kutaga mayai hadi 340 kwa mwaka ikiwa wanapata matunzo mazuri.

Hoja yake ya pili Mhe. Salim Abdalla je, kupungua nguvu za mwenendo wa umeme haukuathiri uzalishaji wa *liquid nitrogen*. Jawabu ni kwamba upungufu wa nguvu wa mwenendo wa umeme unasababisha kutofanya kazi kwa mtambo wa kusitisha uzalishaji wa gesi. Napenda kumuarifu Mhe. Salim kuwa tatizo la umeme limerekebishwa kwa kuweka *transformer* mpya kituoni.

Hoja yake ya tatu wizara haioni umuhimu wa kupeleka mtaalamu kwenda kujifunza matengenezo madogo madogo ya mtambo wa *liquid nitrogen*. Wizara imeona umuhimu wa kumfunza mtaalamu wetu nchini Uholanzi juu ya matengenezo ya mtambo wa kuzalisha *liquid nitrogen* na mtaalamu huyo atapalekwa katika mwaka huu wa fedha.

Hoja yake ya nne mashamba darasa ya ufugaji wa samaki yapo Pemba tu je, Unguja hakuna. Mhe. Naibu Spika, kwa hivi sasa Unguja hakuna shamba darasa la ufugaji samaki lakini katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya shamba darasa kwa upande wa Unguja.

Hoja yake ya tano kwamba hakuna mfanyakazi mwanamke katika Idara ya Mipango Pemba. Mpango wa wizara kuelimisha wafanyakazi wake wa chini kuwa na wafanyakazi wenye *master plans*, uvamizi wa maeneo ya karantini na kuanzisha maeneo mapya ya karantini.

Hoja hii vile vile imechangiwa na Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe, Naibu Spika ni kweli hatuna mfanyakazi wa kike katika Idara ya Mipango Pemba. Wizara yangu sasa imekwishawapelekea maombi ya kuajiri wataalamu katika fani ya mpango kwa kuzingatia jinsia vile vile.

Wizara ina mpango na mkakati wa kuwaendeleza wafanyakazi na tumetenga fedha kuwaendeleza wafanyakazi wetu. Wizara vile vile imekwishayapima maeneo yake ya karantini yakiwemo Kisakasaka na taratibu za kutafuta hati miliki zinaendelezwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub na yeye alikuwa ana hoja kadhaa ikiwemo ya chombo cha uvuvi cha Muyuni kupelekwa Kizimkazi. Mhe. Jaku Hashim, bahati mbaya hayupo lakini ataelezwa. Mhe. Naibu Spika, chombo vya uvuvi cha Shehia ya Muyuni "B" kimepelekwa Kizimkazi kuhifadhiwa baada ya wanakikundi cha Muyuni kugombana na kupelekana kituo cha Polisi. Baada ya kufikia hatua hiyo, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni Mhe. Jaku Hashim aliomba Wizara yangu ya Uvuvi kuingilia kati suala hili ili kunusuru chombo, mashine na mtego visije kuharibiwa na wanakikundi.

Hatua iliyofuata baada ya hapo ni kuwa Wizara yangu ilifuatilia Polisi na kwenda kuvichukua vifaa hivyo na kwenda kuvihifadhi ofisini Kizimkazi. Kwa upande wa pili Wizara yangu ilitaka uhakika wa makubaliana ya kikundi hicho ikiwa wameafikiana ili vifaa hivyo viweze kurejeshwa halan. Na hivi sasa tayari Wizara yangu imeshapokea barua kutoka Wilayani kuwa makubaliano yameshafikiwa na tayari vifaa vimesharejeshwa. Kwa kuwa suala hili lilianzishwa kwa Mhe. Mwakilishi wa Muyuni Mhe. Jaku, wizara inalirejesha kwake kwa kuhakikisha kulisimamia ili mgogoro huo usijirudi tena.

Mhe. Marina Tomas, naye aliuliza miradi mingapi ya juu iliyotolewa na *MACEMP* ambayo ipo hai. Mhe. Naibu Spika, jumla ya vikundi vilivyopatiwa fedha za mradi wa MACEMP kupitia utaratibu wa TASAF ni 322 kati ya hivi vikundi 274 sawa na asilimia 85, viko hai na vinaendesha shughuli zao vizuri. Vikundi 30 vilivyosalia sawa na asilimia 15 havifanyi vizuri kutokana na kutoelewana baina ya wenyewe kwa wenyewe.

Mhe. Subeit Khamis na yeye alikuwa na hoja kadhaa. Hoja yake ya kwanza Wizara ilisema itawapatia wafugaji mbuzi wa maziwa. Lakini katika jimbo langu hakuna mbuzi wa maziwa. Wizara yangu inajua umuhimu wa kuendeleza ufugaji wa mbuzi katika maeneo ya Micheweni, kwa vile wananchi wengi wanafuta mbuzi wa kienyeji. Kutokana na hali hii ndio maana mradi wa JP5 uliamua kuboresha uzalishaji wa mbuzi kwa kuwapatia wafugaji mbuzi jike na dume bora wa maziwa.

Matunda yake yanaonekana katika Shehia za Shumba Mjini/Mjini Micheweni, Majenzi na Maziwa Ng'ombe ambapo wapo wafugaji wachache wanakamua mbuzi hao. Wao wanafaidika kwa ongezeko la haraka uzito wa mbuzi wao na kufikia uzito wa soko mapema na kupata bei kubwa.

Hoja yake ya pili Mhe. Subeit ni juu ya ufugaji wa samaki ni wa kitoweo tu na sio wa kibiashara. Mhe. Waziri atueleze uzalishaji wa samaki umefikia kiasi gani. Jawabu ni kwamba ni kweli kuwa ufugaji wa samaki kwa sasa haujafikia kiwango cha juu kibiashara. Ufugaji wa samaki upo katika hatua za mwanzo ambapo Wizara inaendelea kutoa mafunzo ndani na nje ya nchi.

Wizara imejenga mabwawa darasa ili kueneza utaalamu wa ujenzi wa mabwawa bora ambayo yataongeza uzalishaji wa samaki. Hata hivyo kuna maeneo ambayo yameanza vizuri kama vile Pujini, Chambani, Mangapwani, Nungwi na Ufugaji wa Kaa, Msuka na Kisakasaka.

Hoja yake ya pili Mhe. Subeit kwamba wavuvi wa Zanzibar wanateswa wakienda Tanzania Bara kuvua. Je, wavuvi tutawatendea nini ili kuondosha mateso ya Bara. Mhe. Spika, suala la uvuvi si la muungano kwanza, hivyo Zanzibar inatumia sheria zake na Bara ina sheria zake. Mvuvi yoyote atakayekwenda Bara atalazimika kufuata sheria za Bara. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi watusaidie kuelimisha wavuvi wao kuhusu hilo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, na yeye alikuwa ana hoja kadhaa, vifaa vya uvuvi kuharibiwa bila ya kupelekwa Mahakamani. Hoja hii imechangiwa vile vile na Mhe. Hassan Hamad Omar wa jimbo la Kojani. Ukweli ni kwamba Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya Uvuvi ya 2010 kifungu cha 27, kimetoa mamlaka kwa Mahakama kuharibu mitego baada ya Mahakama kukata shauri. Hivyo mitego mingi ambayo inachomwa moto na Wizara yangu kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kama ambavyo inaonekana ZBC, Star TV, na TV nyenginezo ilikuwa ni kwa amri ya Mahakama na si vyenginevyo.

Kifungu 35 ambacho kimempa mamlaka Mkurugenzi wa Uvuvi kuharibu mitego ikiwa muhusika mwenyewe aliyekamata akitaka kesi yake nje ya Mahakama kwa uthibitisho rasmi na barua atakayoandika na kukubali makosa yake mwenyewe. Kwa hivyo uwezekano wa nje ya Mahakama upo.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya Mahakama nilizonazo hapa ikiwa ni vielelezo ambavyo vimeandikwa na wavuvi kuthibitisha makosa yao na kwa mitego isiyofaa hutakiwa wao wenyewe kuharibu au kuvichoma moto.

Mhe. Naibu Spika, kwenye vipengele vyote viwili hivi mvuvi huyo huwa hastahiki kupewa nyenzo mbadala kutokana na kwamba amekamatwa kwa maana nyengine. Nyenzo mbadala zilikuwa zikitolewa kwa yule atakayewasilisha mitego yake Afisini. Ukiwasilisha utapata njia mbadala bila ya kukamatwa. Aidha nyenzo hizi mbadala zilikuwa zikitolewa na mradi wa MACEMP ambao hivi sasa hauna tena fedha za kutoa nyenzo mbadala.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi aliendelea na hoja yake ya pili, elimu inahitajika zaidi ya wakulima na wakusanyaji wa mwani. Mahitaji ya boti ya kubebea boti imefikia hatua gani. Suala la kujenga kituo cha utafiti huko Shamiani Mwambe.

Wizara kupitia Idara ya Mazao Baharini itaendelea kutoa elimu ya ukulima wa mwani, ukaushaji wa mwani ili kuimarisha ubora wa mwani na kuimarisha soko. Tutashajihisha Kampuni za Mwani zenye huduma ya kutoa boti kwa wakulima wa mwani kufanya hivyo kwa mujibu wa makubaliano yao. Aidha Wizara itakapopata uwezo wa kibajeti pia tutasaidia wakulima.

Mhe. Mohammed Said Mohammed ametoa ushauri na wizara imeuchukua na itaufanyia kazi na tunakushukuru sana. Hoja yake ya pili ni kwamba lini tutaanza mitaala ya uvuvi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli tulikuwa tuna Chuo cha Uvuvi ambacho hivi sasa hakipo. Wizara yangu imekwishawasiliana na Idara ya Vyuo vya Amali na katika ya Bajeti ya mwaka 2012/2013, tutashirikiana na kuanzisha Mitaala ya uvuvi endelevu utakaosomesha katika Vyuo vya Amali, Vitongoji na Mkokotoni.

Mhe. Abdalla Mohammed na yeye alihoji kifungu cha umeme 220408 gharama za umeme kila Idara kimewekewa. Gharama za umeme zinajumuisha pamoja na vituo vya Wizara viliopo Wilayani, Mkoani, ambavyo vipo mbali na Wizara ambayo mwaka jana vilikuwa havijalipiwa.

Mhe. Nassor Said Salum na yeye alikuwa ana hoja kadhaa chumba cha kutundika nyama Kisakasaka kipo wapi. Chumba hichi kilitolewa kutokana na uchakavu wake na kuwa sio salama kwa matumizi. Wizara imepanga kuweka chumba chengine katika bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013.

Hoja yake ya pili kwa nini mradi wa mafua ya ndege bado upo na umewekewa bajeti wakati ugonjwa wa mafua ya ndege haupo hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mradi huu unashughulikia kuingia nchini mafua ya ndege na magonjwa yasiyo na mipaka. Mafua ya ndege hayapo hapa nchini lakini magonjwa haya mengine yapo hapa Zanzibar kama vile mahepe kwa kuku, ugonjwa wa miguu na midomo na ugonjwa wa ngozi kwa ng'ombe na kadhalika. Lengo kuu la mradi huu ni kupunguza na kuzuia uwezekano kwa magonjwa haya kuingia hapa Zanzibar.

Hoja yake ya pili je, kuna matibabu yeyote yanayotolewa kwa wanyama wanaoteswa. Mhe. Naibu Spika, ndio wanyama wanaoteswa hupatiwa matibabu katika kliniki zetu.
Hoja ya tatu gharama ya kupeleka umeme Kisakasaka, ilikuwa ni kiasi gani na ilipewa Kampuni gani. Mhe. Naibu Spika, gharama hizi ilikuwa ni shilingi 50 milioni na Kampuni ya Usaju limited ilipewa kazi hiyo.

Hoja yake ya nne ni lini mchakato wa Tumka utakamilika. Kanuni za maeneo mapya ikiwemo Tumka tayari zimeshapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Asha Abdu na yeye vile vile, mwani kampuni zinaongeza bei hadi kufikia 1500 kwa kilo. Kuhusu bei ya mwani ni kama nilivyokwisha kutoa maelezo kwamba tutashirikiana na Wizara ya Biashara na Kampuni za Mwani kuangalia muafaka wa bei ya mwani. Aidha tutaendelea kuhamasisha matumizi ya mwani kwa soko la ndani kwa matumizi ya chakula na vipodozi.
Hoja yake ya pili ufugaji wa samaki Shungi, Mhe. Waziri atatusaidiaje. Jawabu ni kwamba kuhusu ufugaji wa samaki Shungi nimefikia eneo hilo na nashirikiana na wafugaji hao kwa ukaribu sana na yeye mwenyewe analielewa hilo.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali aliuliza je, hakuna haja ya kuwepo mtaalamu wa ngazi ya *Masters* Pemba, Mhe. Waziri una mpango gani. Ipo haja na hivi sasa wapo wafanyakazi wanaoendelea na mafunzo hayo ambao ni hawa wafuatao:-

1. Ndugu Mohammed Zamir; anamaliza mwezi wa Septemba 2012 na atafanya kazi Idara ya Mipango Sera na Utafiti Pemba.

2. Ndugu Mayasa Ali Hamad; anatarajiwa kuanza mafunzo ya *Master* kozi ya *Environmental Studies* katika Chuo cha *Open University* kwa mwezi wa Agosti 2012.

Mhe. Salim Abdallah na yeye alikuwa na hoja kadhaa, maeneo ya karantini na uvamizi wa Kisakasaka maeneo mapya ya Unguja na Pemba. Karantini ya Kisakasaka inaendelea kutafutiwa hati miliki ili upatikane uwezo wa kisheria kuwahamisha wavamizi. Kisakasaka inahudumia ukanda wa Dar-es-Salaam na pwani. Maeneo mapya yanahitajika ili kuudhibiti ukubwa wa mifugo inayoingizwa nchini ufanyike kwa lengo la kupunguza uagiziaji wa mifugo nchini mwetu kwa njia ya malengo ambapo uingizwaji wa maradhi kutoka nje ya nchi utapungua. Vile vile ukusanyaji wa mapato utaongezeka tokea mifugo inayoingizwa nchini.

Kwa upande wa Pemba nzi wengi Gando na Donge, Mwanda yanatarajiwa kuwa maeneo mapya ya karantini.
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na yeye alikuwa na hoja kadhaa, wakati wa Pindua Wimbi, mabwawa au matuta yanakatika na kupoteza au kukimbia kwa samaki. Je, Wizara itatumia njia gani na kuweza kuwasaidia wafugaji hao na hali hii ya Pindua Wimbi.

Wizara inaendelea kutoa taaluma zaidi ya ujengaji bora wa mabwawa ya ufugaji, na pia wizara imejenga mabwawa ya mfano ili wafugaji kwenda kuona mabwawa hayo ya mfano ili wafugaji waweze kujenga mabwawa kama hayo. Aidha wizara kupitia Mazao ya Baharini inawachukua wafugaji hao kwenda kuona na kujifunza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo nachukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia hoja hii na wale waliotoa ushauri nawahakikishia kuwa ushauri wao tutauzingatia kwa manufaa ya wadau wote wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Naibu Spika, namba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale waliokubali hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013, anyooshe Mkono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)
(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya Bajeti ya Wizara sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 22 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0012 Idara ya Mazao Baharini Pemba	shs.15, 000,000/=
Kifungu 0014 Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo Pemba	shs.12, 000,000/=
Kifungu 0015 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba	shs. 6,000,000/=
Kifungu 0016 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja	shs.2, 107,000,000/=
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	shs. 6,000,000/=
Kifungu 0601 Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja	shs.59, 000,000/=
Kifungu 0701 Idara ya Mazao Baharini Unguja	shs.70, 000,000/=
Kifungu 0801 Idara ya Uzalishaji wa Wanyama	shs.15, 000,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.2, 290,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote

Kifungu 0010 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mwenyekiti, nilizungumza kuhusu kesi ya wavuvi wa Chwaka.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hapa Pemba

Kifungu 0010 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Pemba	shs.54.646,000/=
Kifungu 0011 Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba	shs.581, 700,000/=
Kifungu 0012 Idara ya Mazao Baharini Pemba	shs.77, 112,000/=
Kifungu 0013 Idara ya Uzalishaji Wanyama Pemba	shs.64, 600,000/=
Kifungu 0014 Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo Pemba	

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia nilihoji hatma ya mashamba ya mifugo kama vile lilioko Chamanangwe. Mhe. Waziri akaniambia kwamba shamba lile sasa hivi lipo kwenye idara yake, mengine yamepelekwa ZSTC na sehemu nyengine.

Hili katwambia kwamba anatumia kuhusiana na utafiti. Sasa hebu atwambie ana wanyama wanyama pale na ana laboratory ya kiwango gani ambayo hutumia kwa kufanyia utafiti.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali lake Mhe. Mwakilishi.

Kama nilivyoeleza awali kwamba shamba lile tunalo sisi wenyewe na tunakusudia kulifanyia kazi. Hivi sasa siwezi kumwambia ni ng'ombe wangapi, nitamjibu hilo

lakini wapo ng'ombe na vile vile nitamueleza kiasi gani tumefikia juu ya shamba hilo, lakini afahamu tu kwamba shamba tunalo wenyewe na tuna mpango mkubwa tu wa kuliendeleza shamba lile kwa sababu tuna imani kuwa litaleta faida kubwa hasa kwa upande wa Pemba na ndio maana hatukulitoa hili.

Naomba Mhe. Mwakilishi aridhike na anikubalie. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu laboratory ipo,

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Eeh! *Laboratory*

Mhe. Mwenyekiti: Kauliza na *laboratory* ipo pale kwenye shamba lile

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: *Laboratory*? Eeh! Laboratory ipo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mheshimiwa anatwambia kwamba baadae atatujibu lakini hili fungu tunataka kulipitisha hivi sasa. Sasa sijui muongozo wako unakuwaje tusubiri baadae basi na sisi tuje tupitisha fungu.

Lakini sidhani kama pale hiyo laboratory na hao wanyama wapo. Sasa ninadhani Mhe. Waziri atuweke sawa ili tupate kuendelea katika hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri bado Mhe. Mjumbe ana wasi wasi wa kuwepo wanyama pale pamoja na hiyo laboratory yenyewe. Hebu mtoe wasi wasi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Mimi labda Mhe. Mwenyekiti, nimuondoshee wasi wasi Mhe. Mwakilishi na kama nilivyomueleza kwamba awache tupitishe hiki kifungu ajenge imani kwamba siwezi kumdanganya kabisa. Baadae tutamletea hiyo takwimu kama tuna ng'ombe wangapi na kiasi tutafikia malengo yetu.

Naomba mheshimiwa uniamini.

Mhe. Mwenyekiti: Anaomba umuamini wanyama wapo, lab ipo na baadae mutazungumza zaidi kwa sababu hakujitayarisha kujua kuna ng'ombe wangapi sasa hivi wapo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tuendelee.

Mhe. Omar Ali Shehe: Subiri Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! malizia.

Mhe. Omar Ali Shehe: Lakini Mwenyekiti, hapa tunafanyakazi kubwa sana ya kupitisha mafungu. Naiomba serikali iwe makini sana kwa sababu hatuwezi kupitisha

mafungu kwa kitu ambacho hakipo na kitu kama hiki kwa kweli serikali itakapokuja hapa mbele yetu na kuomba fedha, kwa kweli iwe na majibu kamili.

Leo kwa sababu ya Mhe. Jihad kutokana na upya wake katika wizara, ninasema tuendelee lakini mara nyengine katika hili hatuwezi tukalikubali kwa kweli. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante ujumbe umefika serikalini. Tunaendelea.

Kifungu 0014 Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo Pemba	shs.63, 600,000/=
Kifungu 0015 Idara ya Maendeleo ya Uvivu Pemba	shs.68, 648,000/=
Kifungu 0016	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kupata ufafanuzi hasa kwa kilio cha wananchi wa Marumbi, kile nilichokuwa nikikizungumza nilipokuwa nikichangia.

Kwanza tunashukuru sana Idara ya Uvuvi inavyofanya kazi hasa kupitia miradi ya MACEMP. Tumeshuhudia wananchi wetu wengi ambao walikuwa wanafanya kazi zao kinyume cha taratibu, walikuwa wanazuiliwa nyavu zao, zinachomwa moto lakini baadae huwa wanapewa nyengine.

Lakini wananchi wangu hawa wa Marumbi ingawa mimi pengine labda kwa hoja hii wanaweza wakanitaka huko baadae nikagombee jimbo, samahani ninamtania rafiki yangu. Lakini kubwa zaidi tulikuwa tunataka maelezo, wananchi hawa wa Marumbi, wao hawakukamatwa na Idara ya Uvuvi, lakini wao walipata hujuma kutoka kwa wananchi wenziwao, wamechomewa maboti yao na nyavu zao.

Sasa sijui ile huruma ya wizara kuhusi kupitia Idara ya Uvuvi ili kuwaangalia wananchi wetu wale, kwa sababu hivi sasa na ukiangalia mwezi huu wa Ramadhani wameshaathirika sana, hawapati kwenda baharini na kufanya shughuli zao.

Jee, wizara itaweza kuwasaidia vipi wananchi hao. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusiana na suala la Marumbi.

Ni kweli kulikuwa na mgogoro na kwa kweli mgogoro huo mimi mwenyewe binafsi nilikwenda pale na nikazungumza na kamati zote mbili za uvuvi wa Chwaka na Marumbi, na tukafikia muafaka mzuri tu.

Tulikwenda kuweka maboya ili kuona ile mipaka ya hifadhi na tulikwenda sote kwa pamoja boti mbili mimi na watu wa Chwaka na Marumbi na tukakubaliana vizuri, na kwa kweli kila upande uliridhika na baada ya hapo tukafanya mazungumzo na kila mmoja akatoa dukuduku lake.

Upande wa Chwaka tukazungumza, upande wa Marumbi tukazungumza. Kama wizara kwa sababu nia yetu ni kuwaendeleza wavuvi wetu ili kuwaondoshea umaskini na sio kuwakomoa kama inavyofahamika.

Kwa kweli waliridhika na hilo na tukasema yale matatizo yote ambayo yanayohusu watu wa Chwaka na wale yanayohusu watu wa Marumbi basi tutakaa pamoja hakuna kisichozungumzika. Kwa sababu munapofikia suluhu basi kuna baadhi ya mambo huwa munayasamehe ni kawaida.

Kwa hivyo Mhe. Hamza ninachokuahidi tu kwamba nitakwenda tena kule kukutana na watu wa Marumbi na Chwaka ili tuone namna gani ya kuwasaidia wale, na tuna mpango mzima hapa wa kuwasaidia hususan watu wa Marumbi na Chwaka na zaidi kuwachukua wale vijana kuanza kuwapeleka Uchina kwenda kujifunza njia mbadala ya uvuvi huo.

Kwa hivyo Mhe. Hamza ninakuomba tu uwe na subra, mwelekeo sio mbaya kama hivyo unavyofikiriwa isipokuwa ni watu wawili watatu wenye maslahi yao kibinafsi ambao ndio wanaovuruga, lakini tumefikia pahala pazuri na tutawasaidia ipasavyo.

Hata Mhe. Rais alipokwenda na suala hili vile vile aliniuliza na akaniambia basi lishughulikie sana na jaribu sana kuwatizama kuwashirikisha katika kila hali ya maendeleo ili watu waondokane na migogoro, kwa sababu sisi wenyewe tumechoka na migogoro. Kwa hivyo Mhe. Hamza ninakuomba uwe na subra, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo sana na kauli ya Mhe. Waziri. Tatizo langu ni hali ya wananchi kuendelea kusota na umaskini na suala hili Mhe. Mwenyekiti, hata mimi kamati yangu kwa bahati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa tuliwahi kuletewa kesi, na kweli kuna tatizo baina ya watu wa Chwaka na Marumbi.

Ukiangalia wote matatizo yao yanalingana. Hata suala alilolizungumza Mhe. Subeit jana pia tuliwahi kulizungumza, lakini tatizo kwamba wizara inachukua muda mrefu kuweza kutekeleza zile ahadi ambazo inazozifanya.

Mfano, kama suala alilolizungumza Mhe. Subeit jana, Idara ya Uvuvi tayari baada ya amri ya Mahakama ilikwishakutoa ruhusa kwamba Mahakama ifanye utaratibu na bahati mbaya hivi sasa Mwanasheria Mkuu hayupo ambalo angelitusaidia zaidi au Waziri wa Sheria, kwamba tayari Idara ya Uvuvi wao walikwishakukubali kuwarejeshea nyavu zao watu wa Chwaka, lakini mpaka leo hakuna muongozo wowote wa kuweza kuwarejesha kwa sababu jambo kama limeshafika Mahakamani ni lazima liende na utaratibu.

Sasa utakuta watu wa Chwaka wamekwama nyavu zao zimezuiwa, Idara ya Uvuvi imeshakubali kuwapa lakini hakuna muongozo kutoka Mahakamani au Polisi namna gani ya kuweza kuwapa. Lakini hawa watu wa Marumbi vile vile na wao ndio wamepata hasara, serikali inachukua muda mrefu.

Serikali kila inapochukua muda mrefu kuhusu kutatua suala lile, mimi sitaki tuje tumwambie Mhe. Jihad na yeye ameshindwa kuwasimamia watu wake na yeye awajue. Sasa kwa sababu kule Mkuu wa Wilaya kama mutakumbuka kesi ya Chwaka na Marumbi si ndogo haikuanza leo, Mkuu wa Wilaya ya kule ameshawahi kumwaga manyanga hadharani. Sasa hatutaki na Mhe. Waziri wetu yaje yamfike hayo.

Sasa mimi nilikuwa ninaomba tujitahidini kidogo alau mufanye haraka haraka kwa sababu watu wa Chwaka wanaumia na watu wa Marumbi wanaumia. Mhe. Waziri ukishanikubalia hilo kwamba mutalifanyia kazi kwa haraka sana na maamuzi yale yaliyokuwepo Mahakamani ambayo yameshatolewa hukumu na Mahakama yatekelezwe na watu wa Marumbi mutawafanya nini. Mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, itakuwa hakuna tatizo.

Nia yetu sote hapa ni kuwatetea wananchi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, nimekusikia Mhe. Hamza na kama unavyojua mimi si mtu matatizo kwa kweli, sana ninapenda suluhu. Kwa hivyo mimi ninachukulia ahadi na nitachukulia haraka sana suala hilo kuhakikisha kwamba watu wa Marumbi na Chwaka wanakaa salama usalimini na wanapata haki zao.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na vile vile nimshukuru Mhe. Hamza kwa kuileta hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu tatizo la Chwaka na Marumbi serikali imeona umuhimu wa kulipatia ufumbuzi wa kudumu na hivi sasa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ana mpango wa kukutana na wavuvi wa sehemu hizo mbili ili tatizo hili liweze kumalizika na waweze kukaa kwa salama.

Ni hivi karibuni atakwenda na yapo mambo mazuri watafanyiwa wavuvi wetu hawa ili waendelee kufanya shughuli zao kwa vizuri zaidi. (*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema kuhusu Jimbo la Muyuni wamenyang'anywa boti yao na ikapelekwa Kizimkazi. Sasa sijui Mhe. Waziri alipokuwa akitoa majumuisho aliwahi kunijibu au nilikuwa sipo mimi, nilikuwa ninataka ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninakumbuka nilipokuwa ninatoa majumuisho yangu na nikasema bahati mbaya Mhe. Jaku alikuwa hayapo na hii kwa kweli wakati mwengine inakuwa inaturejesha nyuma.

Kwa kweli tulisema kwamba kule kilichotokea pale wanakijiji wako pale walikuwa wanagombana. Kwa hivyo tukasema kama sababu ni boti, wacha tuiondoe kwanza na ipo Kizimkazi haitumiki ipo ofisini mpaka hapo wanakijiji hao watafahamiana ndipo tutawarejeshea.

Kwa taarifa ni kwamba tayari inaonekana kuwa kuna mafahamiano mazuri. Kwa hivyo tunachokuomba Mhe. Jaku ushirikiane na wanakijiji pamoja na mimi mwenyewe ili twende tukawakabidhi boti hiyo. Kwa hivyo Mhe. Jaku nakuomba tushirikiane. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tuendelee.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Jana wakati ninachangia nilizungumza kuhusu wananchi wa Paje na nyavu na hadi hii leo hawajapelekewa nyavu hizo. Ninamuuliza Mhe. Waziri jee, nyavu hizo watapelekewa lini ili waendelee na kazi yao.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kwamba tunaofidia ni wale ambao wamesalimisha. Sasa sijui kama watu wa Paje walisalimisha kwa hiyari zao au walinyang'anywa.

Kama walinyang'anywa basi itakuwa ni vigumu lakini kama wamesalimisha basi nitafuatilia hili suala ahlani nihakikishe kwamba tunawapa vifaa vyao ili nao wawafaidike na uvuvi huo. Ahsante.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, walisalimisha.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Mhe. Mwenyekiti, kama wamesalimisha basi inshaallah tuwe na subra na nitalifuatilia na nitawapa vifaa vyao. Ahsante.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, ninataka kujua ni lini wategemee kupelekewa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Mhe. Mwenyekiti, siwezi kusema ni lini hasa kwa sababu ni mambo ya kwenda kukaa kwanza turatibu sisi na wao, kwa hivyo mimi nimemwambia kwamba ahlani tukipata ushahidi wa kila kitu basi hatutochukua muda na tutakaa na Wakurugenzi wa Uvuvi tuone kwamba wanapata haki zao madam wamesalimisha kwa hiyari yao, hatuwezi kuwanyima haki yao. Ahsante.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyekiti, naona itakuwa kila siku kesho kesho, ningeomba anihakikishie kwamba ikiwa mwezi ujao nijue ili wananchi wangu hapa wanasikia kwamba waende ikiwa mwezi wa kumi, ikiwa mwezi wa kumi na moja na tarehe fulani lakini wananchi wajue, maana yake kila siku kesho kesho wameshachoka.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Mhe. Mwenyekiti, tupo hapa kuja kupitisha bajeti na hiyo mipango ya kuwafidia basi yote imo ndani ya bajeti hii. Kwa hivyo namuomba Mhe. Mjumbe tupitishe ili tulitekeleze haraka sana.

Kwa hivyo baada ya bajeti tu tutatekeleza.

Mhe. Asha Abdu Haji: Tuendelee nitafuatilia ahsante sana.

Kifungu 0016 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja shs.387, 498,000/=
Kifungu 0201

Mhe. Salmin Awadhi Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikitoa mchango wangu juu ya wizara hii nilizungumzia juu ya wasi wasi wangu na idadi ya tones za samaki ambazo Mhe. Waziri ametueleza, ametutolea takwimu hapa na takwimu ambazo nimekuwa na wasi wasi nazo na juu ya zoezi zima la ukusanyaji wa takwimu hizi.

Pamoja na maelezo kwamba ameeleza kuwa wana watu wao katika madiko mbali mbali ambao wanakusanya hizo takwimu. Sasa ninataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba mimi ni mnunuzi mkubwa sana wa samaki katika madiko mbali mbali, lakini utaratibu uliopo pale hauwawezeshi maofisa wake kuweza kukusanya takwimu za idadi ya samaki.

Kwa hivyo ninasema takwimu hizi sio sahihi na ukizingatia kwamba kwa mfano diko la Malindi ambalo kuna samaki ambao wanauzwa baharini, watu wanakwenda kununua samaki baharini wakisha wanakuja nao huku, wanazifuata boti baharini.

Sasa sijui takwimu hizo zitakuwa zinakusanywa vipi. Ninalotaka kumwambia Mhe. Waziri akubaliane na mimi kwamba takwimu hizi alizotuletea sio sahihi na kwa sababu kutokana na mazingira ya ukusanyaji wenyewe, lakini pia atueleze kwamba atapiga marufuku suala la kuuza samaki baharini jambo ambalo ni hatari na linaweza likaleta maafa badala yake samaki waje wauzwe huku kwenye madiko, badala ya baharini kama inavyofanyika pale Malindi.

Akikubaliana na hayo Mhe. Waziri basi hamna tatizo tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Umemfahamu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Eeh! kwa kiasi fulani nimemfahamu.

Kwanza nimeupokea ushauri wake huo kwamba kupiga marufuku kuuziana samaki baharini. Hilo inshaallah tutajitahidi kulipigia marufuku kwa sababu linatupotezea takwimu kama alivyosema ni kweli.

Lakini kwa upande wa takwimu sisi tunaamini kile ambacho tunakipokea kwa sababu tumeweka maafisa wetu pale na tunaamini kwamba mvuvi baada ya kwisha kumaliza shughli zake ni lazima aje dikoni. Sasa kama ile kama kenda nje ya diko kwa kweli

itakuwa ni matatizo mengine. Lakini mimi ninachukua ushauri wake tutajitahidi kujaribu kuhakikisha kwamba wavuvi wote wanakuja kuuza samaki zao dikoni badala ya kuuziana ndani ya bahari.

Kwa hivyo Mhe. Salmin ninakuomba uniridhie ndugu yako ili tutekeleze hayo majukumu pamoja. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri na nimuombe hili suala la upigaji marufuku wa kuuza samaki baharini, alifuatilie na alichukulie hatua kwa sababu linaweza likaleta athari. Lakini na hili jengine ambalo Mhe. Waziri amelizungumzia juu ya takwimu zinazoletwa na watu wao, mimi nimuombe Mhe. Waziri na Mawaziri wote wawe wafuatiliaji wa masuala hayo na kama Waheshimiwa Mawaziri watakuwa wanafuatilia kila jambo basi watagundua mambo mengi sana yanafanyika katika mawizara yao badala ya kukaa maofisini wakapokea taarifa kutoka kwa watendaji; hawa watendaji mara nyingi wanakuwa wanababaishababaisha.

Kwa hivyo Mhe. Waziri na Mawaziri wengine niwaombe wawe wawe wafuatiliaji badala ya kukaa ofisini, kuna mambo mengi yanafanyika ambayo wao wenyewe wanakuwa hawayajui. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio pahala pangu kwa sababu pale muliniambia kwamba ni Pemba, hapa si Pemba sasa.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilichangia nilitoa vielelezo vya Mahakama na nilimwambia Mhe. Waziri kama kuna barua iliyotolewa tarehe 9 mwezi wa pili na kuna barua iliyotolewa tarehe 23 mwezi wa tano.

Angalie difference hizo, mwezi wa pili na mwezi wa tano na hivi leo hivi sasa tupo katika mwezi wa nane, kesho tunaingia mwezi wa nane na Mahakama imeshatoa maamuzi kama wapewe vitu vyao. Sasa kulikuwa na uzito gani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aseme kama kulikuwa hawajakamilisha vielelezo. Vielelezo gani vya mwaka mzima vilivyokuwa havipatikani na wakati Chwaka pale ni karibu.

Wananchi hawa wamechukuliwa vifaa vyao, watu wanataka wafanye kazi wapate risiki na watoto wao na Mahakama imeshaamua hawapewi, kulikuwa kuna matatizo gani. Mhe. Waziri aseme hivyo vifaa vilivyokuwa havijakamilika ni utaratibu gani.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri katika majumuisho yangu nilieleza hii hali halisi, hii kesi kweli ipo na hati zote ninazo hapa zinazohusiana na kesi hiyo. Labda nimsomee tu kidogo aone kwamba wapi tulifikia.

Nilisema tu kurejesha vifaa vilivyokamatwa kama vielelezo vya kesi ya Bwana Abdalla Makame Mweleza. Kwa heshima naomba uhusike na mada ya hapo juu, rejea barua yako yenye kumbukumbu hiyo hapo tarehe 23 mwezi wa tano 2012.

Washtakiwa hao walikamatwa katika eneo la Mfumbwi Chwaka. Vifaa vilivyokamatwa navyo ni nyavu ambayo ni kinyume na kifungu cha hiyo, vioo, samaki ambao baada ya Mahakama kuwatizama wakaharibiwa, madau sita. Kwa hivyo Mahakama imeamuru idara irejeshe vifaa hivyo haramu kwa wahusika, hivyo tunawaomba Mahakama itupatie muongozo wa kukabidhi vifaa hivyo kwa wahusika ili kuepukana na utata unaoweza kujitokeza.

Hii ni hatua ambayo tumeweza kuichukua baada ya kuheshimu maamuzi ya Mahakama lakini mambo ya kukabidhiana yana taratibu zake, huwezi kwenda tu ukampa kwa sababu leo na kesho anaweza kukwambia kitu fulani hamna. Lakini Mahakama ndio waliotoa maamuzi wanakuja pale tukakabidhiana kuhakikisha kwamba vitu vyote ambavyo wamekamatwa navyo vipo sahihi na sio sisi tunaocheleweshа hii process ni Mahakama.

Ni lazima tukubaliane kwamba process za Mahakama na tumezilaumu sana hapa zinachukua muda mrefu, na sisi tulipokata rufaa hii tumechukua muda mrefu hajajibiwa mpaka leo. Kwa hivyo na sisi tunalalamiko hivyo hivyo kwamba Mahakama kwa kweli kutoa maamuzi ni binde kwa kweli.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo Mhe. Subeit ninachokuahidi kwamba tumalize bajeti hii inshaallah tutashirikiana mimi na wewe, tutakwenda Mahakamani kuwaambia jamani kuna nini.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mhe. Waziri lakini Mahakama hiyo yenyewe ndio iliyotoa barua kama wakabidhiwe. Sasa huu utaratibu wa kuwa Mahakama imeshatoa barua kumpa mkurugenzi au muhusika yeyote yule kama wakabidhi na muna maelezo ya kuwa hakuna rufaa yoyote, muda wa rufaa umeshapita.

Kwa hivyo ukiangalia kama hakuna tena muda wa rufaa, hivyo natoa barua hii ili wakabidhiwe vitu vyao. Sasa utaratibu gani tena baada ya hivyo, ndio ninavyouliza ni utaratibu gani na barua zote hizi mbili za Mahakama; kuna barua ya tarehe 23 na kuna barua ya tarehe 9 mwezi pili inayotoa maamuzi ya kuwa wapewe vifaa vyao baada ya kuona kama kesi hawana na upelelezi wote umekwisha.

Na kuna barua iliyotolewa kwa mara ya pili tarehe 23 mwezi wa tano kuwaambiwa kama wapewe tena nyavu 47, vioo 16, samaki wao; samaki hawapatikani tena wameshaliwa, lakini na madau 6 wapewe.

Sasa kitu gani ushahidi gani na vifaa vyote hivi na Mahakama hizi karatasi zao. Sasa Mhe.Waziri akiniambia twende Mahakamani mimi na yeye tukafanye utaratibu gani na wao tayari barua zao wameshakamilisha.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninadhani hata mimi nilipokuwa nikichangia nililizungumza suala hili. Mheshimiwa hapa ni suala la Mahakama wao

kwa sababu wao wameshatoa barua lakini unapotoa kitu huwezi kwamba mtu hakuna ushahidi wowote, kwa hivyo ni lazima iwepo Mahakama, wawepo na watu wa Idara ya Uvuvi na wenyewe wahusika.

Sasa hili ndio maana nilipokuwa nikitoa ile hoja yangu nikasema angelikuwepo Mwanasheria Mkuu au Waziri wa Sheria, wao ndio wangetoa ahadi lini Mahakama itakwenda Idara ya Uvuvi ili kuwaitwa wananchi kuwakabidhi vitu vyao, mimi ninafikiri huo ndio utaratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo mazuri. Aidha nimshukuru Mhe. Hamza kwa ufafanuzi mzuri lakini pia nimshukuru sana ndugu Mhe. Subeit kwa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu wa Mahakama pale ambapo inatolewa hukumu na utekelezaji wake haujafanyika muhusika anatakiwa kwenda Mahakamani kwa ajili ya kazi ya hukumu ile ili utekelezaji ufanyike kwa wakati. Kwa hivyo wananchi kule wanahyo haki ama Mhe. Subeit kwa niaba ya wananchi anayo haki ya kwenda Mahakamani ili Mahakama kwa sababu Mhe. Waziri ameeleza hapa kuna mambo mengine yanahitaji utaratibu wa Kimahakama ili ukamilishaji wa hayo mambo yaende sahihi ili wananchi hao wapate vifaa vyao.

Kwa hivyo kunapotokea ucheleweshaji wa namna hiyo, wananchi wanayo haki ya kwenda Mahakamani kwa ajili ya kukatizia hukumu ile ili utaratibu ule ukamilike kama ulivyopangwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, huo ndio utaratibu mzuri na si vizuri sisi hapa ndani ya Baraza lako tukufu kuyatolea majibu mambo ya Mahakama, kwa sababu tutakuwa tunaingilia *process* za Mahakama.

Kwa hivyo kwa kifupi ningemuomba sana Mhe. Mwakilishi ashirikiane na wananchi waende Mahakamani kuliulizia tena jambo hili ili taratibu za kimahkama zifanyike na vifaa vile wakabidhiwe. Kwa sababu wizara wako tayari kukabidhi vifaa vile, sasa cha msingi hapa ni kukazia hukumu iliyotolewa na Mahkama ili hatua ziendelee na sisi kama Baraza hatuna uwezo wa kuingilia uamuzi wa Mahkama.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali lakini twende pamoja na hao wahusika wa hii kesi.

Mhe. Mwenyekiti: Waziri kakubali mtashirikiana juu ya suala hilo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia masuala ya mashamba lakini moja Mhe. Waziri amenijibu vizuri la Pangeni, sasa nilikuwa nataka nijue na hili la Bambi. Nilisema kuwa mara nyingi sana watu wa Wizara ya Kilimo mashamba mengi sana wameyaachia hilo moja nashukuru sana, sasa na hili ningeomba iwe maalum kuwa na wao watu wa Bambi waachiwe shamba hili, nao kwa kufanya miradi yao ili kuondoa umasikini kutokana na shamba

hilo. Naomba sana hilo anihakikishie jibu liwe zuri halafu mimi nimuachie ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Mjumbe nimesikia ombi lake. Kwa hivyo ni suala ambalo linazungumzika kwa kweli, acha tupitishe bajeti tutatizama uwezekano, na sio wa mwanzo kufanya hivyo wengine tumeshafanya. Kwa hivyo hata na wao tunaweza tukawasabilia tukawaambia basi tumieni sehemu kadhaa au eka ngapi zilizobakia tuachieni. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe acha tulitizame hilo suala baada ya bajeti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana nae Waziri lakini kwa namna moja, kwa sababu kuna kipindi fulani alinambia maneno kama hayo mazuri, matamu kuhusu habari ya uchaguzi wa vijana wa riadha, hatimaye jambo likaisha nikaja nikamkamata Waziri mwengine. Sasa mimi ningeomba twende kunako *hansard* yetu iwe nzuri, anambie ikisha bajeti njoo ofisini twende tukawasaidie wananchi wetu hawa hilo mimi nitakubaliana nalo, lakini anambie kuwa linasemezeka tuangalie bado nitakuwa mgumu wa kifungu hiki.

Ili nisiwe na wasiwasi Mhe. Mwenyekiti, mara hii anishirikishe hasa mimi na yeye tukae twende tukapange tuwapelekee wananchi, kwa sababu wananchi wa Bambi sasa hivi hawana pa kulima, hatari iliyoko kule wanagombana na JKU, wananchi wanatishiwa mabunduki, wanadhalilishwa. Sasa mimi nataka hili suala liondoke kabisa ajisafishe Mhe. Waziri wangu kuwa hili suala mimi na yeye twende bega kwa bega kama waziri anayemnong'oneza hapo alinambia hivyo hivyo, ikisha bajeti nende nikakae nae pamoja tulipange. Sasa na mimi naomba na hilo tukae vizuri tukapange.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante tutakaa tutapanga halafu kwa kushauriana na ofisi yangu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, hakuna tatizo lolote naomba tuendelee.

Kifungu 0201 – Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	239,001,000
Kifungu 0401 – Idara ya Uendeshaji na Utumishi	585,412,000
Kifungu 0601	

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimepiga sana buti langu lakini hulisikii. Wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia shamba la mifugo la Tunguu, na nikajenga mashaka juu ya wajanja wachache waliochukua hekta karibuni 1,000 na kubakishwa hekta 50 ambazo zinaonekana nazo pia zina mashaka. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri wakati ananijibu alinieleza kwamba walifikia pahala kwamba shamba walihisi wao hawana mahitaji nalo wamelirejesha ardhi. Mimi nakubaliana naye lakini bado mashaka yangu yangalipo katika shamba hili kwamba limechukuliwa na wajanja pasipo na utaratibu, na halitumiki katika hali halisi ya kinadharia ile ambayo imekusudiwa. Sasa hili sitaki Mhe. Waziri alijibu nataka wewe Mhe. Mwenyekiti ulichukue uliingize katika Kamati Teule iliyoundwa wakati wa hotuba ya ardhi wende wakalifanyie kazi. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba taarifa zako.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tumelichukua tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hili suala alilolizungumzia Mhe. Ali Salum Haji, Mwakilishi wa Kwahani, Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako tukufu hili lilishapitisha uamuzi wa Kamati Teule na zile hadidu rejea zimeshatolewa na Spika, kwa hivyo suala hilo nafikiri mjadala ule wa kamati teule umeshafungwa kwa shughuli zake zile. Kwa jambo hili Mhe. Mwakilishi angependa apate majibu kutoka kwa Mhe. Waziri ili amueleweshe hatua zinazochukuliwa kuhusu suala la shamba lakini si kwa kuingizwa kwenye Kamati Teule.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hadidu rejea zimeshatolewa katika kazi, kwa hivyo hii haiwezi kuongezeka naomba umsikilize Waziri majibu yake.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Sijamfahamu aseme tena.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia hofu yangu juu ya Shamba la Mifugo la Tunguu, na nikaelezea kwamba kuna hekta karibuni 1,000 zimechukuliwa na wajanja za shamba hilo la mifugo. Mhe. Waziri wakati anakuja kujibu kajibu kuwa *concern* yao kwamba hawakutaka kuliendeleza kutokana na matatizo ya kuwa mifugo hawana, lakini hili shamba bado linalalamikiwa. Na yeye akasema baada ya kuhisi kwamba wao hawana mahitaji nalo wamelirejesha ardhi, hilo ndio jawabu lake. Lakini sasa kama limerejeshwa ardhi mimi bado nina hofu katika hili kwa sababu hili shamba lilikuwa la mifugo, na ninahisi limechukuliwa na wajanja, ndio maana nikaeleza kuwa kama limechukuliwa na wajanja na tayari kuna Kamati Teule iliundwa kwa sababu ya kuchunguza masuala haya, ndio nikakuomba wewe Mwenyekiti na hili liingizwe ili likafanyiwe kazi kujua nani kachukua na kwa malengo gani.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nafikiri cha msingi hapa kwa sababu nimeshajibu kwamba hili suala haliko mikononi mwetu, kwa hivyo labda ningemuomba Mhe. Mjumbe a-*rise concern* yake, aende Wizara ya Ardhi na ajaribu kufuatilia hilo suala ili kuona kama kuna wajanja au laa. Kwa sababu mimi tena sina uhalali wa kulijibu hili suala wakati haliko ndani ya mikono yangu. Kwa hivyo nakuomba Mhe. Mjumbe ufanye hivyo.

UTARATIBU

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais amezungumza kwamba kuna *terms of reference* za Kamati Teule zimeshapitishwa hapa kitu ambacho hatukumbuki hicho. Si sahihi maelezo yake, hatujapitisha *terms of reference* za Kamati Teule. Kwa hivyo, mimi ningeomba hili kwanza tufute kwenye *hansard* kwamba halimo si sahihi maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, maneno yangu ni sahihi kwa kuwa mara baada ya Baraza hili linapoamua kuundwa

Kamati Teule juu ya jambo fulani, Mhe. Spika, hutoa muongozo maalum wa jambo hilo kushughulikiwa na Kamati Teule ile. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana hata ukikumbuka Kamati Teule iliyokwisha ilipoleta ripoti yake jambo hili tulilizungumza sana. Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa aelewe kwamba hadidu rejea za Kamati Teule ile zimetolewa na sasa Kamati Teule inatakiwa kuanza kazi zake kwa sababu ya kutekeleza wajibu ulioelekezwa na Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani nisaidie tukimaliza bajeti yetu kuna kazi za kamati, nadhani kamati inayohusika tutaituma ikafanye kazi hiyo kwa niaba ya Baraza.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuchukua busara zako mimi bado sijajitosheleza katika nafsi yangu. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Mhe Waziri kaitupia Wizara ya Ardhi, lakini ninachotaka kukizungumza mimi kwamba hili shamba lilikuwa la mifugo, na sababu ya kutupiwa mipira kupelekwa ardhi hapa ulitumika ujanja wa hili shamba kulihodhi, sasa kama kule wana hadidu rejea zao basi tuunde Kamati Teule kufuatilia hili shamba lililoporwa la mifugo ili serikali iangalie limechukuliwa kwa namna gani. Kwa sababu ile kulipeleka ardhi yenyewe natumai ni ujanja wa kutafuta njia ya kulihodhi pasipo na njia za utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani hatujapishana sana, ni hivi waziri halimo katika mikono yake sasa hivi, Baraza lishakubali kamati ikifanya kazi itakwenda kuchunguza halafu itatoa ripoti kwenye Baraza tatizo nini, na sisi tutakuja kusikiliza ripoti sote hapa, mtasoma ripoti yaliyoonekana halafu tutajadili kwenye Baraza naona hakuna tatizo.

Mhe. Ali Salum Ali: Ahsante kwa kulinda heshima ya kwamba somo yangu tuendelee.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia habari ya ufugaji wa samaki, na Mhe. Waziri alitoa ahadi, ufugaji wa mbuzi alitoa ahadi, lakini ahadi hizo bajeti iliyopita hazikutekelezwa. Namuomba Mhe. Waziri ni lini atatekeleza ahadi hizo alizowekewa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Kwa mbuzi nakubali lakini samaki hamna. Mbuzi tumekubaliana kwamba tutoe nusu kwa nusu, yeye atoe nusu na sisi tutoe nusu, lakini suala la samaki hatujakubaliana. Naomba ajaribu kuvuta kumbukumbu zake ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, namuomba hiyo ahadi ya mbuzi anipe inatosha.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo tuendelee?

Mhe. Hassan Hamad Omar: Hajanijibu ati.

Mhe. Mwenyekiti: Hajafahamu hebu eleza vizuri.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, naomba anijibu hiyo ahadi ya mbuzi ataitekeleza lini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, hamna shida baada ya yeye kuleta sehemu yake na mimi yangu nitatoa hamna shida.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0601 Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja 628,630,000
Kifungu 0701

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri pamoja na ustadi wake wa kujibu, nilisema sana kuhusu wananchi wetu hawa wanaopanda mwani kuwa wanapenda sana kudhalilishwa na hawa matajiri, na nikaelekeza kuwa serikali kwa nini isifanye jambo kwa makusudi ikawatafutia mashine za miradi midogo midogo ili waweze kujikimu kuondoa umasikini kuliko kupita katika migongo ya matajiri. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri alinijibu vizuri lakini na hili naomba anijibu vizuri ili kuwaokoa wananchi wetu wa kando kando za pwani na waweze kuzalisha mwani kwa wingi zaidi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na maoni ya Mhe. Mjumbe ni kwamba sisi tunazungumza na chombo kile cha Jumuia ya Wana Mwani (JUWAMWAZA), hicho ndicho tutakaa tutashirikiana namna gani ya kuwasaidia kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo; ili kuona kwamba na wao wanapata mashine za kusarifu mwani. Tumeona mifano kadhaa tuliyoelezwa humu Kidoti, Fumba, kwa hivyo na hili tutakaa na JUWAMWAZA ili tuone kwamba tunawasaidia kuwa na mashine za kusarifu mwani.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina matatizo na Mhe. Waziri, kwa sababu wananchi wa Kiwengwa wamenituma hivyo. Sasa na wao itakuwa bado hawajaanza kukaliwa kitako kwa hivyo nakupa taarifa na wao wanaomba sana nao uwajumuishe katika kukaa nao kitako ili kuweza kuwasaidia wananchi wa Kiwengwa. Naomba Mhe. Waziri kutokana na majibu yake mazuri tuendelee.

Kifungu 0701 Idara ya Mazao ya Baharini Unguja 206,653,000
Kifungu 0801

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilihoji juu ya hatma ya Shamba ya Makurunge, shamba ambalo tulipewa kwa ajili ya kuendeleza suala zima litokanalo na mifugo na wanyama wetu. Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya shamba ni hayo, kwamba Zanzibar tulipewa kwa ajili ya dhamira hiyo. Mhe. Waziri kajibu kuwa shamba lile sasa hivi liko kilimo, najua liko kilimo kwa sababu wakati tulipokubaliana kwamba suala lile sasa hivi lifanyiwe utaratibu ili Zanzibar ikabidhiwe hatimiliki, wakati ule wizara ilikuwa iko pamoja baina ya uvuvi pamoja na kilimo, lakini wamiliki hasa wa shamba lile ni Wizara ya Mifugo kwa sababu ndio dhamira hasa ya kuendeleza mifugo.

Sasa kwa kuwa taasisi iliyokabidhiwa iko mifugo, lakini shamba wenye hati ya umiliki ni Wizara ya Mifugo sijui Mhe. Waziri katika hili analifuatilia vipi kuziunganisha, ili

wizara yake pamoja na taasisi hii ya Kizimbani ionekane kwamba inafanikisha, halafu shamba lile walitumie kama wizara.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli si wazo baya acha nikae na Wizara ya Kilimo na Maliasili tuone utaratibu gani wa kufanya, kama kuna haja ya kulirejesha au bado wanataka kutumia nafikiri hakuna ubaya. Kwa hivyo acha nikae na Waziri wa Kilimo na tukikubaliana kurejesha basi litarudi kwenye milki yetu. Lakini kwa hivi sasa kama nilivyoeleza kwamba tumewapa wao, hivyo lazima kwanza nirudi kwao ili kuwaomba wakinikubalia basi tutachukua, kwa sababu nahitaji ardhi ya kuweza kuendeleza mifugo. Ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, ushauri umekubaliwa lakini katika kukubali ameonesha wasiwasi fulani hivi kwamba kukiwa kuna haja. Hivi serikali imeshafika hatua ya kuona kwamba hakuna haja ya shamba lile. Mimi nadhani umuhimu na haja ipo sasa ni kiasi tu cha Mhe. Waziri kukubali kwamba wizara yake itakaa pamoja na taasisi ile ya Kizimbani kuona kwamba wanaharakisha mchakato ili shamba lile lirudi katika mikono ya serikali, na wizara itumie kwa ajili ya kuendeleza mifugo. Nadhani si suala la kwamba *unless* serikali iamue vyenginevyo. Tusikie kauli ya serikali.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi tutakaa nao Wizara ya Kilimo ili tuone kwamba shamba lile linarudi katika milki yetu. Ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake mazuri Mhe. Waziri alinijibu vizuri lakini na mimi niliuliza suala la ng'ombe waliopelekewa watu wa Kitope ambao ni wabovu, na ambao tulitegemea kuwa watazalishwa ili wanyama wawe wengi. Lakini sasa nataka nimuulize hivi, ni nani anayekwenda kununua ng'ombe wale, wanakwenda kununua wenyewe wafugaji au kuna wataalamu ambao wanawapeleka. Ninaomba hapo kwanza anisaidie kama yupo mnunuaji maalum wa Wizara ndio mimi nitaweza kujua nini cha kufanya, la kama wanakwenda wenyewe vile vile Waziri niweze kumsamehe. Naomba jibu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni wizara ndio wanaonunua halafu wataalamu wetu wanawapelekea wakulima katika njia za kitaalamu kabisa. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri ni mpya lakini ingekuwa kama si mpya ningesema mimi sikubaliani nalo. Kwa sababu kama wizara kwa nini waende wakanunuliwe wananchi ng'ombe wabovu, hawaoni kama tunapoteza pesa za wafadhili. Lakini kwa kuwa yeye ni mpya naomba Mheshimiwa kuwa hili suala asilikubali tena, kwa sababu unapokwenda wizara tutafute wataalamu na twende tukatafute ng'ombe ambao wanakwenda na wakati, na yale maeneo yenyewe hususan kama huko Jimbo la Kitope wameingia hasara kubwa sana. Naomba

Mhe. Waziri usilirejee leo nakusamehe Waziri mpya, lakini mara nyengine nakuning'inia hapa. Tuendelee.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa mara nyengine tena. Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilichangia suala la kopa ng'ombe lipa ng'ombe, nilikuwa napata mashaka na mradi huu, na ndio maana nikamtaka Mhe. Waziri basi aniletee kima cha mradi ule ulipoanzishwa na faida yake, kaniletea dola laki moja na nusu na faida zilizopatikana kwa wakulima kuweza kuwawezesha pamoja na faida za maziwa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri mimi bado sijajiridhishwa katika hili, kwa sababu lengo la mradi ilikuwa kopa ng'ombe lipa ng'ombe na mradi huu kwa kipindi kirefu mimi sijauona kwenye vitabu vyake pia haumo. Mimi nataka anieleze huu mradi sasa hivi unasimamiwa na nani, tuna ng'ombe wangapi kwa kuweza kukopesha. Ninachokifahamu mimi labda Mhe. Waziri tumueleze kwa sababu yeye mpya tufike pahala tumuonee huruma watendaji wanamdanganya, hawa ng'ombe hawakuwa kopa ng'ombe lipa ng'ombe, hawa ng'ombe imekuwa chukua ng'ombe ukajitajirishe na vielelezo tunavyo, waliochukua ambao hawajarejesha. Sasa mimi anipe ufafanuzi mzuri halafu tufike pahala nijue nini cha kuendelea Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomueleza maelezo ni kama hayo lakini mwenyewe hakuridhika na anahisi labda ninadanganywa, wacha basi tupitishe bajeti na mimi nitalifuatilia kwa kina kabisa nione kama kweli nimedanganywa au laa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeridhika nayo kwa sababu nimesema zamani kwamba najua ni mpya na mimi nitamsaidia kumpa hivyo vielelezo. Ahsante.

Kifungu 0801 – Idara ya Uzalishaji wa Wanyama Unguja	571,500,000
Jumla ya Fungu:	**3,529,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 22 – WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0016 – Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia katika Idara hii ya Maendeleo ya Uvuvi nilizungumzia suala zima la kiwango cha fedha zilizotengwa katika mradi huu wa *MACEMP*, ni shilingi milioni mia moja tu fedha ambazo zinaonekana ni kidogo kuliko zile zilizotolewa na serikali mwaka jana. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alieleza kwamba wao wanatoa fedha kwa ajili ya vipaumbele. Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri je, hili suala la usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari kuu sasa katika ukanda wa pwani imekuwa sio kipaumbele. Na kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ni muhimu na kwa sababu unashughulikia suala zima la uhifadhi wa maeneo ya ukanda wa pwani, na tayari kuna

maeneo ya hifadhi na kwenye kitabu chake Mhe. Waziri ametupa malengo kumi ya mradi huu ambayo yanategemewa kutekelezwa katika kipindi hiki.

Sasa nataka kumuuliza katika haya malengo kumi ambayo amepanga humu kuyatekeleza. Je, hizi shilingi milioni mia moja kwa kweli zitatosha mpaka tufike pahala tuone kwamba suala la uhifadhi wa ukanda wa bahari kuu si muhimu. Kuna mambo mengi, kuna *activities* nyingi sana katika mradi huu. Kwa hivyo nataka atueleze Mhe. Waziri kwamba sasa kipaumbele katika eneo hili kwa kuwa mradi ule unaofadhiliwa na wahisani limekwisha.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza aelewe tu kwamba *activities* zote za mradi huu zinamalizika mwezi wa Ogasti, 2012. Kwa hivyo, fedha hii tumetenga kwa ajili ya ku-*sustain* huo mradi kwa vile Mradi wa *MACEMP* unamalizika Ogasti 31. kwa hivyo, tumeweka kifungu hicho kwa ajili yak u-*sustain* huo mradi ni fedha ambayo tunatoa na Bara huwa wanatoa vile vile, kwa hivyo ni kwa ajili ya *sustainability.*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Sikumuelewa vizuri Mhe. Waziri na kama nilivyomueleza ndivyo kwamba ni mradi ambao unamalizika mwezi wa Disemba kwa maana hiyo kuna fedha bado zipo kama sikosei ambazo zimetolewa na wafadhili. Lakini mbona fedha hizo kiwango hiki cha fedha hazikujitokeza humu kwenye bajeti hii ambazo nazo zilikuwa zinahitaji ziwemo katika hicho kiwango kilichokuwa kimebakia ambacho kinategemewa kutumika mpaka hapo ilikuwa kioneshe hapa. Kwa sababu fedha zote zinazotumiwa na serikali ni lazima zionekane katika kitabu hiki ili ziidhinishwe. Sasa fedha hizi zimebakia kiasi gani na zitaidhinishwa vipi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na maelezo mazuri aliyoyatoa Waziri wa Mifugo na Uvuvi ni kwamba mradi wa *MACEMP* unamaliza shughuli zake Agosti mwaka huu, na kwa kweli ulikuwa unamaliza mwezi huu wa Juni, lakini kukafanyika mashauriano ili fedha ambazo ziliombwa mwaka jana katika bajeti basi zimalizie. Kwa hivyo, mwaka huu hakukuwa na sababu tena ya kuomba tena fedha kwa sababu mradi wenyewe ndio unamaliza fedha ambazo zinatumiwa ni zile ambazo zimeombwa mwaka jana.

Kwa hivyo, Mradi wa *MACEMP* kimsingi umemaliza shughuli zake na fedha hizi shilingi milioni moja zilizowekwa hapa ni shughuli za *Marine Legacy Fund* ni pesa ambazo Zanzibar tunatoa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatoa na World Bank inatoa kwa ajili ya kusimamia shughuli ndogo ndogo za mazingira katika ukanda wa pwani. Kwa hivyo, hivi ndivyo ambavyo kwa nini shilingi milioni moja zimewekwa hapo ni kwa ajili ya ku *sustain* huo Mfuko ambao umewekwa kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza shughuli za nini. Lakini kimsingi hakukuwa na sababu tena ya kufanya bajeti kwa sababu shughuli za mradi zimemaliza.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri aliyepita ndio amenizonga kabisa na kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tokea huko awali tunakotoka fedha zilizokuwa zikitolewa na serikali tulikuwa tuna-*support* zile fedha zilizokuwa zikitolewa na wahisani. Fedha zilizokuwa zikitolewa na wahisani zilikuwa

zinaonekana humu ili zipitishwe, safari hii serikali imetoa shilingi milioni mia moja ambapo hakuna fedha za wahisani hapa, ambapo mradi unakamilika mwezi wa Agosti na tayari kuna malengo kumi ya kutekeleza mradi huu.

Sasa hebu tupewe taarifa vizuri ili tuweze kupitisha hili fungu, kwa sababu hakuna fedha za muhisani hapa ambazo zimepitishwa ni hizi, fedha hizi zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza malengo kumi ambayo mwaka huu tunategemea kuyatekeleza kupitia mradi huu. Mimi swali langu nimemuuliza ni swali jepesi tu, ni kujibu kwamba ah kipaumbele sasa hakipo basi au tusiwe na wasi wasi katika hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Labda Mhe. Mwakilishi hajafahamu vizuri, kimsingi ni kwamba mradi umemaliza shughuli zake na mwezi huu wa Juni ndio ilikuwa mradi kwa kweli unafunga vitabu. Sasa kuna fedha ambazo ziliombwa mwaka jana ambazo mara hii haziwezi tena kuombwa ndio ambazo zinamalizia hadi Agosti. Fedha hizi ambazo zimeombwa ni mchango wa Serikali ya Zanzibar kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uhifadhi unaitwa *Marine Legacy Fund;* ni mfuko ambao utaingizwa, sisi tutaingiza fungu letu ndio hizi ambazo tumeziomba, wenzetu wa Jamhuri ya Muungano na wao wataingiza, na wakishaona hivyo na wao kwanza sisi tuonekane ile *commitment* yetu baadae ndio wafadhili nao wataangalia kwa asilimia ambayo tuliingiza. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Mjumbe aelewe hivyo kwamba kipaumbele sasa hivi cha mradi huu ni ku-*sustain* shughuli za uhifadhi wa mazingira katika shughuli za kazi na ndio maana tunaomba hizi fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Habari na Mhe. Waziri wa Mifugo pamoja na masuala mazuri anayouliza Mhe. Mwakilishi. Kama nimemuelewa vizuri Mhe. Salmin pia alitaka kujua ni namna gani shughuli za ulinzi wa bahari kuu zitafanyika kwa fedha hizi, licha ya jitihada zinazofanyika katika kulinda maeneo yetu ya bahari ya ndani, lakini alitaka kujua je, kwenye bahari kuu tutafanya vipi kulinda shughuli zetu ili wavuvi pengine kutoka nje wasiweze kuvua humo na vile vile kusiweze kuharibiwa mazingira katika maeneo hayo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hii mamlaka inayosimamia uvuvi wa bahari kuu moja katika majukumu yake ni kuwemo pia suala la ulinzi katika maeneo ya bahari zetu. Kwa hivyo kwa vyovyote vile katika kufanya shughuli zao za kila siku, moja katika jukumu jengine ni kuhakikisha kwamba wanalinda maeneo yetu ya uvuvi kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya dola ili kuhakikisha kwamba katika maeneo haya ya bahari kuu pia watu hawayaingilii na kufanya vile wanavyoona wao wangependa wafanye, lakini zinafanyika shughuli kwa kufuata taratibu zilizowekwa na nchi yetu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, lengo la mradi huu wa *MACEMP* una malengo mengi, lakini kubwa ni usimamizi wa mazingira katika ukanda wa pwani pamoja na bahari kuu. Kama alivyoeleza Mhe. Waziri ni sawa kwamba suala la ulinzi wa bahari kuu utasimamiwa na mamlaka hii ya bahari kuu, na huwa wao Wizara wanatoa pesa kwa mujibu wa kipaumbele. Sasa mimi swali langu ni dogo tu jee kipaumbele katika eneo hili sasa limekwisha na kwa sababu tayari kuna maeneo haya

ambayo wao wametueleza kuna malengo kama kumi hivi ambayo yanatekelezwa, mbali ya huo ulinzi wa bahari kuu na nini ni katika huu usimamizi wa eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa nikichangia nilieleza wasiwasi wangu juu ya serikali kutoipa kipaumbele ile miradi ambayo tayari wahisani wameshaingiza fedha nyingi. Sasa inapomalizika ile miradi sasa serikali nayo wanaiacha solemba, matokeo yake inakuwa zile nguvu za wahisani zinapotea.

Sasa hapa inaonekana ni jinsi gani serikali ilivyokuwa haitoi kipaumbele kwa mradi huu ambao tayari umeshafadhiliwa kwa pesa nyingi tena za mkopo kutoka World Bank. Sasa hii Mhe. Naibu Spika, ni hatari na mimi niiombe serikali kwamba miradi kama hii itengewe fedha ili iwe endelevu, suala la uhifadhi wa maeneo haya ya ukanda wa pwani ni suala muhimu ambalo ni fedha nyingi zimekopwa kutoka World Bank.

Kwa hivyo kwa mara nyengine tena wakati wa bajeti zinazokuja tuzingatie haya kuliko kuyaacha haya. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tunaendelea serikali imesikia mchango wako. Tunaendelea.

Kifungu 0016 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja	shs.400, 000,000/=
Kifungu 0201 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	shs.200, 000,000/=
Kifungu	

Mhe. Mwenyekiti: Mjumbe wameshaitikia kimepita hicho, tizama chengine.

Kifungu 0601 Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wakati ninachangia kifungu hiki nilikuwa nimezungumzia masuala ya ugonjwa wa mafua ya ndege. Ninataka kujua tu Mhe. Waziri kwamba nilimuuliza ni utaratibu gani ambao wizara inajipanga katika kutoa elimu kwenye mafua ya ndege, kwa sababu ukizingatia Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa jirani zetu Uganda kuna mripuko wa ugonjwa wa Ebola na mtiririko huo huo na sisi ni majirani, kwa hivyo nilikuwa ninataka kujua tu Mhe. Waziri ni utaratibu gani amepanga katika kutoa elimu katika masuala ya ugonjwa wa mafua ya ndege.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo anifafanulie sijampata vizuri hasa amekusudia nini Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mwenyekiti: Rudia hoja yako.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia kwenye kifungu hiki nilizungumzia ugonjwa wa mafua ya ndege na katika kitabu chake ameweka bajeti pale, kwenye mwaka jana kulikuwa na milioni hamsini na tano na mwaka juu kuna milioni thamanini, kwa hivyo kutokana na tatizo la ugonjwa huu wa mafua ya ndege wizara yake imepanga vipi kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na tatizo ugonjwa

huu wa mafua ya ndege ukizingatia kwamba hivi sasa majirani zetu kama Uganda kuna mripuko wa ugonjwa wa Ebola, pengine katika kujikinga na mambo haya jee, wizara imejipanga vipi katika kutoa elimu kwa wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali imeunda kamati maalum ya kushughulikia mafua ya ndege. Kwa misingi huo tunapokea ushauri Mhe. Nassor ili hatua za kuelimisha umma ziendelee kwa nia ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa salama na maradhi hayo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ningeomba kwamba serikali ikafanya semina kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukajua hasa matatizo ya maradhi haya. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana serikali imesikia kwamba kwanza sadaka huanza nyumbani. Tunaendelea.

Kifungu 0601 Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja shs.229, 960,000/=
Kifungu 0701

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia suala la mwani nilisema kwamba suala hili ni kuwa lipo katika bei ya mwisho kwa kilo unaouzwa kwa bei ndogo, lakini Mhe. Waziri hakunihakikishia bei hii ya mwani ni lini itatangazwa hasa ikawa inafanana na bei ya vitu vyengine katika kilo.

Kwa sababu hata bei ya maji ya drop ina bei kuanzia elfu ni mwani peke yake uliosema kuanzia shilingi mia. Ni lini bei ya mwani itatangazwa kama bei ya kitu chochote kinachofanana na kilo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na kama nilivyoeleza awali kwamba hili suala sio la taasis moja. Kwa hivyo mimi kama taasisi siwezi nikaamua bei peke yangu ni lini lakini ni lazima nikae na taasisi nyengine, yaani taasisi ya Wizara ya Biashara pamoja na wafanyabiashara wenyewe ndio hapo tutajua ni lini hasa tutapata hii bei mpya.

Kwa hivyo ni lazima tukae na taasisi nyengine ili tutoe maamuzi, peke yangu siwezi kukwambia ni lini. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu lakini ni lini utakaa na taasisi hizi kujua bei.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni baada ya bajeti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia pamoja na Waziri kuwa amenijibu lakini nilitaka kufahamu kwa sababu nilimueleza kama serikali imetoa kipa umbele kwa wafugaji wa samaki, na nia na madhumuni ni kuwapunguzia wananchi umaskini ili wanapofuga waweze kuzalisha na kujikwamua katika maisha yao.

Lakini nilimwambia Mhe. Waziri ufugaji wa samaki mpaka hivi sasa ni ufugaji wa samaki wa kitoweo tu haujawa wa uzalishaji tukaona kama kweli kuna uzalishaji. Kwa hivyo sasa ninataka Mhe. Waziri aniambie wizara yake kupitia serikali itachukua juhudi gani kukuza biashara hiyo ya ufugaji wa samaki kuona kama ni biashara sio ya kitoweo. Ni lini watasimamia kuona kama sasa hivi itakuwa ni biashara endelevu na sio ya kitoweo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, katika majumuisho yangu nilieleza hilo kwamba ni kweli kuwa mpaka hivi sasa ufugaji wa samaki haujawa wa kibiashara hasa, kwa sababu huu ndio mwanzo tu na ndio maana tumeweka mashamba ya madarasa na tumeona mfano mzuri kule Pujini kwa kweli yeye mwenyewe binafsi ameshaanza tayari kupakia samaki kwenye pick up anakwenda kuuza Chake Chake.

Nilimshuhudia mimi mwenyewe, kwa hivyo sasa inaonekana ni trend kwa sababu yeye tayari ana mashamba makubwa na ndio maana tukalitenga lile shamba lake kuwa ni shamba darasa, kwa sababu yeye tayari anaanza kufanya mauzo makubwa.

Na vile vile tuna huu mradi wa Korea ambao utahamasisha na kufufua mashamba mengine ili kuona kwamba huu ufugaji wa samaki unakua siku hadi siku. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi hiyo project ipo ya Kora ambayo tayari tumeshatenga maeneo Pemba mengine ili kuona kwamba ufugaji wa samaki unakwenda kibiashara zaidi. Huu ni mwanzo tu lakini ninaamini kwamba baada ya muda mfupi basi mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kajibu vizuri lakini naomba kama hili suala tukianzisha kitu basi tukipe uzito, tusianze ikawa ni kuanzisha halafu tukawa tunarudi nyuma. Kila siku sisi huwa tunaanzisha mambo halafu huwa tunarudi nyuma, baada ya kwenda mbele tunarudi nyuma, maana mambo yetu ni kujaribu tu.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri kama alivyokwisha kuzungumza basi hili suala kuwa linapewa uzito na liwe endelevu. Kama halina maana tuone kuwa halina maana tuliachie, kama lina maana basi tulikuze, tusiwe tu kama tunazungumza tu uvuvi wa bahari kuu lakini hatufiki mwisho, maisha tunataja tu hapa kwenye vitabu. Tuendelee.

Kifungu 0701 Idara ya Mazao ya Baharini Unguja	shs.811, 200,000/=
Kifungu 0801 Idara ya Uzalishaji Wanyama Unguja	shs.122, 000,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.1, 763,160,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya

mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio haya. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika**,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika**,** awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani na utulivu. Ni dhahiri kwamba hali hii ya amani na utulivu imezidi kuimarika tangu kuasisiwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Umahiri na uadilifu katika uongozi wake umekubalika hapa Zanzibar na tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, maarifa na hekima zaidi ili aendelee kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika**,** nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutekeleza vyema ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015; kwa kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya adui maradhi, njaa na umasikini kwa mafanikio makubwa. Mafanikio hayo yamewezesha kukua kwa uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuvutia wawekezaji, na imepelekea Serikali za nchi zilizoendelea na wahisani kuwa na imani na Serikali na hivyo kuwafanya waendelee kutoa misaada katika sekta za kiuchumi na kijamii.

Mhe. Naibu Spika**,** aidha, nazipongeza juhudi za Mhe. Rais za kufuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi za Serikali kupitia maagizo, maelekezo, ziara zake za Mikoa yote ya Zanzibar na majadiliano ya ana kwa ana na watendaji wa Serikali. Hatua hizo zimeweza kuimarisha ufanisi katika utendaji, uwajibikaji, usimamizi na ufuatiliaji wake wa karibu wa majukumu ya Wizara na taasisi za Serikali.

Mhe. Naibu Spika**,** napenda pia kumpongeza Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad, Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa juhudi zao za kufuatilia maendeleo ya sekta ya kilimo pamoja na kutupatia ushauri wa mara kwa mara juu utekelezaji wa majukumu ya sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Salmini Awadhi Salmini, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013. Naishukuru sana Kamati hiyo kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2012/2013 katika kikao chake kilichofanyika Ofisi za Baraza la Wawakilishi tarehe 28 Mei, 2012. Napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika**,** naomba pia nikupongeze wewe binafsi kwa umahiri wako katika kuliongoza Baraza hili Tukufu ambalo linatoa maamuzi mazito katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini.

Mhe. Naibu Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Jang'ombe kwa kuendelea kunipa mashirikiano na kuwa na imani na mimi katika kusimamia na kuleta maendeleo ya jimbo hili. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha ili kuharakisha kuleta maendeleo jimboni. Aidha, napenda kuishukuru familia yangu kwa kunipa ushirikiano na kuwa wavumilivu katika kipindi chote ninapokuwa katika majukumu ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa masikitiko makubwa napenda kutoa pole kwa wanafamilia, ndugu, na jamaa wa Wawakilishi wenzetu waliofariki dunia katika kipindi hiki cha utekelezji wa majukumu yetu, marehemu Khamis Mussa Silima ambaye hadi anafariki alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini Unguja na marehemu Salum Amour Mtondoo aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi - AMIN. Pia, tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie ndugu wa marehemu moyo wa subira na uvumilivu hasa katika wakati huu mgumu.

MCHANGO NA UKUAJI WA SEKTA YA KILIMO

Mhe. Naibu Spika**,** Sekta ya Kilimo inaendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wetu kwa kutoa ajira zaidi ya asilimia 45 ya wakaazi wa Zanzibar. Kiuchumi, sekta hii imeweza kuchangia wastani wa asilimia 32.2 katika pato la taifa na asilimia 75 ya mapato ya fedha za kigeni (OCGS, 2011). Ni dhahiri kwamba Sekta ya kilimo ina mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha, kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora na hivyo ina mchango mkubwa katika ustawi wa maisha yetu.

Mhe. Naibu Spika**,** mwaka 2011, Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia 5.7 ikilinganishwa na asilimia 4.6 ya mwaka 2010. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika Sekta ndogo ya mazao ya chakula na kuwepo kwa hali ya hewa nzuri katika msimu wa Vuli 2011 kulikoshajiisha wakulima kuongeza juhudi za uzalishaji hasa katika kilimo cha muhogo na migomba. Aidha, ongezeko la uzalishaji

lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa miundombinu ya umwagiliaji maji pamoja na utekelezaji wa Miradi na Programu za Kuendeleza na kutoa huduma katika Sekta ya Kilimo, Mifugo na Maliasili.

Mhe. Naibu Spika**,** Wizara ya Kilimo na Maliasili imeendelea kutekeleza dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo kwa kuendeleza zao la Mpunga na mazao mengine ya chakula ili kuongeza uzalishaji wa chakula na kudhibiti mfumuko wa bei nchini. Aidha Wizara inaendelea na mpango wake wa Ufufuaji wa zao la karafuu kwa lengo la kuimarisha mchango wa kilimo katika mapato ya wananchi, kupunguza umasikini na hatimae kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kukuza uchumi wa nchi yetu. Mipango yote hii inajumuisha utoaji wa ruzuku katika pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea, mbegu, miche na dawa za magugu pamoja na huduma za matrekta ambapo Serikali ilichangia zaidi ya asilimia 75 ya gharama ili wakulima wapate fursa ya kuzipata na kuzitumia pembejeo na huduma hizi kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mpunga na kushajiisha upandaji upya wa mikarafuu.

HALI YA UZALISHAJI

Mhe. Naibu Spika**,** msimu wa kilimo wa mwaka 2011/12 uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka ukilinganisha na mwaka 2010/2011. Zao la muhogo liliongezeka kutoka tani 229,284 mwaka 2010 hadi tani 273,342 mwaka 2011, ndizi kutoka tani 102,258 mwaka 2010 hadi tani 110,250 mwaka 2011, mpunga kutoka tani 21,014 mwaka 2010 hadi tani 23,702 mwaka 2011, viazi vitamu kutoka tani 58,953 mwaka 2010 hadi tani 92,715 mwaka 2011 na zao la mahindi kutoka tani 3,112 mwaka 2010 hadi tani 3,281 mwaka 2011.

Mhe. Naibu Spika**,** hata hivyo, mazao ya majimbi na viazi vikuu uzalishaji umeshuka kutoka tani 6,443 mwaka 2010 hadi tani 4,940 mwaka 2011 na viazi vikuu kutoka tani 7,487 mwaka 2010 hadi tani 4,212 mwaka 2011. Kushuka kwa uzalishaji wa viazi vikuu kumesababishwa na kupungua kwa eneo (ekari) ambapo mwaka 2010 ekari 1,497.4 zililimwa ukilinganisha na ekari 842.4 mwaka 2011.

Mhe. Naibu Spika, taarifa za hali ya hewa katika kipindi cha masika 2012 si za kutia moyo hasa kwa kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua. Takwimu zinaonyesha kuwa kumekuwa na upungufu mkubwa wa mvua za masika mwaka huu ambazo zimenyesha kwa kiwango kidogo sana chini ya wastani wa kila mwaka. Katika kipindi cha mwezi Machi tumepata mvua milimita 150.5 sawa asilimia 84 ya wastani, katika mwezi wa April tumepata mvua milimita 178.4 sawa na asilimia 43 tu ya wastani, na katika mwezi wa Mei tumepata mvua milimita 115.5 sawa na asilimia 42 tu ya wastani wa mvua kwa mwezi huo. Kwa ujumla katika kipindi cha miezi mitatu ya masika tumepata mvua milimita 444.4 sawa na asilimia 51 ya wastani wa mvua ya milimita 870 ambayo hupatikana kila mwaka katika msimu huu wa masika.

Mhe. Naibu Spika, hali hii imeathiri sana ukulima wa mpunga wa kutegemea mvua ambapo sehemu kubwa ya kilimo hicho kimedumaa hasa katika maeneo ambayo wakulima wamechelewa kupanda mpunga kutokana na kuchelewa kupata huduma za

matrekta. Wizara yangu tayari imeshafanya tathmini ya athari iliyopatikana katika maeneo yote ya kilimo cha mpunga Unguja na Pemba kwa lengo la kuishauri Serikali juu ya hatua za kuchukuliwa kuwasaidia wakulima walioathirika na janga hili la ukame na upungufu wa mazao yao. Napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wakulima wote wa mpunga ambao wameathirika kutokana na upungufu huu wa mvua za msimu.

Mhe. Naibu Spika**,** napenda kuwahakikishia wakulima wote kupitia Baraza lako kuwa Serikali ipo pamoja nao na kwamba itafanya kila linalowezekana kusaidiana nao kukabiliana na hali hii ya upungufu wa mavuno. Aidha Wizara yangu imefanya maandalizi ya kutosha katika msimu ujao wa kilimo kuwapatia wakulima pembejeo na huduma za matrekta mapema ili kuwahi matayarisho na kuzitumia vizuri mvua za msimu ambazo zimeonekana haziaminiki.

MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI 2012/2013

Mhe. Naibu Spika**,** muelekeo wa Wizara ya Kilimo na Maliasili katika bajeti ya mwaka 2012/13 ni kuendelea kutekeleza mikakati ya Mapinduzi ya Kilimo iliyoanza utekelezaji wake katika mwaka 2011/12. Kwa upande wa mazao ya chakula, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa kuliendeleza zao la Mpunga kwa kuimarisha utoaji wa ruzuku katika pembejeo na huduma za Kilimo, kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliagi maji, kuimarisha matumizi ya zana bora za kilimo yakiwemo matrekta na zana za kupandia, kuvunia na kusagishia mpunga, kuimarisha utoaji wa mafunzo na taaluma ya ukulima bora wa mpunga wa umwagiliaji na mpunga wa juu pamoja na kushajiisha upandaji wa mbegu ya *NERIKA* kwa maeneo ya kilimo cha juu kwa kuongeza idadi ya mashamba ya mafunzo na maonyesho ya uzalishaji wa *NERIKA* katika kila Shehia na kuongeza uzalishaji wa mbegu hii ambayo imeonekana inastawi vizuri katika maeneo mengi ya juu hata katika hali ya upungufu wa mvua.

Mhe. Naibu Spika**,** Wizara pia itaendelea na utafiti na kushajiisha uzalishaji wa mbegu bora kwa mazao ya mizizi hasa muhogo, viazi vitamu na viazi vikuu sambamba na kuongeza mafunzo na utoaji wa elimu kwa wakulima wa mazao haya. Aidha Wizara itaendelea na utafiti wa mbegu bora za migomba na kuendeleza mafunzo ya ukulima bora wa mboga mboga zinazostawi hapa nchini pamoja na mbinu mchanganyiko za kudhibiti maradhi na wadudu waharibifu ili kudumisha ubora na kuongeza uzalishaji wa chakula na hatimae kuchangia katika punguzo la mfumuko wa bei.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili pia inaendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuanzisha maghala ya akiba ya chakula ya Zanzibar kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kusababishwa na majanga ya kimaumbile. Katika mwaka wa fedha 2012/13, Wizara itaifanyia kazi ripoti ya uchambuzi yakinifu iliyowasilishwa Serikalini na Mshauri mwelekezi aliyeajiriwa na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (*FAO*) juu ya namna bora ya kuanzisha, kusimamia na kuendesha maghala ya akiba hapa Zanzibar;

Mhe.Naibu Spika**,** kwa upande wa mazao ya biashara, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na utekelezaji wa Mpango Maalum wa kuimarisha uzalishaji wa zao la karafuu kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Mikarafuu ambao pamoja na mambo mengine umeweka wazi malengo yafuatayo:

- Kuimarisha utoaji wa Elimu kwa wakulima ambapo Wizara imelenga kutoa mafunzo ya uoteshaji wa miche katika vitalu, upandaji na uhudumiaji wa mikarafuu, uvunaji na uanikaji kwa lengo la kuongeza wingi na ubora.

- Kuimarisha ukaguzi kwa karafuu zinazosafirishwa nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha kuwa zina viwango vinavyokubalika kimataifa.

- Kuongeza uzalishaji wa miche ya mikarafuu kufikia miche 1,000,000 mwaka 2012/2013 na kuigawa kwa wakulima bila malipo ili kurejeshea mikarafuu mingi ambayo imezeeka na kufa. Pia upandaji utaendelea kuimarishwa kwa kuhakikisha wakulima wote wameorodheshwa katika daftari maalum lililotayarishwa na kukaguliwa maeneo yao kabla ya kugaiwa miche hiyo.

- Kufanya sensa ya mikarafuu kwa lengo la kupata taarifa muhimu ikiwemo kujua idadi ya mikarafuu, umri pamoja na maeneo yaliyooteshwa. Taarifa hizo zitasaidia Wizara kutoa muongozo juu ya njia bora ambazo zitatumika katika kuendeleza na kuimarisha zao la karafuu hapa Zanzibar.

- Kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Masoko kuandaa utaratibu maalum utakaotekelezwa kila mwaka wa kuwazawadia wakulima bora wa zao la karafuu kwa lengo la kuhamasisha na kuthamini juhudi na michango yao katika kulifufua na kuliendeleza zao hili.

- Kuimarisha utafiti wa zao la karafuu kwa lengo la kuliendeleza na kuongeza tija na ubora wake. Maeneo maalum yatakayopewa kipaumbele katika utafiti ni pamoja na utafiti wa maradhi ya mikarafuu, mbegu bora zenye uzazi mzuri na zinazostahamili maradhi. Njia bora za uvunaji zisizoathiri mikarafuu pamoja na kilimo mseto cha karafuu na mazao mengine ya viungo ikiwemo Hiliki, Vanila na Manjano.

- Kuyasimamia na kuyaendeleza mashamba ya Serikali ya mikarafuu yaliyokuwa chini ya Wizara ya Ardhi ambayo kwa muda mrefu yaliachwa bila kuendelezwa. Hatua za awali za kuyajua na kuyaorodhesha zimekamilika.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea na usimamizi wa Maliasili kwa kushajiisha uhifadhi wa misitu ya asili na matumizi endelevu ya maliasili zisizorejesheka. Aidha Wizara itaimarisha ulinzi katika maeneo ya misitu yenye vyanzo vikuu vya maji pamoja na kutekeleza mpango mahsusi wa upandaji miti na uhifadhi wa maeneo hayo. Wizara pia itaendeleza kampeni za upandaji miti kitaifa

katika maeneo yenye vyanzo vya maji, fukwe za bahari na maeneo mengine yaliyoathirika kwa kuwashirikisha kikamilifu wananchi na taasisi zao katika kampeni ya upandaji miti kitaifa ambayo itaendelea kufanyika kila mwezi kadiri hali ya hewa na mazingira ya bahari yatavyoruhusu.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI MWAKA 2011/2012

MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Naibu Spika; Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 238, 500,000. Kufikia Juni, 2012 Wizara imekusanya Tsh. 539,751,956 sawa na asilimia 226 ya makadirio ya lengo kama .inavyoonekana kwenye kiambatisho nambari 11.

MATUMIZI YA FEDHA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika**;** kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 8, 304, 475,836 kwa kazi za kawaida na Tsh. 500, 000,000 ikiwa ni Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani. Hadi kufikia Juni, 2012 kwa kazi za kawaida Wizara imepata Tsh. 7,961,604,481 sawa na asilimia 96 na Chuo cha Kilimo kimepata Tsh. 495,000,000 sawa na asilimia 99.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 3, 600, 000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Juni, 2012 fedha zilizopatikana ni Tsh. 3,313,552,544. Sawa na asilimia 92 kwa mchango wa SMZ. Kwa upande wa wahisani fedha zilizotengwa kwa mwaka 2011/2012 ni Tsh. 4,539,849,000 hadi kufikia Juni, 2012 Wizara imepata jumla ya Tsh. 4,056,059,874 sawa na asilimia 89 ya lengo**.** Kiambatisho nambari 12 kinaeleza mchanganuwo wa fedha hizo Kiidara.

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika**;** Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ya Kilimo na Maliasili inakadiriwa kukusanya Tsh. 426,000,000 (Mapato). Na inakadiriwa kutumia Tsh. 23,827,116,000 kati ya hizo Tsh. 11,820,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na Tsh. 500,000,000 ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani na Tsh. 11,507,116,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi 11 ya maendeleo ambapo Tsh. 2,090,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali na kwa upande wa wahisani wa maendeleo ni Tsh. 9,417,116,000. Makadirio hayo Kiidara yameoneshwa kwenye kiambatisho nambari 17.

Mhe. Naibu Spika**;** Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na mambo mengine imefanikiwa kutekeleza kwa kiasi kikubwa malengo iliyojipangia kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:

- Wizara imesambaza pembejeo kwa wakulima wa mpunga ikiwemo mbegu, kutoka tani 124 (2010/2011) hadi tani 322 (2011/2012); ambapo asilimia 41 ya wakulima wa mpunga wamefaidika ukilinganisha na asilimia 16 ya

msimu uliopita. Aidha, matumizi ya mbolea yaliongezeka kutoka tani 242 hadi tani 524 na dawa ya magugu kutoka lita 18,000 hadi lita 20,000;

- Kuongezeka kwa eneo lililolimwa mpunga wa kutegemea mvua kutoka ekari 29,000 hadi kufikia ekari 31,900;
- Kuongezeka eneo la umwagiliaji maji kwa kujenga miundombinu kutoka hekta 700 hadi kufikia hekta 750;

- Kuongezeka uzalishaji wa miche ya mikarafuu kutoka 240,000 mwaka 2010/2011 hadi kufikia miche 591,000 mwaka 2011/2012;

- Kuongezeka uzalishaji wa miche ya misitu katika vitalu vya Serikali na vya watu binafsi kutoka miche 1,000,000 hadi miche 2,5000,000;

- Kukamilika kwa kanuni ya kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto na kuanza kufanya kazi. Aidha, jumla ya misumeno ya moto 31 imekamatwa na utaratibu wa Sheria unaendelezwa;
- Kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka makisio ya Tsh. 238,500,000 hadi kufikia Tsh. 539,751,956;

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA (2011/2012) NA MALENGO (2012/2013)

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji katika Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2011/2012 ulilenga katika kuongeza uzalishaji wa mazao yenye ubora na tija, kuongeza ufanisi katika udhibiti wa matumizi ya maliasili na kupunguza uharibifu wa mazingira. Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo kupitia taasisi zake kwa mwaka 2011/2012 pamoja na malengo ya mwaka 2012/2013 ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ndio kiungo kikuu cha Wizara ikiwa na majukumu ya kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati na Mipango ya Maendeleo pamoja na kazi za Utafiti. Aidha, Idara inaratibu mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya Wizara, taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jumuiya za Kikanda, Sekta Binafsi, Jumuiya na Asasi zisisizo za kiserikali pamoja na Washirika wa Maendeleo.

MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara ilipanga malengo yafuatayo:

- Kuendelea kutayarisha na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango na Miradi ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Maliasili;

- Kufanya mapitio ya Sera ya Kilimo, Sera ya Misitu, Sera ya Mbegu na Haki miliki za wavumbuzi wa mbegu;

- Kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na maliasili;

- Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Utafiti na Dira ya Elimu kwa Wakulima (Research Master Plan and Extension Vision);
- Kuendelea kusimamia programu na miradi mipya na inayoendelea;

- Kuendeleza mashirikiano na taasisi za utafiti ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) katika kufanya tafiti na utoaji wa matokeo;

- Kuendelea kuratibu mashirikiano kati ya Wizara na taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi;

- Kuandaa warsha na kutoa toleo la tatu la utafiti (3rd Annual Agricultural Research Proceeding);

- Kutayarisha na kutoa jumla ya nakala 2,000 za Jarida la Mkulima na kusambaza kwa wadau wa sekta ya kilimo;

- Kukusanya mapato yanayokadiriwa kufikia TSh. 238,500,000 kutoka vyanzo vilivyo chini ya Wizara;

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Jumla ya Tsh. 539,751,956 zilikusanywa kutoka vyanzo vya mapato ambazo ni sawa na asilimia 226 ya lengo lililowekwa;

- Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo imekamilika na Sheria ya Uanzishwaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Zanzibar (ZARI) zimekamilika na zimeshawasilishwa Serikalini. Aidha, mapitio ya awali ya Sera ya Kilimo na Sera ya Misitu yamefanyika;

- Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na maliasili umefanyika;

- Wizara kwa kushirikiana na *COSTECH* imefanikisha uchapishaji wa toleo la pili la tafiti (2nd Annual Research Review Proceeding, 2011);

- Mpango Mkuu wa Utafiti na Dira ya Elimu kwa Wakulima (*Research Master Plan and Extension Vision*) umetekelezwa kwa kuanzishwa Taasisi ya Utafiti pamoja na Sheria yake. Aidha, Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa kazi za utafiti (*Strategic Plan*) kwa miaka mitano 2012 - 2017 umeanza kutayarishwa;

- Nakala 1,500 za Jarida la Mkulima zimetolewa na kusambazwa kwa wadau wa sekta hiyo;

- Kamati ya utafiti inayoshirikisha wataalamu kutoka taasisi za *SUZA*, IMS, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo na Maliasili imeanzishwa na kuanza kazi ya uainishaji wa maeneo ya kipaumbele ya utafiti;

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara iliendelea kusimamia utekelezaji wa programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo kama ifuatavyo:

- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo–*ASSP*, (Kiambatisho 1);
- Programu ya Kutoa Huduma za Mifugo *ASPD-L* (Kiambatisho 2);
- Programu ya Usarifu wa Mazao (Kiambatisho 3);
- Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Kilimo na kuongeza Thamani ya Mazao (*MIVARF*) (Kiambatisho. 4);

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuimarisha mifumo ya Kisera, Sheria, Mikakati na Mipango/Miradi ya Wizara ili kukabiliana na changamoto zilizopo kwa kufanya mapitio ya Sera za Kilimo, Karantini na Mbegu; Mswada wa Sheria ya Haki Miliki ya Wagunduzi wa Mbegu; Sheria na Kanuni za Misitu; Mkakati wa Mageuzi ya Kilimo (*ATI*); na Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Masoko (*ZAMP* IP);

- Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya kisekta na Wizara *(M* & *E*); ikiwemo mawasiliano na utoaji taarifa kwa njia ya tovuti (www.kilimoznz.or.tz); kutoa nakala 2,000 za Jarida la Mkulima;

- Kuimarisha mashirikiano kati ya Wizara na taasisi za ndani, za kikanda na nje ya nchi; ikiwemo kukamilisha na kuratibu mfumo wa pamoja wa kitaasisi katika Sekta ya Kilimo (*ASP-Z*); kushiriki katika Vikundi Kazi vya kitaifa, mikutano na makongamano ya kitaifa; kikanda na kimataifa;

- Kuimarisha tafiti za kijamii, kiuchumi na kisayansi ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo kwa kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya maeneo ya kipaumbele ya utafiti; na Kuandaa warsha na kutoa Toleo la Tatu la Utafiti wa Kilimo (*3rd Annual Agricultural Research Proceeding*);
- Kuendelea kusimamia programu na miradi mipya na inayoendelea.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliombewa Tsh. 3,762,586,769 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 3,619,614,081 sawa na asilimia 96 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara inaombewa kutumia jumla ya Tsh.1,844,094,000 kutoka Serikalini na Tsh. 7,160,570,000 kutoka kwa Wahisani.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii inajukumu la kutoa huduma za uongozi wa rasilimali watu na utawala katika Wizara, ikiwa ni pamioja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Pia inajukumu la kuratibu masuala mtambuka kama Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Kwa mwaka 2011/2012 Idara ilipanga malengo yafuatayo:

- Kutayarisha mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi (*Training Master Plan*) itayoonesha maeneo ya vipaumbele katika fani za Wizara;
- Kuimarisha utendaji katika uhifadhi wa kumbukumbu zikiwemo taarifa za wafanyakazi na rasilimali za Wizara (*DataBase*);
- Kutayarisha mpango mkakati (*Strategic Plan*) wa miaka mitatu wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa kazi;
- Kuhakikisha rasilimali za Serikali zilizomo ndani ya Wizara zinatunzwa na kupatiwa hatimiliki;

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi na Mfumo wa uwekaji na uhifadhi wa kumbukumbu za wafanyakazi na rasilimali za Wizara imekamilika;
- Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi wenye lengo la kuimarisha ufanisi wa kazi umekamilika;
- Jumla ya wafanyakazi 198 wamepatiwa mafunzo kama ifuatavyo; 72 (wanawake 25 na wanaume 47) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini, wafanyakazi 40 (wanawake 17 na wanaume 23) mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na 86 (wanawake 45 na wanaume 41) mafunzo ya muda mrefu;

- Wafanyakazi 152 wameajiriwa (110 Mabwana/Mabibishamba waliomaliza mafunzo Chuo cha Kilimo Kizimbani na wafanyakazi 42 (wanawake 4 na wanaume 38) wameajiriwa katika kada nyengine tofauti);

- Wafanyakazi 15 (wanawake 8 na wanaume 7) wamefariki dunia. Aidha, wafanyakazi 101 wamestaafu kwa hiari na kwa mujibu wa sheria na wafanyakazi 34 wamekwenda likizo bila ya malipo na 12 wamepewa uhamisho wa nje ya Wizara;

- Upimaji wa mashamba na vituo vya utafiti katika maeneo ya Kidichi, Kizimbani, Selem, Bambi na Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa Unguja umekamilika pamoja na michoro yake. Kwa upande wa Pemba upimaji na uchoraji umekamilika kwa Shamba la utafiti la Matangatuani, maeneo ya Ofisi za Kilimo (Weni), Ofisi ya Idara ya Kilimo Mkoa wa Kusini (Wawi Chake chake) na Ofisi ya Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka (Kizimbani);

- Upimaji na uchoraji pia umefanyika katika nyumba za Wizara ziliopo Mbweni, Mazizini, Saateni na Maruhubi (Ofisi za *ASSP*/*ASDP*-L) kwa Unguja. Kwa Pemba, nyumba ya Afisa Mdhamini (Wete) pamoja na eneo la Kiwanja cha nyumba ya Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka (Bopwe);

- Uhakiki wa rasilimali za Serikali zilizomo ndani ya Wizara umefanyika.

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa 2012/2013 Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kukusanya mapato yanayokadiriwa kufikia TSh. 426,000,000;
- Kuendelea kuhakiki mali za serikali zilizo chini ya Wizara na kupata hati miliki;
- Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi;
- Kusimamia maslahi na kuwawekea mazingira mazuri wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliombewa Tsh. 170,700,000 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Idara imepatiwa jumla ya Tsh 147,887,080 sawa na asilimia 87 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Iidara inaombewa kutumia jumla ya Tsh. 938,760,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA KILIMO

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa Wakulima, Uhifadhi na Ukaguzi wa Mazao na kutoa mafunzo kwa wazalishaji.

MALENGO YA IDARA YA KILIMO MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/12, idara iliwekewa malengo yafuatayo:

- Kuwaelimisha wakulima 1,500 juu ya mbinu za kilimo bora;
- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabibishamba/mabwanashamba 120 juu ya mbinu bora za kilimo na Utafiti wa mazao ya chakula, biashara, usarifu wa mazao;
- Kuandaa ziara 12 za wakulima na mabibi/mabwanashamba ili kuweza kubadilishana utaalamu ikiwemo kuwapeleka katika maonyesho ya nane nane Tanzania Bara;
- Kutayarisha Makala 15 na vipeperushi 600 na kupatiwa wakulima;
- Kutayarisha vipindi 60 vya redio na 37 vya TV na kuvirusha hewani;
- Kununua gari tano kwa lengo la kufanikisha utoaji wa huduma za elimu kwa wakulima;
- Kuendeleza kazi za karantini na ukaguzi wa mazao;
- Kuzalisha na kusambaza tani 12 za mbegu za mahindi na mtama tani 5 na jamii ya kunde tani 8;
- Kununua na kusambaza mbolea tani 590 (245 TSP na 345 Urea);
- Kutoa huduma za kilimo cha matrekta kwa kushirikiana na wenye matrekta binafsi pamoja na kutengeneza matrekta mabovu 29 na zana zake;

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2011/12

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara imetekeleza kazi zifuatazo:

- Jumla ya wakulima 1,500 walipatiwa mafunzo ya kilimo bora cha mazao ya chakula ukiwemo mpunga Unguja na Pemba;
- Mabibi/Mabwana shamba 137 kutoka Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo juu ya mbinu za kisasa za kilimo. Aidha, ziara za ndani za wakulima kutembeleana na kubadilisha utaalamu zilifanyika na wakulima 60 walishiriki;
- Makala 6 zilitolewa juu ya mbinu za kilimo bora kwa mazao ya chakula. Aidha, vipindi 14 vya Redio na 6 vya TV vilitolewa juu ya njia sahihi ya ulezi wa ndama, malisho ya mifugo, ufugaji bora wa kuku na nyuki;
- Vipeperushi 1,000 juu ya maradhi ya migomba vilitayarishwa na kutolewa kwa wakulima;

- Mitego mikongwe 20,000 ya kunasia nzi waharibifu wa matunda imebadilishwa dawa na mitego mipya 65,000 imesambazwa kwa wakulima wa Wilaya 9 (mitego 12,103 Pemba na mitego 35,580 kwa Unguja). Aidha, mitego 47,683 ilisambazwa maeneo ya mjini ikiwemo kwenye masoko, vituo, madukani na kwa watu binafsi walioomba.

- Tathmini ya uangamizaji wa nzi hao inaonesha uharibifu wa embe umeshuka kutoka asilimia 75 mwaka 2007 hadi 30 mwaka 2011/12;

- Kazi za ukaguzi wa mazao na Karantini ziliendelea na mikungu 170 ya ndizi iliyoingizwa nchini kinyume cha sheria na yenye maradhi ilikamatwa na kuharibiwa. Kwa upande wa ugaguzi wa bidhaa za hapa nchini, jumla ya tani 4,490 za karafuu zilikaguliwa kabla ya kusafirishwa;

- Ekari 31,933 za kilimo cha mpunga sawa na asilimia 96.76 ya lengo zimelimwa Unguja na Pemba;

- Tani 160 za mbegu ya mpunga kutoka T/Bara zimenunuliwa na tani 162 zimezalishwa kupitia mikataba na wakulima sawa na asilimia 90.7. Aidha, tani 8.7 za mahindi na tani 2.6 za mtama, zimezalishwa na kuuzwa kwa wakulima na kuuzwa kwa wakulima kwa bei ya Tsh. 200 kwa kilo;

- Tani 245 za *UREA* na 245 za TSP zimenunuliwa na kuuzwa kwa wakulima Pemba na Unguja kwa bei ya Tsh. 200 kwa kilo;

- Matengenezo ya Matrekta 27 (Pemba 8 na Unguja 19) yamefanyika. Aidha matrekta 10 mapya (*NEWHOLLAND 75HP 4WD*) yamenunuliwa kwa njia ya mkopo ambapo Pemba yamepelekwa 4 na Unguja 6. Vilevile matrekta ya *PADEP* 2 Pemba na 6 Unguja yalijumuika na matrekta ya Serikali katika kuendeleza kazi za ukulima wa mpunga kwa msimu huu 2011/1012;

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuhakikisha upatikanaji wa mbegu ya mpunga tani 570, mbolea tani (*UREA* 1,000 na TSP 500), dawa ya kuulia magugu lita 30,000 ili kuongeza uzalishaji;

- Kutoa huduma za kilimo na kusimamia ukulima wa mpunga ekari 40,000;
- Kuwaelimisha wakulima 1,500 juu ya mbinu za kilimo bora;

- Kudhibiti maradhi ya mimea na wadudu waharibifu wa mazao;

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Mabibi/Mabwana Shamba 95 juu ya mbinu bora za kilimo;

- Kuzalisha tani nane za mbegu ya mahindi, tani mbili za mbegu ya mtama na tani 570 za mbegu ya mpunga ikiwemo *NERICA*;

- Kuzalisha mbegu ya mpunga wa kwa mikataba ya wakulima na mashamba ya JKU;

- Kutayarisha lita 500 za dawa ya asili kwa ajili ya kuulia wadudu waharibifu wa mimea na kupunguza matumizi ya dawa za viwandani;

- Kuyafanyia matengenezo matrekta 46 na power tiller 75 kwa ukulima wa mpunga wa 2012/2013;

- Kutoa mafunzo kwa mafundi na madereva 100 wa matrekta na Power Tillers;

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliombewa Tsh. 3,410,361,974 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Idara imepatiwa jumla ya Tsh 3,313,671,438 sawa na asilimia 97 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Iidara inaombewa kutumia jumla ya Tsh. 5,153,430,000 kutoka Serikalini.

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu la kupanga na kutekeleza kazi za utafiti wa Kilimo na Maliasili na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi na wadau wengine. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inajumuisha vituo vyote vya utafiti vilivyo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

MALENGO YA TAASISI YA UTAFITI KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ililenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo;

- Kuzalisha mbegu mama za muhogo katika eneo la hekta 25 katika vituo vya utafiti;
- Kuchapisha makala za utafiti;

- Kufanya utafiti wa mbegu bora za mpunga, mazao ya mizizi na mbogamboga;

- Kukarabati majengo, barabara na miundombinu mengine ya vituo vya Kizimbani Unguja na Matangatuani Pemba.

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mwaka wa fedha wa 2011/2012 Taasisi imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Matayarisho ya awali juu ya Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo yameanza;

- Uzalishaji wa mbegu mama za muhogo hekta 18 umefanyika katika vituo vya utafiti. Aidha, uzalishaji wa mbegu mpya za muhogo kwa biashara kwa wakulima 120 umefanyika na tafiti za mbegu zinazostahamili maradhi zinaendelea;

- Makala mbili za utafiti wa mpunga, viazi vitamu na muhogo zimechapishwa;

- Majaribio ya mbegu za mboga mboga kutoka China na *AVDRC* yameanzishwa;

- Uchunguzi wa udongo katika mabonde ya mpunga yanayoingia maji chumvi likiwemo Mziwanda Pemba umefanyika;

- Jaribio la mbegu 3 za mpunga zenye kustahamili maradhi ya Ugonjwa wa Manjano ya Majani ya Mpunga kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*IAEA*) linaendelea;

- Uchunguzi wa aina 15 za mbegu za mpunga kwa ajili ya kuibua mbegu chache zitakazotumiwa na wakulima katika maeneo yao umefanyika;

- Uchunguzi wa aina mpya za mbegu za mpunga 33 zinazostahamili maradhi, wadudu na zenye uzazi mkubwa kutoka Kyela, Mbeya unaendelea. Aidha, tafiti za mbegu mpya aina 70 za mpunga kutoka China;

- Utafiti wa aina 28 wa mbegu za mpunga zinazostahamili maradhi, wadudu na zenye uzazi mkubwa kwa pamoja baina ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Shirika la Kimataifa la Utafiti wa Mpunga unaendelea;

- Ukusanyaji na uhifadhi wa aina 50 za mbegu za mpunga za kienyeji unaendelea;

- Mkandarasi kwaajili ya ujenzi wa maabara ya mpunga na ukarabati wa maabara nyengine tatu amepatikana.

- **MALENGO YA TAASISI KWA MWAKA 2012/2013**
  Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuendeleza utafiti wa mbegu bora za mpunga, mazao ya mizizi, mbogamboga na matunda ili kupata mbegu mpya zitakazotoa mazao mengi zaidi;

- Kufanya utafiti wa kilimo bora cha mikarafuu;

- Kuimarisha mazingira na uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma za utafiti;

- Kufanya utafiti wa kuendeleza misitu na matumizi bora ya maliasili zisizorejesheka;

- Kuendelea na utayarishaji Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Taasisi ya Utafiti.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Taasisi iliombewa Tsh. 597,306,000 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Taasisi imepatiwa jumla ya Tsh 529,259,702 sawa na asilimia 89 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Taasisi inaombewa kutumia jumla ya Tsh. 1,306,200,000 kutoka Serikalini.

CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo na mifugo kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari na kufaulu masomo katika fani ya sayansi.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Chuo kimelenga kutekeleza malengo kama ifuatavyo:

- Kutoa mafunzo ya cheti kwa wanafunzi 140 wa mwaka wa kwanza;
- Ujenzi wa bweni la wanafunzi ambao unafadhiliwa chini ya Programu za ASSP/ASDP-L uko katika hatua za awali;
- Kutoa mafunzo kwa wakulima 500 katika mabonde matatu ya mpunga wa umwagiliaji;
- Kukamilisha usajili wa Chuo kwa Baraza la Vyuo vya Ufundi Tanzania (NACTE).

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Chuo kimetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Mafunzo yametolewa kwa wanafunzi 150 (69 mwaka wa pili na 81 mwaka wa kwanza);

- Ujenzi wa bweni la wanafunzi umeanza na unatarajiwa kumalizika Disemba, 2012;
- Mafunzo ya kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji yametolewa kwa wakulima 500 wa Weni na Mangwena kwa Pemba na Kibokwa kwa Unguja;
- Chuo kimepata usajili wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi – *NACTE*.

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kimelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 130 wa Cheti na 20 wa Diploma;
- Kujenga bweni la wanafunzi wa kike;
- Kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima wa mpunga kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE* II.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Chuo kiliombewa Tsh. 500,000,000 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Chuo kimepatiwa jumla ya Tsh 495,000,000 sawa na asilimia 99 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Chuo kinaombewa jumla ya Tsh. 500,000,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Naibu Spika, Idara ina jukumu la kulinda na kuhifadhi misitu ya asili na wanyama pori, kusimamia mashamba ya misitu na mbegu, upatikanaji wa miche bora, kuhamasisha wakulima kilimo cha biashara na kuratibu uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imelenga kutekeleza malengo kama ifuatavyo:

- Kuzalisha miche 1,000,000 ya matunda, viungo, misitu na mapambo;
- Kuanza utaratibu wa kupandisha hadhi ya Msitu wa Hifadhi ya Masingini na Msitu wa Muyuni – Jambiani;
- Kupeleka huduma za gesi ya kupikia Pemba;
- Kuanza kuhifadhi vianzio vya maji vilivyomo nje ya misitu ya hifadhi;
- Kupanda miti ya misitu katika eneo la hekta 80 na kuvuna mita za ujazo 3,000 kwenye mashamba ya Serikali;
- Kuandaa na kutekeleza mipango ya misitu ya vijiji.

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Miche 591,000 ya mikarafuu imeoteshwa;
- Miche 2,500,000 ya misitu,viungo, mapambo na matunda imeoteshwa;
- Upandishaji hadhi msitu wa Masingini umeanza kwa kuchora ramani na uwekaji wa mipaka. Aidha, hekta 440 za Msitu wa Muyuni - Jambiani zimepimwa na ramani imechorwa;
- Huduma ya gesi Pemba tari imepelekwa;
- Utafiti katika vyanzo vya maji umefanyika na imebainika kuwa vyanzo vya maji vimevamiwa na mtiririko wa maji umepungua;
- Hekta 100 za mashamba ya Serikali imepandwa miche ya misitu na mita za ujazo 700 zimevunwa. Aidha, upandaji wa mikandaa hekta 10 Ambasha na Micheweni, Pemba Upandaji wa hekta 9 katika maeneo yaliochimbwa mchanga Donge, Unguja umefanyika;
- Mipango ya Usimamizi wa Rasilimali za Misitu ya Jamii 42 imekamilika kwa hatua za awali.

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuotesha miche 1,000,000 ya mikarafuu pamoja na kufanya Sensa;
- Kuotesha miche 1,000,000 ya matunda, viungo, misitu na mapambo katika vitalu vya Serikali;
- Kupanda miti ya misitu eneo la hekta 100;
- Kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu na kilimo cha mazao ya biashara;
- Kufanya tathmini ya akiba ya mchanga;
- Kurejeshea maeneo yanayochimbwa matofali ya mawe na mchanga hekta 10;
- Kufanya tathmini ya misitu na miti iliyopo Zanzibar (*Wood biomass*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara itasimamia miradi mikuu minne ambayo ni:

- Mradi wa Mpango wa Taifa wa Uimarishaji Mikarafuu; (Kiambatisho 6.)
- Mradi wa Hifadhi Misitu ya Asili (*HIMA*); (Kiambatisho 7)
- Mradi wa Hifadhi wa Misitu ya Ukanda wa Pwani; (Kiambatisho 8)
- Mradi wa Kuangamiza Adui Kunguru.

Mhe. Naibu Spika, Mradi wa Kuangamiza Kunguru ni mpya umeanza mwezi Machi, 2012 na unatarajiwa kutumia Tsh. 474,180,000 kutoka Serikali ya Finland. Lengo kuu

la mradi huu ni kuangamiza kunguru wote walioko Unguja na Pemba kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira na wanajamii.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliombewa Tsh. 3,736,694,053 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Idara imepatiwa jumla ya Tsh 3,205,036,673 sawa na asilimia 86 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara inaombewa kutumia jumla ya Tsh. 1,679,140,000 kutoka Serikalini na Tsh 2,019,954,000 kutoka kwa Wahisani.

IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina jukumu la kuratibu kazi za uhakika wa chakula na lishe ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa juu ya matukio yanayohusiana na hali ya uhakika wa chakula na lishe hapa nchini.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imelenga kutekeleza malengo kama ifuatavyo:

- Kuratibu masuala ya uhakika wa chakula na lishe;
- Kufanya upembuzi yakinifu (*feasibility study*) juu ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*National Food Reserve*);
- Kukamilisha Sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo na kuandaa Mpango wa Utekelezaj wa Sera;
- Kuweka na kutekeleza mfumo wa kukusanya na kutoa taarifa ya Uhakika wa chakula nchini na tahadhari ya mapema (*Early Warning*);
- Kukarabati maghala ya akiba manne ikiwa ni matayarisho ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Uanzishwaji wa kamati zinazosimamia masuala ya uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za Taifa, Wilaya na Shehia kama ifuatavyo:

    i. Baraza la Kitaifa la Kusimamia Uhakika wa Chakula na Lishe (*National Food Security and Nutrition Council*);

    ii. Kamati Tendaji ya Makatibu wakuu kutoka wizara zenye majukumu la kusimamia masuala ya uhakika wa chakula na lishe (*Intersectoral-Steering Comittee*);

iii. Kamati za maendeleo ya Wilaya ambazo zitakuwa na jukumu la kusimamia masuala ya uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za wilaya na shehia;

iv. Kamati za Uhakika wa chakula na Lishe katika Shehia.

- Upembuzi yakinifu juu ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa umekamilika. Upembuzi huu unatoa maelekezo juu ya masuala yafuatayo:

    i. Utaratibu wa kuanzisha na kuendesha hifadhi ya chakula ya Zanzibar;

    ii. Mafunzo yanayohitajika kwa watendaji watakaosimamia hifadhi hiyo;

    iii. Fedha zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati wa maghala, ununuzi wa nafaka na vifaa vinavyohitajika;

    iv. Mapendekezo juu ya mfumo wa kisheria unaohitajika katika kuendesha hifadhi ya chakula;

    v. Maelekezo juu ya viwango vinavyohitajika vya maghala ya kuhifadhia chakula;

    vi. Mapendekezo juu ya tafiti zinohitaji kufanyika ili kuwa na taarifa za kina zitakazopelekea hifadhi ya chakula ya taifa kuendeshwa kwa ufanisi pasi na kuweko kwa hasara kwa upande wa Serikali na Sekta binafsi;

- Mfumo wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za Uhakika wa Chakula na Lishe na kutoa tahadhari ya mapema umeandaliwa;

- Vipindi viwili vya televisheni juu ya elimu ya lishe, afya na malezi bora kwa watoto walio chini ya miaka mitano vimetayarishwa na kurushwa kwa mashirikiano na kitengo cha lishe kilicho chini ya Wizara ya Afya;

- Mkutano wa wadau kujadili hali ya lishe nchini, kuibua aina ya miradi ya lishe ambayo itatekelezwa chini ya ufadhili wa *USAID* kupitia Program ya Mwanzo Bora na kuainisha maeneo ambayo yatafaidika na mpango huo ulifanyika;

- Tathmini ya awali ya mahitaji ya ukarabati wa Maghala manne ya akiba imefanyika na kazi ya kukarabati maghala hayo inatarajiwa kufanyika katika mwaka ujao wa fedha;

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuendelea kuratibu ushiriki wa Sekta na Taasisi mbali mbali katika kutekeleza Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe, Sheria namba 5 ya mwaka 2011;
- Kutoa mafunzo kwa wadau juu ya ukusanyaji, uchambuzi na uandishi wa ripoti juu ya masuala ya uhakika wa chakula na lishe;
- Kuendeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na utowaji wa tahadhari ya mapema juu ya hali ya Uhakika wa Chakula na Lishe nchini;
- Kukarabati maghala ya akiba;
- Kutoa elimu ya lishe na afya bora kwa jamii kwa njia ya redio na televisheni pamoja na taarifa nyengine za hali ya uhakika wa chakula nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliombewa Tsh. 1,043,616,000 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 878,473,365 sawa na asilimia 84 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara inaombewa kutumia jumla ya Tsh. 629,760,000 kutoka Serikalini na Tsh. 236,592,000 kutoka kwa Wahisani.

IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ina majukumu ya kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini pamoja na kutoa utaalamu kiufundi wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu, kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji katika utekelezaji wa kazi za kila siku za utunzaji wa vianzio vya maji. Idara pia inatoa huduma za elimu na pembejeo za kilimo kwa wakulima wa umwagiliaji maji.

MALENGO KWA MWAKA 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imelenga kutekeleza malengo yafuatayo**:**

- Kusimamia ujenzi wa miundombinu mipya ya umwagiliaji maji kwa ekari 237 ili kufikisha jumla ya eneo la kilimo cha umwagiliaji la ekari 1987 Unguja na Pemba; katika mabonde ya Bumbwisudi, Kisima Mchanga, Kilombero, Kikobweni, Koani, Ubago, Kwajibwa na Kiboje Mwembeshauri;

- Kujenga mtaro mkuu wa mita 500, kujenga matuta katika ekari 25 bonde la Koani;

- Kukamilisha uwekaji wa umeme katika kituo cha Saninga, Mtwango na Makombeni;

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabwana/mabibishamba 40 Unguja na Pemba;

- Kusomesha wafanyakazi wawili Msc na wanane kwa kiwango cha Diploma;
- Kutoa mafunzo kwa wakulima 120 wa bonde la Kibokwa;
- Kutayarisha vishamba 10 vya maonesho ili kuongeza taaluma kwa wakulima wa mpunga na mbogamboga katika mabonde ya umwagiliaji maji;
- Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika maeneo mawili ya vituo vya uzalishaji mbegu ekari 65 ambapo Kibonde Mzungu ekari 40 na Ole ekari 25;

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2011/2012

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Visima viwili vya kumwagilia vimechimbwa Bumbwisudi na kimoja Makombeni na majaribio ya wingi wa maji yamefanyika;
- Transfoma na pampu mpya imenunuliwa na imefungwa Cheju/Jendele;
- Pampu mpya na Transfoma imewekwa bonde la Saninga;
- Pampu ya kisima cha Uzini imetengenezwa na inafanya kazi;
- Motor mpya ya aina Franklin ya kisima cha *Grass- root* Kibokwa imefungwa na pampu inafanya kazi;
- Bumbwisudi (*Field* 7) transfoma mpya, umeme na pampu mbili za visima zimefungwa na zinafanya kazi;
- Transfoma mpya, umeme na pampu ya kisima Cheju imefungwa;
- Ujenzi wa vibanda vya pampu katika bonde la Cheju, Bumbwisudi na Makombeni umefanyika;
- Mitaro ya saruji ya kumwagilia mita 3,750 imejengwa katika vituo vya Bumbwisudi, Cheju/Ndijani, Uzini, Kinyakuzi, Makombeni, Mipopooni na Kianga;
- Mitaro ya udongo mita 1,620 imejengwa katika vituo vya Cheju/Jendele, Bumbwisudi Field (No.5) na Kwa Dobi - Pemba;
- Mitaro ya kutolea maji mita 3,270 imechimbwa Kinyakuzi, Bumbwisudi na Mipopooni;
- Mtaro wa kuzuia mafuriko (flood drain) mita 1,140 umejengwa Kinyakuzi;

- Tuta la kuhifadhia maji ya kumwagilia (*Reservoir dam*) limejengwa bonde la Kwa Dobi;

- Vidaraja vidogo *(foot bridges*) vinne (4) vimejengwa bonde la Kinyakuzi na Kikobweni;

- Barabara ya kiwango cha kifusi mita 1000 imejengwa Bumbwisudi;

- Vyanzo vya maji vya Mto Mawe, Kikobweni na Kianga vimepandwa miti na kupigwa matuta ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi;

- Upimaji na uchoraji wa ramani na usanifu wa miundombinu umefanyika Kibondemzungu, Ubago, Koani, Muyuni, Kiboje mkwajuni, Mchangani kwa Unguja na Ole, Msaani, Kwajibwa, Mziwanda na Wapape kwa Pemba; ramani hizi zimewasilishwa JICA kwa kuombewa ufadhili;

- Vishamba vya maonesho kumi vilitayarishwa Cheju, Kibokwa, Bumbwisudi, Ubago, Kianga na Uzini kwa Unguja na Mangwena, Tungamaa, Saninga na Tibirinzi kwa Pemba;

- Uandishi wa Miradi sita mipya ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji (Ubago, Koani, Muyuni, Kiboje, Mchangani na Kwajibwa) ulifanyika na kuwasilishwa *JICA* kwa kuombewa fedha na;

Mhe. Naibu Spika, mbali na malengo iliyojipangia kwa mwaka 2011/2012 Idara pia imejenga matuta ya kuzuia uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya mashamba ya Mziwanda - Micheweni mita 787 na Koowe –Wete mita 230.

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kukamilisha ujenzi wa miundombinu kwa ekari 300 za maeneo yanayofaa kwa kilimo cha Umwagiliaji maji**;**

- Kutekeleza Mpango maalum wa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji kama ifuatavyo:
  - ✓ Kujenga mitaro ya saruji mita 800 pamoja na vigingi vyake;
  - ✓ Kujenga msingi wa udongo mita 1000;
  - ✓ Ukarabati wa njia za shambani mita 1,000, mabanio, pampu na visima, pamoja na ofisi na ghala za mashambani;
  - ✓ Kuchimba visima sita na kununua pampu sita pamoja na uwekaji wa umeme katika vituo vya Kiboje Mkwajuni, Kibokwa, Kibonde Mzungu, Cheju, Bumbwisudi na Ole;

- ✓ Ujenzi wa vibanda sita vya pampu (*pump house*) pamoja na ofisi mbili mpya;

- ✓ Uwekaji wa umeme katika visima vya bonde la Mtwango kwa Unguja na Machigini na Makombeni kwa Pemba na;

- ✓ Utayarishaji wa ardhi hekta 80 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliji maji;

- Kutoa mafunzo kwa wakulima na wafanyakazi wa sekta ya umwagiliaji maji;

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara iliombewa shilingi 1,973,694,298 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2012 Idara imepatiwa jumla ya shilingi 1,940,403,492 sawa na asilimia 98 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara inaombewa jumla ya shilingi 1,120,380,000 kutoka Serikalini.

CHANGAMOTO ZA WIZARA:
Mhe. Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika msimu huu wa kilimo bado tulikabiliwa na changamoto nyingi kama ifuatavyo:-

- Kutokana na kiwango cha ruzuku kilichowekwa pamoja na uhamasishaji juu ya matumizi ya pembejeo na faida zake kumekuwa na mahitaji makubwa kuliko ilivyotarajiwa katika makisio. Hali hii imesababisha baadhi ya wakulima kukosa huduma na pembejeo hizo kwa wakati;

- Mabadiliko ya hali ya hewa, kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha mvua za Vuli zilizonyesha kwa muda wa miezi miwili zilipelekea kuchelewa kwa kazi za ukulima wa matrekta ilisababisha huduma za matrekta kutofanyika kama ilivyopangwa kwa baadhi ya maeneo;

- Kuharibika kwa baadhi ya matrekta pia kulichangia kwa kiasi fulani kutokuwalimia wakulima wote kwa wakati;

- Uvamizi wa maeneo ya kilimo kwa suala la makaazi ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa mchanga na ukataji wa matofali Pemba;

- Ongezeko kubwa la mahitaji ya mazao ya maliasili kuliko uwezo wa uzalishaji;

- Matumizi mabaya ya zana zinazopelekea uharibifu wa mazingira ikiwemo msumeno wa moto;

MFUMO WA BAJETI UNOZINGATIA *PROGRAM*:
Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata maendeleo endelevu imeamua

kuanzisha mfumo wa bajeti kwa kuzingatia programu na miradi husika **(***Programs Based Budget***)**. Katika kutekeleza azma hio, Wizara sita zimeteuliwa kwa majiribio kutekeleza bajeti zao kwa kuzingati mfumo huo wa program na miradi husika na Wizara ya Kilimo na Maliasili ni miongoni mwa Wizara hizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako Tukufu lipokee muhutasari wa bajeti itakayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Maliasil kwa kuzingztia mfumo wa programu. Ni imani yangu kwamba Wajumbe wa Baraza letu Tukufu wataupitia muhtasari huu na kuelewa utaratibu wa mfumo huu wa bajeti unaozingatia programu na miradi husika.

SHUKRANI:

Mhe. Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo, zikiwemo nchi za Japan, Finland, Norway, Ireland, China, India, Israel, Mouritius, Korea ya Kusini, Marekani, Misri na Uholanzi. Aidha, Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *IFAD, UNDP, FAO, JICA, UNICEF, WFP, USAID, KOICA, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, Rockfeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation*. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyonayo. Napenda kuwashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Naibu Katibu Mkuu wa Kilimo, Naibu Katibu Mkuu wa Maliasili pamoja na Wakurugenzi wa Idara; Taasisi na Asasi zote zilizo chini ya Wizara hii; watumishi wote wa Wizara pasi na kuwasahau na wadau wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2011/2012 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. *(Makofi)*

Ni matarajio yangu kwamba Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2012/2013. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii.

MAKADIRIO YA MAOMBI YA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 23,827,116,000/= kati ya hizo shilingi 11,820,000,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 500,000,000/= ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani na shilingi 11,507,116,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi 11 ya maendeleo ambapo shilingi 2,090,000,000/= ikiwa ni mchango wa Serikali na kwa upande wa wahisani wa maendeleo ni shilingi 9,417,116,000/=.

Kiambatanisho. 1. Programu ya Kuendeleza Huduma za Kilimo - *(ASSP)*
MWAKA ULIOANZA: Programu ilianza mwezi Juni ya mwaka wa fedha 2006/2007

MALENGO 2011/2012	**UTEKELEZAJI**
Kuendelea kuwapatia mafunzo wakulima katika fani za *SACCOS* na usarifu wa mazao;	Jumla ya wakulima 45 walipata ma pamoja na mafunzo ya usarifu w Donge-Unguja na Matangatuani –P vya kilimo vya shamba darasa mafunzo ikiwemo ya SACCOS ka Pemba;
Kujenga bweni katika chuo cha Kilimo Kizimbani;	Mchakato mzima wa taratibu za n wa bweni zimekamilika na ujenzi um
Kuendelea kusaidia vituo vya kupashana habari Unguja na Pemba	Fanicha kwa ajili ya vituo 2 vya ku Micheweni Pemba zimenunuliwa;
Kupeleka wakulima katika ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara;	Jumla ya wakulima 18 walipelekwa nane yaliyofanyika Dodoma;
Kuimarisha shughuli za utafiti katika vituo vya utafiti na mashamba ya wakulima;	Ununuzi wa "polythene bags" kw Kizimbani umefanyika sambamba na tano ya uanganishi wa masoko n mazao kwa vikundi vya Unguja na P
Kuendeleza uzalishaji wa mbegu bora za mpunga ,mahindi na kunde;	Mafunzo kwa ajili ya uzalishaji mahindi na kunde katika viku yamefanyika Unguja na Pemba
Kuwapa mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wa Programmu;	Mafunzo ya kompyuta kwa mamb yalifanyika pamoja na mafunzo wafanyakazi wa programmu.

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

- Kuendelea kuvipa taaluma za kilimo bora vikundi 108 vya skuli za wakulima kwa kwa mzu masomo vinane.
- Kujenga bweni katika chuo cha Kilimo Kizimbani.
- Kuendelea kusaidia vituo vya kupashana habari.
- Kupeleka wakulima katika ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara.
- Kuimarisha shughuli za utafiti katika vituo vya utafiti na mashamba ya wakulima.
- Kuendesha warsha ya wadau kuhusu mapitio ya utekelezaji wa kazi za Programu kwa kipindi
- Kuwapa mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wa Programmu
- Kuendesha vikao vya kamati ya uongozi na, vikao vya wawezeshaji wa wilaya

Kiambatanisho. 2. Programu ya Kuendeleza Sekta za Mifugo *(ASSP-L)*
MWAKA ULIOANZA: Programu ilianza mwezi Juni mwaka wa fedha 2006/2007

MALENGO 2011/2012	**UTEKELEZAJI**
Kuvipa taaluma vikundi 360 vya skuli za wakulima wafugaji na vikundi 30 vilivyoibuka venyewe;	Mafunzo kwa ajili ya vikundi 36 wafugaji pamoja na vikundi vilivyoil

Kuwapatia mafunzo wawezeshaji 180 wakulima/mifugo na wazalishaji wa mbuzi;	Mafunzo kwa ajili ya wawezeshaji yalitolewa
Kukarabati vituo 5 vya afya ya wanyama na maabara 2 za mifugo za Unguja1 na Pemba 1.	Ukarabati wa vituo 3 vya afya vya 2 ulifanyika;
Kununua vifaa kwa ajili ya vituo 5 vya afya ya wanyama pamoja na maabara 2 za mifugo za Unguja (1) na Pemba (1);	Vifaa kwa ajili ya vituo 3 vya a maabara 2 vimenunuliwa
Kununua chanjo 900,000 za maradhi ya mahepe na kuzigawa katika Shehia 90 za programmu;	Jumla ya dozi 900,000 za chanj pamoja na kukamilisha zoezi la Unguja na Shehia 40 za Pemba;
Kununua dozi 1,600 za chanjo ya vibuma kwa ndama 1,600;	Jumla ya dozi 320 za chanjo ya kuchanjwa ndama 320 Unguja na P
Kusaidia kuweka mitambo mitano ya biogas kwa wafugaji.	Mitambo mitano ya Biogas ilikamili Pemba

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

- Kuwapatia mafunzo msasa watoa huduma za msingi za mifugo 50;
- Kuengeza watoa huduma za msingi za mifugo wapya 45 na kuwapatia mafunzo ya siku 40 pa kwa ajili ya kuanzia kazi za utoaji wa huduma hizo;
- Kuwapatia mafunzo msasa wawezeshaji 100 wakulima na mifugo;
- Kuanzisha vikundi vipya 300 vya wakulima na wafugaji na kuvipatia mafunzo bora;
- Kuendelea kuvipa taaluma za kilimo bora vikundi 72 vya skuli za wakulima;
- Kuendelea kuvipa taaluma za kilimo na ufugaji bora vikundi 700 vya skuli za wakulima;
- Kununua chanjo za maradhi ya mahepe dozi 900,000 na kuzikabidhi katika Idara ya Huduma Mifugo;
- Kununua chanjo za maradhi ya vibuma dozi 2,000 na kuzikabidhi katika Idara ya Huduma ya Utal
- Kuwapatia wafugaji ziara za mafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara;
- Kununua mashine 3 za kutotolea vifaranga na mashine 5 za kusarifu maziwa kwa ajili ya wafugaji

KIAMBATANISHO Nam. 3 MRADI WA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO (AGRO- PROCESSING)

Muda wa Mradi: Miaka mitatu, (Julai 2010/Juni 2013**) Gharama/Wachangiaji. K**OICA: US $ 2.300 milioni
Lengo kuu: Kujenga uwezo wa wakulima juu ya usarifu wa mazao na ujasiriamali pamoja na kutoa ubora kwa bidhaa zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza ajira na kipato kwa wazalishaji.
Gharama kwa mwaka 2011/2012: US$ 800,000 KOICA na SMZ Sh. 211,700,000

Utekelezaji 2011/2012: • Utafiti juu ya hali ya wajasiriamali wa usarifu wa mazao umefanyika • Kazi ya kuunga umeme katika jengo la usarifu wa mazao inaendelea. • Kazi nyengine zilizopangwa hazikuweza kutekelezwa kutokana na kukosekana fedha zilizohitajika
Gharama kwa mwaka 2012/2013: US$ 0.8 milioni – KOICA na SMZ Sh. 150,000,000
Malengo ya mwaka 2012/2013: • Kukamilisha kazi ya uungaji wa umeme na kufunga vifaa na mashine za kusarifu mazao pamoja na • Kutoa mafunzo kazini kwa wafanyakazi juu ya matumizi ya vifaa na mashine zilizofungwa kwa ubora; • Kutoa mafunzo kwa wadau 80 (wajasiriamali) pamoja na kuandaa ziara za kimafunzo kwa wazalishaji ndani na nje ya nchi; • Kutoa huduma za udhibiti wa ubora kwa mazao yaliyosarifiwa kupitia maabara; • Kukarabati njia ya kuingilia eneo la kituo (Access road) kwa kiwango cha kifusi.

Kiambatanisho. 4. Programu ya Miundombinu ya Masoko - MIVARF

MWAKA ULIOANZA: 2011/2012

MALENGO 2011/2012	**UTEKELEZAJI**
• Kutayarisha mazingira ya kufanyia kazi na kuteua watendaji wa Programu;	Uteuzi wa watendaji wa Progra matengenezo ya ofisi za kudumu; za 2012;
• Kutoa mafunzo ya uelewa wa mundo na misingi ya utekelezaji wa Programu kwa watendaji;	Mafunzo ya uelewa wa muundo Programu kwa watendaji wakuu w 2011;
• Kufanya uzinduzi wa Programu;	Programu ilizinduliwa tarehe 29 No wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi;
• Kufanya mikutano ya uelewa (sensitization meetings) Program kwa wadau katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya na Jamii;	Mikutano ya uelewa (sensitizat imefanyika katika ngazi ya Taifa, Ml
• Kununua vifaa (samani na vitendeakazi) vya kusaidia utendeaji wa kazi;	Vifaa vya kusaidia utendaji wa kazi nk. Vimenunuliwa;
• Kuunda Kamati za Ushauri na Usimamizi wa Kazi za Programu za Mikoa na Wilaya;	Kamati za Ushauri na Usimamizi wa Wilaya zimeundwa pamoja na kute hizo;
• Kufanya mikutano ya uelewa wa kina wa majukumu ya Kamati zaUshauri za Mikoa na Wilaya na taratibu za utekelezaji wa Programu;	Mikutano ya uelewa wa majukumu y za utekelezaji wa Programu imefany za Unguja na Pemba;
• Kuwezesha vikao vya Kamati ya Kisekta ya Usimamizi	Programu imewezesha kufanyika

wa Programu.	Kisekta ya Usimamizi wa Programu.

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

- Kukarabati barabara za mashambani kilomita 50;
- Kuwajengea uwezo na kuwaunganisha na masoko wazalishaji wadogo wadogo;
- Ununuzi na ufungaji wa mitambo miwili ya kuzalisha barafu;
- Kutoa mafunzo ya upangaji, utekelezaji na utunzaji wa miradi ya miundombinu;
- Kuandaa ziara za kimasomo (kwa vikundi) kwenye masoko na kwa wasindikaji mazao;
- Kuwapatia mafunzo wazalishaji juu ya uhifadhi na usarifu wa mazao na;
- Kuwapatia mafunzo ya kujenga uwezo wafanyakazi wa Idara ya Ushirika, SACCOS pamoja na w

Kiambatanisho. 5. Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe

MALENGO 2011/2012	**UTEKELEZAJI**
Kuratibu masuala ya Uhakika wa chakula na Lishe;	Kamati zenye jukumu la kusimamia Uhakika wa Chakula na Lishe zim na Mhe. Rais wa Zanzibar hivi karil
Kufanya upembuzi yakinifu (feasibility study) juu ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (National Food Reserve);	Upembuzi yakinifu juu ya uanzishw umekamilika na mapendekezo na hatua za kuchukuwa katika kuanzis Idara tayari imeanza kuyafanyia Mapendekezo hayo ni pamoja na ku ujuzi, kuandaa utaratibu wa kuhusis
Kukamilisha sera ya Masoko ya Bidhaa za Kilimo na kuandaa Mpango wa Utekelezaji;	Sera ya Masoko ya Bidhaa za imewasilishwa katika kamati ya m na kuanza kwa utayarishaji wa M Sera hiyo;
Kuweka na kutekeleza mfumo wa kukusanya na kutoa taarifa ya Uhakika wa Chakula nchini na tahadhari ya mapema (Early warning);	Rasimu ya mfumo wa ukusanyaji n Uhakika wa Chakula na Lish imepelekwa WFP na FAO kwa kup
Kukarabati maghala ya akiba manne ikiwa ni matayarisho ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa;	Utaratibu umeanza katika kazi h maelekezo kutoka kwa wataalan yakinifu. (Feasibility Study) juu y ya Chakulaya Taifa;

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

- Kuandaa mikutano kwa kamati zinazosimamia masuala ya uhakika wa chakula na lishe;
- Kukamilisha utaratibu wa kuanzishwa kwa maghala ya akiba ya chakula nchini;
- Kutoa mafunzo kwa kamati za uhakika wa chakula na lishe Wilaya za Mkoani na Wete kwa Pe Kaskazini "A";
- Kuanzisha na kutoa mafunzo kwa kamati za uhakika wa chakula na lishe za Shehia nne ziliomo ka

Wete kwa Pemba na Wilaya ya Kati na Kaskazini "A" (shehia mbili kwa kila Wilaya);

- Kutoa mafunzo kwa wadau juu ya ukusanyaji, uchambuzi na uandishi wa ripoti ya masuala ya uha
- Kuendeleza mfumo wa ufatiliaji na tathmini (M&E) na utowaji wa tahadhari ya mapema juu ya h na Lishe nchini.

Kiambatanisho. 6 Mradi wa Uimarishaji Mikarafuu

Lengo kuu: Kuengeza pato la mkulima na taifa kwa ujumla.

Malengo mahususi:

- kuimarisha zao la karafuu kwa kuotesha miche bora
- kupanda upya mashamba ya mikarafuu
- kutoa elimu na kufanya utafiti.

MALENGO	**UTEKELEZAJI**
Kuzalisha miche 500,000 ya mikarafuu	Miche 500,000 imeoteshwa, miche ndio itakayoweza kupandwa katika n
Kufanya matengenezo ya mabanda 10 ya kuzalisha miche ya mikarafuu	Mabanda manne ya kudumu yamej matengenezo
Kutoa elimu ya upandaji na utunzaji wa mikarafuu wilaya saba (7) za Unguja na Pemba	Elimu ya kuendeleza zao la karafuu (3) Unguja na Wilaya nne (4) Pemba isipokua wilaya ya Mkoani wal yametolewa kwa njia ya Radio kipi ZBC kipindi kimoja
Kufanya tathmini ya mikarafuu iliyopandwa baada ya msimu	Tathmini imeanza kwa kukusanya kutembelea mashamba ya mikarafuu
Kufanya sense ya mikarafuu	Makadirio ya gharama ya sensa yam Tsh. 303,131,352 zinahitajika kwa zo

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

- Kuzalisha miche 500,000 ya mikarafuu;
- Kutengeneza mabanda ya miche ya kudumu manne;
- Kutoa elimu bora ya kilimo cha mikarafuu;
- Kufanya sense ya mikarafuu;
- Kufanya tathmini ya mazao ya viungo.

Kiambatanisho. 7 - Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili (HIMA)

Lengo kuu: Kupunguza Hewa Mkaa kutokana na ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu.

MALENGO	UTEKELEZAJI
Kuendelea na mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa Rasilimali za Misitu ya Jamii	Mipango 40 ya Misitu ya Jami imewasilishwa Wizara ya Kilimo na kutangazwa katika gazeti la Serikali ya Matumizi ya Ardhi.
Kuelimisha jamii kuhusu MKUHUMI hadi katika ngazi za wilaya	Elimu ya MKUHUMI imetolewa ka Pemba (Wilaya ya Kusini , Wilaya ”B” kwa Unguja na Wilaya ya Ch Micheweni)
Kusaidia jamii kuanzisha mashamba ya misitu hekta 100 ili waweze kujipatia mahitaji ya nishati na majengo	Jumla ya miche 118,000 sawa na malipo kwa wenye mashamba bina Uroa kwa Unguja,
Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 15 wa Idara ya Misitu na Maliasili yanayohusu MKUHUMI na mabadiliko ya tabia nchi	Wafanyakazi watano wamehudhuria MKUHUMI Afrika ya Kusini, wafa mafunzo ya mabadiliko ya tabia wafanyakazi watatu wamehudh MKUHUMI, Nepali
Kufanya utafiti wa mabadiliko ya tabia nchi hapa Zanzibar ili kutambua athari ambazo zimejitokeza Zanzibar	Utafiti wa kufahamu athari za umefanyika ambapo umeonyesha se visiwa vya Zanzibar zimeathirika ku maji ya bahari
Kufanya utafiti wa kujua matumizi makuu ya misitu kwa jamii, upotevu wake na kuandaa mikakati ya kusaidia jamii kiuchumi ili kupunguza matumizi ya misitu ya asili	Utafiti umepangwa kufanyika mwaka
Utoaji wa gesi bure kwa wananchi wanaotaka kuachana na matumizi ya kuni na mkaa	Kaya 366 za Mjini Magharibi zilif bila ya malipo

Malengo ya mwaka 2012/2013

- Kuwajengea uwezo Kamati 29 za Mipango ya Usimamizi wa Rasilimali za Misitu ya Jamii;
- Kuelimisha jamii kuhusu MKUHUMI;
- Kupanda miche ya misitu hekta 200;
- Kutegeneza vitalu vya kudumu vitano na Kujengea uwezo vitalu binafsi 20;
- Kufanya tathmini ya hewa mkaa na tathmini ya matumizi ya gesi ya kupikia (LPG;)
- Kuwezesha vitalu binafsi 22 Unguja na Pemba.

Kiambatanisho. 8. Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Ukanda wa Pwani

MALENGO	UTEKELEZAJI
Kuweka mipaka ya kudumu katika maeneo ya Misitu ya Hifadhi ya Kiwengwa, Masingini, Ras Kiuyu na Msitu mkuu	Vigingi 250 vya zege vimechomekwa kukam mpaka wa Hifadhi ya Masingini yenye ukubw ramani ya eneo la msitu huo imechorwa; vigin Hifadhi ya Msitu wa Ngezi vimekaguli vilivyong'olewa vimerejeshewa upya na rama vigingi 75 vya Hifadhi ya Taifa – Joz vimerejeshewa upya na eneo la Hifadhi limech Hifadhi ya Msitu wa Kiwengwa limekaguliwa na 70 vilivyong'olewa
Kuanzisha utaratibu wa kupandisha hadhi ya Msitu wa Hifadhi ya Masingini kuwa Hifadhi ya Kimaumbile na kufanya matayarisho ya kutangaza Msitu wa Muyuni Jambiani kuwa msitu wa Hifadhi	Kazi ya kuandaa Mpango wa Hifadhi ya Masingi kwa uwekaji mipaka na uchoraji wa ramani; katik Muyuni kuwa Msitu wa Hifadhi jamii imehamasi juu ya mpango wa Serikali kufanya hifadhi, utafi kutambua rasilmali – asili zilizomo katika ms hatuwa ya awali ya kulipima eneo la msitu huo jumla ya hekta 4,200 zimepimwa na ramani hus mswada wa mapendekezo ya kulitangaza eneo h kuwasilishwa Wizarani kwa hatuwa ya Waziri ku ili wananchi waweze kutoa na kusikilizwa madai y ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuufanya l Hifadhi.
Kuimarisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka	Mipaka ya Hifadhi ya Taifa Jozani-Ghuba ya ukaguzi na jumla ya vigingi 75 vimerejesh kutayarisha ramani mpya.

Malengo ya mwaka 2012/2013

- Kuweka mipaka ya kudumu katika maeneo ya misitu ya Hifadhi ya Kiwengwa, Ras Kiuyu na
- Kuendeleza utaratibu wa kupandisha hadhi ya msitu wa hifadhi ya Masingini kuwa hifadhi ya
- kutangaza Msitu wa Muyuni - Jambiani kuwa msitu wa Hifadhi ya Akiba;
- Kukamilisha mpango wa usimamizi wa Msitu wa Hifadhi ya Masingini na kupitia mipa Hifadhi za Ngezi, Kiwengwa –Pongwe , na Jozani na Ghuba ya Chwaka.

KIAMBATANISHO Nam. 9 MRADI WA UKARABATI NA UJENZI WA MAABARA YA UTAFITI KIZIMBANI (TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO).

Muda wa Mradi: Mwaka (Novemba 2011 hadi Novemba, 2012

Gharama/Wachangiaji. KAMISHENI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA - COSTECH: **Tsh. 641,650,000/=**

Lengo kuu: Kuongeza uwezo wa Taasisi ya utafiti katika kutoa matokeo mazuri ya tafiti.

Gharama kwa mwaka 2011/2012: Tsh. 300,000,000

Gharama kwa mwaka 2011/2012: Tsh. 341,650,000/=

Utekelezaji 2011/2012:

Fedha hizo zimetumika kwa kazi ya utayarishaji wa mikataba ya ujenzi (Tendering) na kuanza kwa

Malengo kwa mwaka 2012/2013:

Taasisi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 inatarajia kutumia jumla ya Tsh. 341,650,000/= kwa kue ujenzi wa maabara pamoja na kuzifanyia ukarabati maabara zilizopo.

KIAMBATANISHO Nam. 10 CHUO CHA KILIMO

MRADI WA KUWAWEZESHA MASKINI KITAALUMA KATIKA MATUMIZI YA MALIASILI NA KUONGEZA THAMANI YA MAZAO.

(Enhancing Pro poor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value Chain –EPINAV)

Muda wa Mradi: Miaka miwili (Oktoba 2011 hadi Oktoba 2013
Gharama/Wachangiaji. Serikali ya Norway
Fedha za Norway (NOK) = 3,611,000/=

Lengo kuu: Kuwawezesha maskini kitaaluma katika matumizi ya maliasili na kuongeza thamani ya ma

Malengo Mahususi

- Kujenga mazingira mazuri ya kimasomo kwa wanafunzi wa chuo cha kilimo kwa kuwapatia vifaa ili waweze kuwasaidia wakulima, na
- Kuwajengea uwezo wa kitaalamu wakufunzi wa chuo kwa kuwapatia nafasi za masomo ya muda m

Gharama kwa mwaka 2011/2012: NOK. 1,479,413

Utekelezaji 2011/2012:

- Jumla ya Tsh. 238,555,149.41 zilitumika kwa mwaka 2011/2012
- Walimu watano (5) wamejiunga na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine katika ngazi ya Shaha mifugo;
- Walimu 21 wamepatiwa ziara za kimasomo ya muda mfupi katika vyuo vya kilimo na mifugo Tanz
- Kompyuta 10 zimenunuliwa kwa ajili ya kufundishia na huduma za mtandao zimeunganishwa kat ofisi ya Mratibu wa masomo;
- Ununuzi wa vifaa vya maabara na mafunzo umefanyika

Gharama kwa mwaka 2012/2013: NOK. 2,131,587

Malengo ya mwaka 2012/2013:

- Kujenga bweni moja la wanawake;
- Kununua vifaa kwa ajili ya maktaba, maabara na kliniki moja ya mifugo;
- Kuwapatia mafunzo walimu watano (5) katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa ngazi ya ya kilimo na mifugo;
- Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mfupi walimu wa chuo cha kilimo;
- Kufanya mapitio ya mitaala ya Chuo cha Kilimo Kizimbani kulingana na mahitaji halisi ya Zanziba

VOTE: 20: WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

KIFUNGU		MAELEZO	MAKISIO 2011 2011/2012	MAKUSANYO JULAI HADI JUNI 2012	SAV AS
03 OFISI KUU PEMBA					
	142224	MAZAO YA MISITU	20,000,000	143,189,950	
	142225	ADA YA UUZAJI WA MAWE MCHANGA NA KOKOTO	13,000,000	33,802,550	
		JUMLA NDOGO	**33,000,000**	**176,992,400**	
	142254	UKAGUZI WA MAZAO	5,000,000	3,750,000	
	142257	MAUZAJI YA MAZAO	1,000,000	-	
	145001	MAPATO MENGINEYO	1,500,000	346,700	
	142101	MAUZO YA MICHE	1,000,000	1,188,800	
		JUMLA NDOGO	**8,500,000**	**5,285,500**	
		JUMLA PEMBA	**41,500,000**	**182,277,900**	
04 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI					
	145001	MAPATO MENGINEYO	2,000,000	6,456,827	
		JUMLA NDOGO	**2,000,000**	**6,456,827**	
15 IDARA YA KILIMO					
	142281	ADA YA UINGIZAJI WATALII	2,000,000	2,735,200	
	142254	UKAGUZI WA MAZAO	10,000,000	12,097,300	
	142257	MAUZAJI YA MAZAO YA MICHE	8,000,000	11,011,000	
		JUMLA NDOGO	**20,000,000**	**25,843,500**	
	142224	MAZAO YA MISITU	90,000,000	105,955,389	
	142225	ADA YA UZAJI WA MAWE, MCHANGA NA KOKOTO	80,000,000	208,719,240	
		JUMLA NDOGO	**170,000,000**	**314,674,629**	
	142101	MAUZO YA MICHE	5,000,000	10,499,100	
		JUMLA NDOGO	**5,000,000**	**10,499,100**	
		JUMLA UNGUJA	**197,000,000**	**357,474,056**	
		JUMLA KUU	**238,500,000**	**539,751,956**	

KIAMBATANISHO Nam 11 – UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA 2011/2012 NA MAKADIRIO KWA MWAKA 2012/2013

VOTE: 20: WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

KIAMBATANISHO Nam 12 - TAARIFA YA BAJETI NA FEDHA ZILIZOTOLEWA KUANZIA JULAI HADI JUNI 2012 KWA UJUMLA

	IDARA	BAJETI 2011/2012 Kazi za kawaida	BAJETI 2011/2012 Kazi za maendeleo SMZ	BAJETI 201 Kazi za mae Wahisani
1	03 AFISI KUU PEMBA	1,749,366,742	-	
2	04 IDARA YA SERA MIPANGO NA UTAFITI	1,084,793,769	551,240,000	2,126,
3	07 IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA	1,205,114,053	300,000,000	2,231,
4	11 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	573,694,298	1,400,000,000	
5	13 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	170,700,000	-	
6	14 IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA	140,400,000	721,500,000	181,
7	15 IDARA YA KILIMO	3,235,361,974	175,000,000	
8	17 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	145,045,000	452,260,000	
	JUMLA	**8,304,475,836**	**3,600,000,000**	**4,539,8**
	RUZUKU WA CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	**500,000,000**		
	JUMLA KUU	**8,804,475,836**	**3,600,000,000**	**4,539,84**

	FEDHA ZILIZO-TOLEWA 2011/2012 Kazi za kawaida	FEDHA ZILIZO-TOLEWA 2011/2012 (Maendeleo ya SMZ)	FEDHA ZILIZOT-OLEWA 2011/2012 (M'leo ya Wahisani)	Jumla
KUU PEMBA	1,696,871,068	-	-	1,696,871
A YA SERA MIPANGO NA UTAFITI	1,046,975,849	384,057,133	2,188,581,099	3,619,614
A YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA	1,174,777,063	235,000,000	1,795,259,610	3,205,036

A YA UMWAGILIAJI MAJI	546,438,492	1,393,965,000	-	1,940,403
A YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	147,887,080	-	-	147,887
A YA UHAKIKA WA CHAKULA	103,924,200	702,330,000	72,219,165	878,473
A YA KILIMO	3,141,288,475	172,382,963	-	3,313,671
ISI YA UTAFITI WA KILIMO	103,442,254	425,817,448	-	529,259
	7,961,604,481	**3,313,552,544**	**4,056,059,874**	**15,331,216,**
KWA CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	495,000,000	-	-	495,000
KUU	**8,456,604,481**	**3,313,552,544**	**4,056,059,874**	**15,826,216,**

VOTE: 20 WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

KIAMBATANISHO Nam 13 - TAARIFA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA KUANZIA JULAI HADI JUNI 2012 KAZI ZA KAWAIDA

	IDARA	BAJETI 2011/2012	FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI/JUNI 2012	%
1	03 AFISI KUU PEMBA	1,749,366,742	1,696,871,068	97
2	04 IDARA YA SERA MIPANGO NA UTAFITI	1,084,793,769	1,046,975,849	97
3	07 IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESH	1,205,114,053	1,174,777,063	97
4	11 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	573,694,298	546,438,492	95
5	13 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	170,700,000	147,887,080	87
6	14 IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA	140,400,000	103,924,200	74
7	15 IDARA YA KILIMO	3,235,361,974	3,141,288,475	97
8	17 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	145,045,000	103,442,254	71
	JUMLA	**8,304,475,836**	**7,961,604,481**	**96**
	RUZUKU KWA CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	500,000,000	495,000,000	99
	JUMLA KUU	**8,804,475,836**	**8,456,604,481**	**96**

VOTE: 20 WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

KIAMBATANISHO Nam 14 - TAARIFA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA KUANZIA JULAI HADI JUNI 2012 KAZI ZA KAWAIDA.

	IDARA	**MSHAHARA**			**MATUMIZI MENGIN**	
		BAJETI 2011/2012	**FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI/JUNI, 2012**	**%**	**BAJETI 2011/2012**	**FED ZIL JUL**
1	03 AFISI KUU PEMBA	1,450,784,742	1,442,027,068	99	298,582,000	
2	04 IDARA YA SERA MIPANGO NA UTAFITI	579,793,769	72,909,291	99	505,000,000	
3	07 IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA	1,085,114,053	1,069,271,703	99	120,000,000	
4	11 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	477,026,298	466,760,198	98	96,668,000	
5	13 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	-	-	-	170,700,000	
6	14 IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA	-	-	-	140,400,000	
7	15 IDARA YA KILIMO	2,711,756,974	2,695,288,221	99	523,605,000	
8	17 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	-	-	-	145,045,000	
	JUMLA	**6,304,475,836**	**6,246,256,481**	**99**	**2,000,000,000**	
	RUZUKU KWA CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	500,000,000	495,000,000	99	-	-
	JUMLA KUU	**6,804,475,836**	**6,741,256,481**	**99**	**2,000,000,000**	

VOTE 20: WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI.

KIAMBATANISHO Nam 15 - FEDHA ZILIZOTOLEWA KWA MIRADI YA MAENDELEO KUANZIA JULAI, 2011 HADI JUNI 2012

	JINA LA MRADI	MAKISIO 2011/2012 SMZ	FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI/JUNI 2012 SMZ	SAWA NA ASILIMOA (%)	MAKISI 2012/201
	PROGRAM YA KUENDELEZA SEKTA YA KILMO NA MIFUGO (ASDP-L)	50,957,000	40,000,000	78	60,000,0
	PROGRAM YA KUIMARISHA HUDUMA YA KILIMO (ASSP)	126,083,000	65,000,000	52	100,000,
	MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	721,500,000	702,330,000	97	300,000,
	MRADI WA KUKUZA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO	211,700,000	208,497,133	98	150,000,
	MRADI WA USHIRIKISHWAJI WA MAENDELEO YA KILIMO (PADEP)	175,000,000	172,382,963	99	-
	MRADI WA KUIMARISHA MIKARAFUU	300,000,000	235,000,000	78	200,000,
	HIFADHI YA MISITU YA ASILI				100,000,
	UHIFADHI WA MISITU YA PWANI				100,000,
	MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA KILIMO CHA U/MAJI	1,400,000,000	1,393,965,00	99	500,000,
	PROGRAM YA UTAFITI WA KILIMO NA MALIASILI	452,260,000	425,817,448	94	400,000,
	PROGRAM YA MIUNDOMBINU YA SOKO, KUONGEZA THAMANI NA MISAADA VIJIJINI	162,500,000	70,560,000	43	180,000,
	JUMLA	**3,600,000,000**	**3,313,552,544**	**92**	**2,090,000**

VOTE 20: WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI.

KIAMBATANISHO Nam 16 - FEDHA ZILIZOTOLEWA KWA MIRADI YA MAENDELEO KUANZIA JULAI 2011 HADI JUNI 2012

WAHISANI

KASMA	JINA LA MRADI	MAKISIO 2011/2012 WAHISANI	FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI/MEI 2012 WAHISANI
610014	PROGRAMUYA KUENDELEZA SEKTA YA KILMO NA MIFUGO (ASDP-L)	714,734,000	1,250,307,644
610015	PROGRAMU YA KUIMARISHA HUDUMA YA KILIMO (ASSP)	471,939,000	684,178,080
610007	MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	181,716,000	72,219,165
610008	MRADI WA KUKUZA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO	700,000,000	-
610006	MRADI WA USHIRIKISHWAJI WA MAENDELEO YA KILIMO (PADEP)	-	-
610005	MRADI WA KUIMARISHA MIKARAFUU	-	-
610003	HIFADHI YA MISITU YA ASILI	1,500,000,000	1,616,731,350
610002	UHIFADHI WA MISITU YA PWANI	731,580,000	178,528,260
610004	MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA KILIMO CHA U/MAJI	-	-
610016	PROGRAMU YA UTAFITI WA KILIMO NA MALIASILI	-	-
660004	PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA SOKO, KUONGEZA THAMANI NA MISAADA VIJIJINI	239,880,000	254,095,375
	JUMLA	**4,539,849,000**	**4,056,059,874**

VOTE 20: WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI.

KIAMBATANISHO Nam 17 - JUMLA YA MAKISIO YA 2012/2013

NO.	IDARA	BAJETI 2012/2013 KAZI ZA KAWAIDA	BAJETI 2012/2013 KAZI ZA MAENDELEO SMZ	BAJETI 2012/2013KAZI MAENDELEO MUHISANI
1	03 AFISI KUU PEMBA	1,844,094,000	-	-
2	14 IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI	748,236,000	490,000,000	7,160,570,000
3	07 IDARA YA MISITU NA MALI ASILI ZISIZOREJESHEKA	1,279,140,000	400,000,000	2,019,954,000
4	11 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	620,380,000	500,000,000	-
5	13 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	938,760,000	-	-
6	14 IDARAUHAKIKA WA CHAKULA	329,760,000	300,000,000	236,592,000
7	15 IDARA YA KILIMO	5,153,430,000	-	-
8	17 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	906,200,000	400,000,000	-
	JUMLA	**11,820,000,000**	**2,090,000,000**	**9,417,116,000**
	RUZUKU KWA CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI	500,000,000		
	JUMLA KUU	**12,320,000,000**	**2,090,000,000**	**9,417,116,000**

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, ahsante hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Tunakushukuru kwa kutumia muda vizuri. Sasa hoja ianze kujadiliwa na mtu wa mwanzo tunamwita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kwa niaba ya Mwenyekiti wake. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo) Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya Kutoa Hotuba ya Maoni ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai, uzima na afya mpaka tukapata fursa ya kukutana hapa leo kutekeleza majukumu mazito ya ujenzi wa nchi yetu.

Aidha, nitumie nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati yangu, juu ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri muda mfupi uliopita.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia, kutumia fursa hii kutoa mkono wa pole kwa msiba mkubwa uliolikumba taifa kutokana na ajali ya kuzama boti ya M.V *Skagit* wiki chache zilizopita, nawaombea wote waliojeruhiwa na waliopoteza ndugu zao Mungu awape moyo wa subira, na wale waliofariki Mungu awalaze mahala pema peponi, Amin.

Mhe. Naibu Spika, naomba vile vile niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ushirikiano wao wa bega kwa bega uliofanikisha kazi za kamati katika kusimamia wizara hii, hata leo nikaweza kusimama hapa kuwasilisha hotuba hii kwa niaba yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu niwataje kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdalla Mohamed Ali	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mjumbe
4.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
5.	Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Mjumbe
6.	Mhe. Rufai Said Rufai	Mjumbe
7.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe
8.	Ndg. Shemsa Maabad Mohamed	Katibu
9.	Ndg. Khamis Hamadi Haji	Katibu

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imepewa majukumu ya kusimamia Sekta za Kilimo na Maliasili, ili kutimiza malengo ya kuongeza uzalishaji wa tija katika kilimo, kuhakikisha uhakika wa chakula na lishe katika nchi na kusimamia uhifadhi na matumizi ya rasilimali zisizorejeshesheka.

Mhe. Naibu Spika, majukumu hayo ni makubwa, kwani bado tunatambua kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa letu. Ili nchi ipige hatua kubwa ya maendeleo basi kujitosheleza yenyewe kwa chakula ni muhimu. Ni ukweli usiopingika kuwa, kilimo bado kinaendelea kuwa muhimili mkuu wa maisha kwa wananchi wanaoishi mjini na vijijini hapa Zanzibar. Inakadiriwa kuwa asilimia 45% ya watu wa visiwa hivi kwa njia moja au nyengine, wanategemea sekta ya kilimo katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Kiuchumi, sekta ya kilimo inakadiriwa kuchangia wastani wa asilimia 32.2 katika pato la taifa na asilimia 75 ya mapato ya fedha za kigeni.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuvuka lengo la makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2011/12. Katika mwaka huo Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 238, 500,000/= na hadi kufikia mwezi Juni 2012 jumla ya shilingi 539,751,956/= zimekusanywa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo mfupi, naomba sasa nieleze japo kwa kifupi maoni ya Kamati yangu, kuhusu mipango ya utekelezaji iliyoanishwa katika Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Idara na Taasisi zilizomo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Idara Ya Mipango, Sera Na Utafiti:

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Idara hii ni kuimarisha mifumo ya kisera, sheria, mikakati na mipango ya wizara katika kukabiliana na changamoto zilizopo, kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya kisera na ya wizara, kuimarisha mashirikiano kati ya wizara na

taasisi za ndani, za kikanda na nje ya nchi, kuimarisha tafiti za kijamii, kiuchumi na kisayansi ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo pamoja na kuendelea kusimamia programu na miradi mipya na ile inayoendelea.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inapendekeza kwamba sera hizo zinazohusu kilimo na misitu pamoja na tafiti zake zichanganye na kujumuisha fikra za makundi yote wakiwemo wakulima wenyewe, wataalamu wa kilimo na watu wa utawala. Kwa hiyo, kamati yangu ilipokuwa inawatembelea wakulima katika maeneo yao, wameonyesha kuwa mara kadhaa sera na mipango inayowahusu, inapangwa kutoka ngazi za juu na wao kuhusika katika ngazi ya utekelezaji tu.

Hata hivyo, kamati yangu inapongeza hatua ya wizara kwa kujiwekea lengo la ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa kwa njia ya tovuti na Jarida la Mkulima. Kamati yangu inashauri walengwa wote hasa wakulima waeleweshwe umuhimu wa kufatilia na kupata taarifa hizo kwa wakati.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya idara hii kiasi cha shilingi 1, 844, 094,000/= zimeombwa kutoka serikalini kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 na shilingi 7, 160, 570,000/= kutoka kwa wahisani, katika kukamilisha malengo mapya na yaliyobaki. Kamati yangu inatoa angalizo kwa serikali kuwa siyo vyema malengo yaliyowekwa katika bajeti iliyopita yawe hayajafikiwa halafu Wizara ikaomba fedha zaidi katika bajeti inayofuata kwa kuweka malengo mengine au yale yale. Hivyo, ni lazima basi yanapowekwa malengo, viwekwe na vipaombele na maelezo ya kina yatolewe ya hatua za utekelezaji zilipofikia na changamoto zake.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi:
Mhe. Naibu Spika, mambo makubwa ambayo kamati yetu inayasisitiza ni suala la mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa hatimiliki wa rasilimali za serikali zilizopo chini ya Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Kamati yangu inaendelea kukumbusha Wizara kuharakisha na kukamilisha zoezi la uhakiki mali zake na kuzipatia hatimiliki ili kunusuru upotevu wa mali hizo hapo baadaye.

Katika mwaka wa fedha 2011/12 kiasi cha wafanyakazi 198 wamepatiwa mafunzo ya ngazi tofauti, kamati yangu imetiwa moyo na hatua hiyo, lakini bado inaona kuwa idadi hiyo ni ndogo na inahitaji kuongezwa, kwani bado wataalamu wanahitajika katika kutatuwa changamoto zinazokabili sekta ya kilimo na maliasili. Hata hivyo, kamati yangu inapongeza hatua ya serikali kuongeza kasma katika idara hii kutoka shilingi 170, 700,000/= katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na kufikia shilingi 938, 760,000/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu hairidhiki na kiwango kidogo cha mishahara wanayolipwa wafanyakazi wakongwe wa sehemu ya ufundi katika Karakana ya Matrekta Mbweni. Kamati yangu inaiomba serikali kupita wizara hii kuwatazama kwa jicho la huruma wafanyakazi hawa, kwa kuwaongeza mishahara ili watakapostaafu wapate cha kujishikiza katika mafao yao. Mhe. Naibu Spika, tunapokumbukana na wenzetu kama hawa tusiwasahau!

Idara ya Kilimo:
Mhe. Naibu Spika, kutokana na punguzo katika pembejeo za kilimo, wakulima wetu wamehamasika sana na kuunga mkono juhudi za serikali kuleta Mapinduzi ya Kilimo, ambapo

jumla ya ekari 31,933 za mpunga zimelimwa Unguja na Pemba ambazo ni sawa na asilimia 96.76% ya lengo lililowekwa. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa mchango wake wa asilimia 75% ya gharama za pembejeo. Hata hivyo, nichukuwe nafasi hii kuitanabahisha Serikali kuwa bado kuna mapungufu madogo madogo ambayo yanatakiwa yarekebishwe, ili mwitiko huo wa wakulima wetu usirudi nyuma.

Miongoni mwa mapungufu hayo ni uwekaji wa takwimu sahihi za idadi ya wakulima, mahitaji halisi ya pembejeo na mashamba yao. Jengine ni usambazaji wa mbegu na madawa. Kamati yangu imekuta malalamiko kwa baadhi ya wakulima wa mpunga ambao walikosa baadhi ya pembejeo kama vile dawa za magugu. Kamati pia inaikumbusha Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kuhakikisha kuwa Idara hii inapatiwa fedha mapema kabla ya msimu wa kilimo haujaanza kwa ajili ya matayarisho ya nyezo kama vile matrekta na kadhalika, ili malalamiko ya wakulima ya kuchelewa kulimiwa mashamba yasiwepo.

Chuo Cha Kilimo – Kizimbani:
Mhe. Naibu Spika, chuo hiki tayari kimeshapata usajili wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) na kinaendelea na utoaji wa mafunzo katika fani za kilimo na mifugo kwa vijana wetu waliomaliza na kufaulu elimu ya Sekondari katika masomo ya sayansi.

Kwa hiyo, kamati yangu inaiomba Serikali ikipe kipaombele chuo chetu hiki kwa kuongeza fungu la bajeti kwani shilingi 500,000,000/= zilizotengwa hazitoji. Chuo kinahitaji kupatiwa vifaa na nyenzo za kisasa za kufundishia na mazingira mazuri ya wanafunzi kujisomea; ili tupate wataalamu walio bora katika fani za kilimo na maliasili.

Aidha, Kamati yangu inaikumbusha Wizara ihakikishe kuwa fedha za mradi wa mafunzo ya walimu na ununuzi wa vifaa kutoka ufadhili wa Norway, zinaoneshwa wazi katika bajeti kwa vile fedha hizo ni za Serikali kupita mkono wa wafadhili hao, kamati yangu ilipopitia bajeti ya Wizara hii, fedha hizo hazijaonyeshwa matumizi yake.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo:
Mhe. Naibu Spika, juhudi kubwa ambazo wizara inazipitisha katika kufikia malengo ya kuwa na mbegu bora na uzalishaji mkubwa wa mazao, hazitafanikiwa endapo hakutakuwa na utafiti wa kutosha katika maeneo yote yakiwemo utafiti wa udongo bora wa kilimo na aina ya mazao, mbegu bora katika eneo stahiki, mbolea bora kwa aina fulani ya mazao na mengi mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, wakati kazi ya kuzifanyia utafiti mbegu nyengine za mpunga, mazao ya mizizi na mbogamboga zinaendelea, kamati inasisitiza kuwa Serikali itenge fedha za kutosha katika bajeti za kuunga mkono tafiti hizi zinazofanywa na wataalamu wazalendo. Kamati yangu inaelekeza kuwa tafiti zinazofanywa na wataalamu wazalendo, ziandikwe na kuhifadhiwa kwa kila hatua zinazofikiwa na hatimae kuchapishwa baada ya kukamilika kwake.

Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe:
Mhe. Naibu Spika, idara hii ni mpya, imeundwa kwa madhumuni ya kuratibu masuala ya uhakika wa chakula na lishe, ndiyo idara inayofanya upembuzi yakinifu juu wa uanzishwaji wa Hifadhi ya chakula ya Taifa (*National Food Reserve*).

Hata hivyo, kamati yangu hairidhiki na maendeleo madogo ya hatua za uanzishwaji huo wa uhifadhi wa chakula zilivyofikiwa, Idara hii ndiyo kwanza inajikongoja katika kuandaa utaratibu wa uanzishwaji wa maghala tu, wakati ripoti ya uchambuzi yakinifu ya mtaalam mwelekezi kutoka Shirika la chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) imeshawasilishwa na Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe imeshapitishwa hapa Barazani tokea mwaka jana. Hivyo basi, kamati yangu inapendekeza kuwa, kwa vile mwaka huu wa fedha idara imeombewa kiasi cha shilingi 629,760,000/= kutoka Serikalini na shilingi 236,592,000/= za wahisani, ni vyema basi, Serikali ikatowa mchango wake kwa wakati ili kufanikisha maendeleo ya mpango huu kuanza mara moja.

Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka:
Mhe. Spika, katika kuinusuru nchi yetu na athari ya majangwa na mmong'onyoko wa ardhi, Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka ina jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba kunakuwa na udhibiti mzuri na utaratibu muafaka wa ukataji na upandaji wa miti lakini pia uteuzi mzuri wa maeneo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji wa mchanga. Kamati inapendekeza kuwepo na zoezi maalumu la upandaji miti kwa kila sekta husika ili kuinusuru nchi yetu na janga la mabadiliko ya tabia ya nchi.

Aidha, katika kunusuru uharibifu wa vyanzo vya maji, wizara ichukuwe hatua kali, kwa kushirikiana na vyombo vingine husika, za udhibiti wa ujenzi holela na uvamizi katika vyanzo vya maji ambavyo vinapunguwa kwa kasi.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaishauri wizara kufanya jitihada ya usimamizi wa hali ya juu katika eneo la ukusanyaji mapato ya vibali vya kuchimba mchanga, kokoto na mawe, ambapo fedha nyingi zinaweza kukusanywa, iwapo mianya ya uvujaji mapato hayo itazibwa. Aidha, tatizo la upatikanaji wa risiti lisifanywe kisingizio cha serikali kukosa mapato katika eneo hili, kamati yangu inaagiza kama tatizo hilo lipo kweli basi lipatiwe ufumbuzi haraka.

Idara ya Umwagiliaji Maji:
Mhe. Naibu Spika, bado tunaamini kabisa kwamba mkombozi wa kilimo cha mpunga ni kilimo cha umwagiliaji maji. Pamoja na kugundulika kwa mbegu ambayo haihitaji maji mengi (*NERICA*) lakini vile vile tuna maeneo mengi ya mabonde, basi ni vyema tukaweka mikakati madhubuti ya kukiendeleza kilimo cha aina hii katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la kuimarisha miundombinu ya kilimo, ujenzi wa misingi ya ndani ya umwagiliaji nalo ni muhimu, kamati yangu imeona kuwa fungu lililotengwa la shilingi 620,380,000/= kwa idara hii halitoshi kutokana na umuhimu wa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji. Kamati yangu inashauri Wizara kuwa, katika kufanikisha ukulima wa tija na kujitosheleza kwa chakula, mikakati yetu sasa lazima ilenge katika kilimo cha umwagiliaji tu, nyakati tulizonazo siyo za kutegemea kilimo cha mvua na kama tunavyojuwa hali inayotukabili ya mabadiliko ya tabia ya nchi inafanya utegemezi wa kilimo cha aina hiyo kuwa ni wa changamoto kubwa.

Mhe. Waziri ametuelezea katika hotuba yake kuwa wastani wa mvua za masika katika kipindi cha miezi mitatu kwa mwaka huu umepunguwa kwa kufikia milimita 444.4 ambazo ni asilimia

51% ya wastani wa mvua ya milimita 870 ambayo hupatikana kila mwaka katika msimu wa masika.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na inawaomba wajumbe wote kwa moyo wa unyenyekevu pamoja na utulivu mkubwa kabisa waijadili na kuipitisha bajeti hii bila ya matatizo ya aina yoyote na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, naomba kuunga mkono Bajeti hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe ahsante kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati kwa kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa maoni yangu binafsi katika bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nilisikia umeshasema na wananchi wako wa Kikwajuni, nikadhani umemaliza. Nakupa fursa.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa napitia *hansard* ya tarehe 06 Julai, 2011 katika Swali Nam. 186 ambalo liliulizwa na Mhe. Wanu Hafidh Ameir juu ya suala zima la ukame ambao umekutikana katika eneo la Micheweni, na swali hili pia likaongezewa nguvu na Mhe. Subeit Khamis Faki.

Kwa kweli hapa Mhe. Waziri kwa wakati ule alielezea suala la kufanyika utafiti juu ya suala zima ule mtama ambao uliingiliwa na wadudu katika eneo la Micheweni, na badala yake wadudu wale wakasababisha wananchi wa Wilaya ya Micheweni wakakosa kupata mavuno mazuri ya mtama kutokana na wadudu wale. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja hapa atusaidie kutuelezea utafiti ule umefikia wapi? Baada ya maelekezo hayo ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nafasi tunampa mchangiaji Mhe. Saleh Nassor Juma, afuatie Mhe. Asaa Othman Hamad na ajiandae Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu kuhusu Hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia kuwa hai na hatimaye kutupa uwezo wa kuondoka kwenye maeneo mpaka katika nyumba hii. Kwa kweli hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Naibu Spika, nadhani nitumie fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu.

Nianze mchango wangu katika ukurasa wa 4 na 5 kuhusu mchango wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo, ambapo Mhe. Waziri ameelezea kuhusu ukuaji wa sekta hiyo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli zaidi ya asilimia 45 ya Wazanzibari wamejikita na kuwekeza maisha yao katika suala zima la kilimo. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba kilimo hichi hakiwasaidii wao wala serikali inayoongoza nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hivi sasa tunayo hii nadharia ya Mapinduzi ya Kilimo, ambayo Mhe. Waziri katika bajeti ya mwaka jana na hata hii amezungumzia sana azma ya serikali kuendeleza Mapinduzi ya Kilimo, lakini ni nadharia tu. Kwa kweli hivi tunavyozungumza ni kwamba msimu wa kilimo wa mwaka jana umemalizika, wakati Mhe. Waziri aliahidi kwamba kutatoa ruzuku ya pembejeo, matrekta, dawa za magugu, lakini jambo la kusikitisha Mhe. Naibu Spika na wala sitaki niseme hazikutoka, isipokuwa hazikukidhi hata asilimia 30 ya mahitaji ya wananchi.

Kwa mfano, Mhe. Naibu Spika katika vijiji vya jimbo langu maeneo ya Vitongoji, Uwandani, Kibokoni, Wawi wakulima walichelewa kupelekewa matrekta na wengine hawakupata kabisa mpaka yakapelekwa matrekta katika msimu wa mvua, yaani mvua inanyesha wao ndio wanachimbuliwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hili ni kwamba tatizo, kwa sababu katika hatua muhimu ya kilimo na wataalamu wanaita *land preparation*, yaani matayarisho ya ardhi ambayo ni hatua muhimu sana katika suala zima la kilimo. Kwa hivyo, katika matayarisho ya ardhi ni pamoja na kuchimbua mapema, kuburuga pamoja na kutayarisha mazingira ya kuweka hiyo mbegu, ili mbegu ukiiweka iweze kupata hewa, maji na mche kuchipua vizuri, lakini leo unachimbua shamba huliburugi mvua tayari imeshaanza kunyesha, sasa ikeshanyesha mvua wakulima wanalazimika kutia mpunga.

Matokeo yake ni kwamba katika maeneo ya Vitongoji pamoja na Wawi, zao la mpunga halikupatikana kutokana na kwamba watu walibweteka kutokana na kauli ya serikali kuwa matrekta yatakwenda tena kwa bei nafuu na wakapeleka mapema, lakini matrekta haya yalichelewa mno na wengine hawakupata kabisa kulimiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hili ni kwamba kweli watu wamewekeza kwenye kilimo, lakini serikali yetu haiko *serious* katika kuhakikisha kwamba Mzanzibari kilimo kinamkomboa na hilo ni moja.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kilimo tumekipa majina mengi, kama vile Kilimo ni Uti wa Mgongo au Siasa ni Kilimo na leo tunayo Mapinduzi ya Kilimo. Lakini nashangaa kwamba Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa wanao wataalamu wazuri, sasa kwenye kuondosha zile taaluma zao za maneno kuzipeleka kwenye matendo ndio tatizo, mimi ninawaheshimu sana, kwa sababu najua katika wizara hii kuna wataalamu wazuri tu waliobobea ambao ni rafiki zangu wapo hapo juu, lakini tunapokwama hivi sasa ni *translation* ya *theory into practical* na matokeo yake wakulima tunaendelea kupata shida Mhe. Naibu Spika.

Kwa hiyo, mimi nadhani Mhe. Waziri na leo unatujia na nyimbo ile ile ya Mapinduzi ya Kilimo. Je, mara hii umejitayarisha namna gani kuhakikisha kila mkulima wa Jimbo la Wawi na maeneo mengine ya Zanzibar wanapata matrekta kwa wakati, pamoja na mbegu za kutosha na sio utupe maneno tu Mhe. Waziri sisi, kwa sababu mwaka jana uliwaambia hivyo hivyo wananchi, naweza kusema hamna mlilolifanya.

Kwa mfano, katika eneo la Kibokoni, Vumba, Udusini, Changuo mpaka Uwandani kuna watu walipata kikombe kimoja cha *NERICA*, sasa kikombe kimoja cha *NERICA* kitakufanya nini wewe, masheha huu mpunga hamuwapi au wanautwanga na kula na watoto wao jamani. Kwa kweli mimi nashangaa wapiga kura wangu wananiambia kwamba nimekwenda kwa Sheha na kupewa kikombe kimoja cha mbegu, mimi nitakifanya nini?

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe.Waziri atuambie kipindi hichi mbegu zilikuwa kidogo au masheha wamezitwanga ikiwa hakuna *NERICA* tutie ule ule Ringa, Kibata Ngoto, yaani tutatia ile mipunga yetu ya asili, lakini mkituambia mnatuletea *NERICA* na halafu mnatuletea kikombe kimoja kitatufanya nini sisi, mnataka kutuua na njaa, kwa sababu ikiwa hakuna *NERICA*, basi twende kule kule kwa Kibata Ngoto, Mzuri Hajipambi tutatia hiyo hiyo sisi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije katika ukosefu wa Mabwana au Mabibi Shamba katika maeneo ya vijiji. Mhe. Naibu Spika, siku zote tunaambiwa kwamba Mabwana Shamba au Maafisa *Organ* tutapeleka, kama kuna tatizo ambalo linatusibu wakulima Mhe. Naibu Spika ni kukosa Mabwana Shamba. Mabwana Shamba ni muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo chochote Mhe. Naibu Spika. Leo hii katika maeneo yetu upande wa mashariki ya Pemba tunalima kilimo cha kujaribu na kubahatisha, kile kile kilimo alichokiacha marehemu Mzee Karume ndio kile kile tunacholima.

Pamoja na kujaa jopo la wataalamu waliokuwepo hapo juu. Kwa sababu wanakaa ofisini hawaji vijijini, hili ni tatizo Mheshimiwa. Leo utamkutia mkulima analima zao hilo hilo, mwaka nenda mwaka rudi katika ardhi hiyo hiyo, wataalamu wanaita mono culture. Matokeo yake yavuni, mazao yake hayamsaidii, yane yeye ni mpunga na mpunga katika ardhi hiyo hiyo. Lakini angekwenda mtaalamu pale akamshauri basi bila shaka angeweza akabadilisha mbinu za kitaalamu akapata kulima vizuri. Hivi sasa napelekewa habari kutoka Vitongoji huko sehemu za Makaani mahindi yameingia kunguni Mgunda, hawajui hata wawafanye vipi.

Ingekuwa wataalamu wanapita pale wangewasaidia sana. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, ikiwa waziri ana tatizo la wataalamu waseme aende ashauriane na Waziri katika mambo ya utumishi wa umma ili awaajiri hawa. Sisi kwa hilo hatutoona shida kumpitishia pesa kwa kutuajiria wataalamu wa kilimo kwa sababu ndio roho zetu tulipoziwekeza. Lakini utakaa mwaka nenda mwaka rudi hapiti, hili ni tatizo, hakuna mabwana shamba matokeo yake tunalima mahindi ardhi hiyo hiyo, hakuna ushauri wa kitaalamu. Tungekuwa tunapata utashauri wa kitaalamu pengine baada ya kulima zao moja tungelima mazao mseto nadhani mafanikio mazuri yangepatikana. Katika hili Mhe. Waziri atakapokuja atatueleza kwamba aidha hawana wataalamu akatwambia tufanye maarifa japo baadhi ya mafungu kumuajiria wataalamu au vipi.

Mheshimiwa mimi ni Katibu wa Chama ch Siasa CUF wa Wilaya katika *election manifesto* ya CUF sisi tumenadi sana kwamba uwezo wa wananchi, kutumia vipawa alivyowajaalia Mwenyezi

Mungu, kwa kutumia mazingira yaliyowazunguka ikiwemo hiyo ardhi kuweza kujipatia kipato na kuishi vizuri. Wenzetu wa TANU wao enzi. zao waliita *education for self reliance*, sisi tukaita utajirisho kipindi kile.

Mheshimiwa inasikitisha sana kwamba serikali haitusaidii wananchi hichi kilimo kikawa kinakidhi mahitaji yetu ya maisha. Sisi katika eneo la Vitongoji kule katika jimbo langu la Wawi na maeneo mengine ya Makaani, Uwandani mpaka jimbo la Ole, Makaani sehemu za Kangagani, sehemu ya Kiuyu, wanalima sana hizi tungule kwa wingi. Lakini la kusikitisha tungule hizi huwa tunapata bei pale mwanzo mwanzo tu, zikianza tu tukipeleka pale Chakechake tunapata kuuza vizuri. Lakini mazao yanapochanganya tunalazimika kuzitupa, maana kuna kuuza na kutupa, sisi tunatupa. Kwa hivyo sisi hatunufaiki wala familia zetu hazinufaiki, hii serikali yenyewe pia hainufaiki. Maana hatuwezi hata ku- *manage* kulipa kodi kwa hiyo bei tunayopata.

Sasa Mhe. Waziri na jopo lako wa wataalamu wa kilimo waliokuwepo hapo juu mtatusaidia nini sisi wakulima ambao mazao yetu huwa hayana bei, mtatumia utaalamu gani katika ku- *stabilize agricultural price* kwa sababu *production* ikiwa kubwa kidogo mazao yanateremka bei. Ninachokuomba Mhe. Waziri katika Wizara yako kupitia jopo lako la wataalamu ambao wengi nawaona hapo swahiba zangu nimesoma nao, utatusaidia nini ku- *stabilize agricultural products* zikiwemo tungule za Vitongoji. Umasikini umetukwama, maana hii Wapemba tunasema ni kiyaso mtu kulala na njaa wakati kitu unacho ni *kiyaso*.

Sasa utwambie Waziri na jopo lako la wataalamu, mtamsaidia vipi mkulima wa Vitongoji Umangani, mtamsaidia vipi mkulima wa Vitongoji Uwandani, mtamsaidia vipi mkulima wa Ole Kangaga, mkulima wa tungule ili aweze kumudu maisha huku akiwa anauza matungule yake bila ya bei, nyinyi mtakabiliana nalo vipi hili la bei ya tungule. Nyinyi mmeanzisha Wizara nzima pale ya vitega uchumi na kupunguza umasikini, sasa sijui kwa nini mnakwama. Tunateketea jamani kwa njaa, tungele tunalima kwa wingi lakini hatuna beii.

Sasa tunataka mtusaidie wataalamu tufanyeje. Nyie kazi yenu ni kuwaambia watu kuja kuwekeza mambo ya utalii tu, wanatupitia humu hawana nguo, wambieni basi waje waweke viwanda wasindike hizo tungule sisi tupate bei pahala tuuze. Msiwambie kuja hapa kutuendea utupu tu hapa. Samahani Mhe. Naibu Spika.

Mheshimiwa vile vile sehemu ya Kiwani, Kengeja na wao wana tatizo hilo hilo. Nadhani kukosekana kwa wataalamu basi vile vile tunakosa ushauri matokeo yake tunaharibu mazingira. Ardhi ukiipanda zao hilo hilo ina maana ardhi inakufa na mazingira yanaharibika, huku kuna mabadiliko ya tabia nchi. Kuna ukataji wa masitu waje watushauri hawa, tulime vipi. Kwa sababu sehemu za Vitongoji na Micheweni tunachoma moto misitu tukilima sasa itakuwaje ni vyema wataalamu waje Mhe. Naibu Spika.

Jengine tuje katika hichi kilimo cha mazao ya misitu. Mhe. Naibu Spika, kama kuna kitu cha kukienzi katika kipindi hichi cha mabadiliko ya tabia nchi ni kulinda misigu na rasilimali zake. Hichi ni kipindi cha matatizo sana hasa sisi tuliyokuwepo katika visiwa. Siku zote hapa kwenye Semina tunaambiwa maneno mengi kuhusiana na mabadiliko ya tabia nchi. Na sisi katika hili ni lazima tukishakupewa ile taaluma tuweza na sisi kuwambia wataalamu waendeleze taaluma ile tunayoipata.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba misitu ya asili tunaihitaji sana tuitunze. Lakini sasa ndio nilisema mwanzo kwa sababu hatuna mabwana shamba, watu tunapanda misitu hii iliyokuwa sio ya asili ili kuitunza ardhi yetu. Lakini hatuna maelekezo ya wataalamu. Kuna miti kama mikaratusi tunapanda sasa, kuna miti kama mivinje tunapanda sasa, mikeshia tunapanda ili kuilinda ile ardhi isiharibike. Lakusikitisha ni kwamba nadharia mbali mbali za kitaalamu zinaonesha kwamba hii badhi ya miti ni tatizo kwa mazingira.

Kuna miti hata ukiipanda inaharibu mazingira, pamoja na kwamba umepanda kwenye ardhi ipo miti ile lakii inaharibu mazingira *in direct*. Kwa mfano mvinje *transpiration rate* ya mvinje inasadikiwa ni kubwa mno. Inakausha ardhi tunavyoambiwa. Ukija hapa unaambiwa haiharibu. Lakini wenzetu Bara mikeshia, mikaratusi wameikata katika maeneo mbali mbali katika Mikoa ya Bara kwa sababu ya kuwepo katika vyanzo vya maji. Siye huku tunaambiwa tupande, huko kwetu sisi Vitongoji kila unapotizama kuna mvinje, huku mihogo haiwi lakini mivinje hailiwi lakini inakuwa.

Mheshimiwa tatizo ni kwamba wataalamu watueleze hichi kilimo cha mivinje kilichokwisha kutambaa sana Kaskazini huku Unguja nimeiyona mingi, Kusini na Pemba kule nimeiyona mingi katika sehemu ya Mashariki ya Pemba katika sehemu za Makaani ni kweli inaharibu ardhi. Kwa sababu mimi najua ukiangalia katika baadhi ya nadharia unaona ni kweli kuna *lenticular transpiration* kwa wingi, kwa hivyo inapoteza maji sana.

Wataalamu wanatwambia vipi. Kwa mfano ardhi ya Vitongoji sasa hivi imeshaanza kuchoka sana kutokana nap engine ni hiyo mivinje. Je, nyie wataalamu hili suala la mivinje ni kweli au ni maneno yetu tu.

Mhe. Naibu Spika: Ujali muda umeshatumia dakika 20 nakuongeza na dakika 5.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa sababu jana nilikosa kuchangia, nashukuru sana.
Mhe. Naibu Spika, sasa twende katika zao leo hili la mkarafuu, napenda niipongeze serikali pale na Mhe. Waziri ingawa simuoni sijui kainama. Mheshimiwa kasema atahamasisha mambo ya miche watatoa bure, hili niipongeze serikali. Nadharia zinaonyesha kwamba mkarafuu katika nchi hii uliingia tangu karne ya 16 na mfanyabiashara mmoja wa kiarabu aliyekuwa anaitwa Saleh .Nadharia zinaonesha hivyo.

Mkarafuu ule ule uliongia katika karne ya 16 hadi leo hii ni ule ule tu, hauna ila kwenda juu sana. Imekuwa ni mirefu mno na wakwezi wengi wa mikarafuu ni akina mama hawaiwezi tena. Sasa nyiye wataalamu wengine hapo juu mpo, waziri na jopo lako wa wataalamu hebu tueleze ni utafiti gani mlioufanya kuweza kuona huu mkarafuu hatuwezi kuupata *high breed.* Naona nyie kazi yenu ni kusema mbegu za Nerica tu, tumefanya nini, mbegu ishirini za mpunga, mkarafuu jee, ni mbegu ngapi ulizozitafuta mkaona kwamba tunaweza tukapata mkarafuu mfupi na unaozaa sana.

Wanawake hawawezi tena kupanda mikarafuu jamani na sisi wanaume tukipanda tukifika juu tunatetemeka tunaanguka. Hapa Zanzibar hapana hata ICU, kule kama tukifika tukapelekwa

Hospitali tufanyiwe uchunguzi, hakuna hata CT-Scan hakuna. Sasa tunaomba hebu wataalamu mukae, muone tangu mkarafuu aliokuja karne ya 16 haubadilishiki ukaja chini kidogo. Lazime muwe *serious* katika hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nimalizie kwa kuwapa mfano hawa wajapani wao walikuwa wakitegemea sana kilimo cha mpunga. Basi kupitia serentisti wao mmoja katika mji ule wa Korosawa bwana mmoja Jiberera Jujikoroin ni Mjapani huyu, alifanya utafiti akaone ile punje moja ya mpunga mbegu ile ukiiweka ardhini inaweza ikatoa miche 24. Wakawa ni wazalishaji wakubwa wa American Pichori, mpaka wakaacha kuzalisha mchele wakaingia kwenye viwanda. Lakini wakawa wanafanya utafiti wa kuzalisha mchele mara kwa mara. Sisi hatuna utafiti huo ni ule ule makarafuu ule tu, hatuwezi ku- *modify*.

Mhe. Naibu Spika, jengine mbali na mche katika huu mkarafuu ikiwa hapana juwa wakulima tuna matatizo sana, siku zote tunauza mpeta. Yaani mpeta ni zile karafuu zilizokuwa hazina bei. Miaka yote hiyo tunategemea mkarafuu huu kama ni zao la biashara. Sisi tunategemea *system* ya kuukaushia kwa jua tu. Juzi moja niliambiwa karafuu ukiwa unaikaushia kwa njia nyengine yoyote inateremka bei. Haya basi hamuwezi kutayarisha ma- *chemise* nyie wataalam, mkafyonza huo muangaza wa jua siku za jua, ikifika siku za mvua mkauteremsha kwenye hizo karafuu zikakauka.

Nyie wataalamu sisi ni wana siasa hatuna hata jambo moja tunalolijua, nyie hamuwezi kufyonza miangaza ya jua baada ya kipindi cha mvua kile mkaiteremsha miyonzi hiyo karafuu zikakauka. Mimi nadhani hawa wataalamu wafanye kazi, waumize kichwa sisi tumetumia fedha zetu kuwasomesha hawa, waumize vichwa ili waone wanasaidia vizazi vijavyo, ili kuzipatia karafuu njia mbadala ya kukaushia ili tupate maslahi tusiuze mpata tu siku za mvua.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima na nitakapokuja kupata maelekezo haya ya kutosha kwamba matrekta yatafika kwa wakati lini Vitongoji pamoja na NERICA pamoja na hizi karafuu zetu miche, tumeshachoka kuanguka mikarafuu, mikarafuu ni mirefu, hapo ndio nitaunga mkono hoja baada ya kupata maelekezo hayo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi angalau kuweza kusema machache kwa wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, ninze kwa kusema kilimo bado ni tegemeo letu na kama tutafanya vizuri tutaweza kusaidia taifa hili na wananchi wake. Mchango wangu miye zaidi utakuwa ni maswali na ushauri. Nimuombe Mhe. Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii Komredi Nyanga na Cruu wake kwamba wana dhima kubwa ya madadiliko haya ya kilimo.

Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza hili, Wizara hii inatoa taaluma, hawa ni wataalamu na wala tusitarajie kwamba wanayo ya zaidi ya ziada zaidi ya taaluma yao. Sisi tuikamate serikali kwa nini serikali imeshindwa kufikisha (a), (b), (c) kupitia kwa Mhe. Waziri. Mhe. Waziri anaomba serikalini, akishindwa kukidhi mahitaji aliyoyaaomba hana jinsi.

Mimi naiyomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuikamate serikali kwa hayo madai yetu. Sasa aliposhindwa taaluma Mhe. Waziri tumkamate hapo. Suala la tekta Mhe. Naibu Spika, matrekta kuna wakati unalifikisha pale ni kiangazi kikali halifanyi kazi na unaweza ukalifikisha tena trekta ni mvua nyingi pia halifanyi kazi. Sasa hawa wenzangu hawana la kufanya watabadilisha matrekta hayo kuelekeza sehemu nyengine.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni maeneo yanayofikwa na maji ya Chumvi. Nadhani Komredi kama umeomba fedha hizo vipi utazitumia kama zitatosha au laa, mjipange kwenye hilo. Lakini haya ni mambo ambayo serikali kwa makusudi ichukue kwamba ni dharura.

Mhe. Naibu Spika, jengine pato la taifa mchango wa kilimo asilimia 32.2 na 75 mapato ya fedha ya kigeni. Ni taarifa njema inatia matumaini. Lakini nasema hatutoweza kutofautisha kilimo na tukaiwacha mifugo mbali, tukasahau na viwanda. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni visiwa hatuna eneo la kujivunia kilimo, tuna eneo la kuweza angalau na sisi tujisogeze kupunguza mahitaji au uwagiziaji.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri na watu wake naomba labda wanisikilize katika hili. Mimi nadhani nimepata mawazo mbadala, wataalamu naomba mnisikilize sana, ikiwa ndivyo sawa la kama sivyo mtaenda vila mnavyoona ndivyo.

Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, lakini mabadiliko ya watu sasa watu ambao wameamua kwa makusudi kuchafua mazingira, uharibifu huo wa mazingira lakini na serikali kushindwa kwake kusimamia haya kuendelea kumwagilia mazao ya kilimo kwa kutarajia kwamba mufikie malengo yale ya umwagiliaji wa zao la mpunga maji tuliyonayo ni *underground water*. Hetu litizameni litaweza kuchukua kwa muda gani, si vyema nahisi tukajiridhisha sisi sasa hivi, tukajakuachia ukame wenzetu, wajukuu na vilembwe vijavyo.

Naomba sana Waziri wa Utumishi Mheshimiwa nataka uje uwatumikie na wengine. Nasema *irrigation* ya Zanzibar ni kutegemea visima ni *underground water*. Lakini *underground* hii ingeleta muelekeo kama tungeweza kumudu kusimamia uharibifu wa mazingira na uchakavu wake. Tungeweza kumudu kuwasimamia wanaolimka sehemu zile wanazojenga sehemu za kilimo, tukakatazana kuyachukua mashamba ya kilimo na tukageuza maeneo ya majenzi. Haya yote yametushinda.

Sasa tutakaposema twende na umwagiliaji huu miaka 50, tutakayoshereheka sisi Ishalla keshokutwa watoto wetu watakuja kusherehekea 50 ijayo. Kama hivyo ndivyo Mhe. Naibu Spika, kama serikali inataka kuamua tuanze sasa isimamie masuala ya upandaji miti kwanza hilo. Lakini haya mengine ya uchumbaji wa mchanga, ukataji chensoo, mpaka leo serikali imeshindwa kutoa kauli juu ya msumeno huu. Minazi inateketea, mikarafuu usiku wa manane, lakini msheha wapo, hili hawaliwezi.

Mhe. Naibu Spika, ili tuweze niseme sijui asilimia 45 ajira ya kilimo kwa Wazanzibari, tutaweza kuipata asilimia ile na ziada yake, kama mazao ya kilimo, mazao ya mifugo tutayaweka kwenye kusindika. Hapa nilitaja kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda ndio tutazungumza ajira. Vyenginevyo wala tusijidanganye hakuna ajira. Ajira ya kilimo itatokana na usindikaji wa mazao haya ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Sasa tusije tukamuhoji tena Komredi juu ya hili, tuihoji serikali, kwenye Sera zake za Viwanda tunataka kusindika tutaendelea kujisifu karafuu mara hii, karafuu mara ile. Tumekwenda kuziuza kwa magunia vile vile, hebu tubadilike, ile tija ni lazima tuibadilishe, karafuu tokea Said wa Said inauzwa kwenye magunia, sasa tunaiyuza vipi. Hapa tunazungumza tija, karafuu hivi iyendavyo tunaipoteza.

Mhe. Naibu Spika, sasa tunasema kuna mkakati huu wa kuongeza idadi ya mikarafuu. Nilikuwa nikitizama mikarafuu milioni moja kama sikosei, Kimkoa ni kila Mkoa kwa Mikoa ya Zanzibar ni miche laki mbili, kila Wilaya ni miche laki moja, kila jimbo majimbo yetu 50, miche ishirini elfu, *Are you serious*. Miche mkarafuu alikuwa akiipanda babu yangu peke yake, leo jimbo zima ati tunaipalengo 20,000. Masuala ya bidhaa hizi ni sawa na bidhaa nyengine kuna kupanda na kushuka. Tumehongera mwaka jana vipi karafuu imetunyanyua tulipokuwepo.

Jamani hebu tutizame tunafanya nini juu ya zao hili. Bado tumpeni fedha nyingi Komredi huyu afanye kazi, vijana wapo kule kwenye suala la tafiti. Mnaposema wafanye tafiti mkarafuu na bibi yangu aweze kuuchuma bila ya kuweka ngazi hatoweza kwa kusema hapa tu, anataka akafanye kazi na kazi haitofanyika bila ya fedha. Kwa hiyo mpeni fedha za kutosha. Tafiti ni kazi nzito inahitaji fedha nyingi. Kwa hiyo kupanga ni kuchagua, tutafute mikarafuu mifupi yenye kuzaa kwa wingi lakini yenye kustahamili maradhi na pia muda mfupi tuwe tunavuna, lakini tumpe na fedha.

Mhe. Naibu Spika, kila taifa Mwenyezi Mungu kalijaalia na mkongojo wake wa kuendesha watu wake, nilisema na leo narudia kwamba, kilimo kwetu kitakuwa na tija endapo tutaitumia bahari kuu. Alichotujaalia Mwenyezi Mungu sisi si ardhi angalau kuweza kuishi, lakini katuzungushia bahari ndio mgodi wetu. Bahari ni yetu Wazanzibari lililotupa kwenda kuipeleka kwengine sasa tunashindwa kuitumia ni lipi, tutaendelea kulaumiana pesa haitoshi, pesa tumeiwacha kule.

Mhe. Naibu Spika, ule mgao kuambiwa Bahari kuu si ya Muungano, uvuvi wa Bahari kuu ndio wa Muungano mamlaka imejengwa hadi sasa jibu sahihi mgao wende vipi, imetajwa *figure* lakini kuna *logistic* kadhaa hazijakaa vyema hadi sasa ku-*operate*. Asilimia 50 imeambiwa itaendesha mamlaka hii, hebu Wazanzibari kaeni hasa tujiulize hamsini zitaendesha hii mamlaka, hamsini iliyobaki inagawiwa tena mara mbili, arobaini ya Wazanzibari, sitini ya Watanganyika. Mimi huwa najiuliza hivi Tanganyika huwa hai pale kwenye maslahi na huwa haipo imekufa pakiwa hapana kitu? Mana kwenye mgao huu imetajwa Tanganyika, sisi hapa ukisema Tanganyika unaambiwa sema Tanzania Bara maana yake wenyewe tunajikanganya.

Tanzania Bara haijaungana na Zanzibar iliyoungana na Zanzibar ni Tanganyika huru kwa hivyo ipeni jina lake iliyozaliwa nalo Tanganyika ndio tutakuwa tunafanya jambo la msingi kabisa na Zanzibar hivyo ndivyo ilivyo. Lakini Tanzania Bara haimo kwenye maandiko yale ya muungano tunatoa mambo ambayo si sahihi. Kwa hivyo, asilimia hii ya uvuvi wa bahari kuu tumeisaliti wenyewe hapa, tumeshindwa kuisimamia na kwa sababu tumeshindwa wenyewe wa kututetea hayupo, kama ni lawama tujilaumu wenyewe.

Kuna wakati Waheshimiwa Wawakilishi mnasema wataalamu wanakwenda kwenye mikutano hii, vikao hivyo vya kufikisha mambo haya, vikao vya wataalamu vina mahali pake vinagonga

kunakobaki sasa masuala ya sera ni viongozi nyinyi wa siasa haya yamepelekwa na nani? Mtadai trekta, mbolea, mtadai nini zitoke wapi pesa hapana mpaka wahisani watake, pesa mnazitupa wenyewe Waheshimiwa mimi bado nasimama hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe, Waziri wangu wa Kilimo na Maliasili na wataalamu wake hili suala la mbolea hebu fanyeni *comparison* hii Minjigwimize iliyoko Arusha ni mbolea nzuri ya kupandia. Mbolea ya kupandia ina *phosphate* nyingi mwanzo ilianza na *powder form* sasa iko chengachenga, lakini pia wamefanikiwa kuitia nitrogen kiasi, *potassium* ipo, boroni imo, sulphur imepatikanwa. Lakini mnaweza mka-*trace* wenzenu wakakuvunjeni moyo, kinapigwa vita kile kiwanda na wajanja ili watu waendelee kuagiza mbolea nje kuna *commission*. Minjingwi ipo Arusha hapatakuwa na *commission*, lakini nakuombeni nendeni wenyewe mtaonana na utawala mtaweza kuzungumza muone kama mkiagiza ama kuagiza pale karibu mtatizama itakavyokuwa kupunguza haya masafa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema yangu leo mimi nimo wizarani kwangu naomba nimalizie mawili. Mhe. Naibu Spika, kwa heshima zote naiomba serikali kwamba ielekeze nguvu kuona ni namna gani visiwa hivi siku hadi siku vinamong'onyoka sasa kwa bahari. Uwezo wa kuyakinga maji ya bahari kifedha ni mgumu hilo halitaki mjadala, lakini basi kwa kutumia rasilimali ziliopo na rasilimali watu tusisubiri hali ikaja ikafika pabaya zaidi. Maeneo yaliyokuwa yakilimwa mpunga sasa hivi mengine ni jangwa wakati wenzetu wengine majangwa wanageuza mahali pa kulima na wanavuna, sisi mle mwa kulima sasa inakuwa jangwa hebu tujiulize tunakwenda wapi? Kwa hivyo, ushauri wangu naomba sana kwamba serikali hebu itupe macho kwenye maeneo haya, tufanye kazi ya ziada kunusuru hili.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho suala la mazingira ikifuatana na hoja nzito inayoulizwa mara zote Shamba la Makurunge. *Comrade* hebu tusaidieni tunataka maelezo ni vipi shamba la Makurunge ambalo liligharimu fedha nyingi za Wazanzibari tukawekeza pale hatima ya shamba hili sasa hivi tumefikia wapi? Tunataka maelezo ya kina, maelezo yenye uhai na mwelekeo juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie wizara hii, waikosoe, waielekeze na hatimaye kuikamata serikali kwa iliyoshindwa wizara, ili iwaongezee fedha waweze kufanikisha waliyokusudia. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumi.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami mchana huu kupata fursa ndogo ya kutoa mchango wangu juu ya Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Kwa hivyo, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa na kusimama mbele ya ukumbi huu kwa kuchangia.

Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na hatimaye nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake bora na makini kwa hotuba yake hapa. Nadhani kama alivyomwita aliyepita nyuma kuwa huyu Mheshimiwa ni *comrade* kweli, amebobea katika masuala mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu na hali ya uzalishaji, kila wizara inayokuja sisi tunasema wizara hii ni muhimu katika nchi yetu. Kwa ufupi wizara zote ni muhimu kwa sababu

ni *chain process*, ni kiungo. Lakini wizara ya kilimo inaambatana na uhai bila chakula hakuna uhai, bila chakula hakuna amani, bila chakula hakuna urafiki wala udugu. Kwa hivyo niseme Wizara ya Kilimo ni moja katika wizara muhimu sana na wizara hii ni vyema ikajua jukumu lake kuwa ni moja katika wizara muhimu sana kwa sababu imebeba uhai wa maisha yetu, bila kula hakuna maisha. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, uhai wetu uko juu ya mgongo wa kama alivyomwita mwenzangu *comrade*.

Mhe. Naibu Spika, wizara imetangaza hapa katika bajeti yake takriban kila sehemu kuvuka malengo ya uzalishaji napongeza kwa hilo. Lakini nichukue zao moja tu la mpunga ambalo wamesema wamevuka lengo, sio kuvuka lengo wamezalisha zaidi mwaka 2011 kuliko ilivyokuwa mwaka 2010. sasa hapa wangepita zaidi kama wangelikuwa ni wasimamizi wazuri wa kilimo, kwa sababu kuna maeneo Mhe. Naibu Spika, huduma halisi za kilimo hazikupita na kama wangelijikita vizuri basi hapo walipofika wangepita na pengine uagiziaji wa chakula ungelipungua, lakini bado wizara hii inaonesha hawajajipanga vyema.

Kwa sababu pamoja na kwamba kuna maeneo ambayo hawakulima hawakupeleka huduma zao lakini bado inaonesha kwa takwimu zao kama ni za kweli kuna ongezeko la chakula. Sasa kama wangeliweza kuhudumia vizuri ongezeko hili lingezidi zaidi ya hapa palipoongezeka, chakula kikizidi uagiziaji kutoka nje ungelipungua na kwa hivyo fedha yetu ingelipungua kutoka nje, fedha ikibakia ndani kwa matumizi ya ndani ile tunayotangaza kuwa uchumi unapanda kwa asilimia fulani wananchi wangeliiona. Lakini leo kila senti inayopatikana inatoka nje unakuja mchele, kwenye fedha nyengine kunatoka nje kwa hivyo lile ongezeko la serikali inalotangaza la uchumi wetu mwananchi wa kawaida halioni. Kutwambia kwa kujenga barabara nyingi ni ongezeko la uchumi hapa mwananchi wa kawaida hakufahamu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, iko haja ya wizara hii kujipanga zaidi. Kuna lugha Mhe. Naibu Spika, sio wizara hii tu, wizara zetu nyingi katika mambo yao mengi kutangaza kuvuka lengo. Kwa kweli lugha hii mimi inanipa mashaka wamevuka walikisia kidogo. Kwa mfano, hapa kwenye ukusanyaji wamesema walilenga kukusanya shilingi 238 milioni *point some thing* na wakakusanya shilingi 539 *point some thing.* Kwa hivyo walivuka lengo sana, hivyo walivuka lengo waliweka kidogo waonekane kuwa ni watendaji.

Mimi hii lugha ya kuvuka lengo Mhe. Naibu Spika, siiungi mkono nahisi wizara inajiwekea makisio madogo halafu wakusanye kingi kidogo waoneshe kuwa wamefanya kazi kubwa, ndani yake hapa kwa maoni yangu mna ujanja fulani kwa sababu pia inawezekana ikawa pamekusanywa zaidi ya kile ambacho wamekitaja hapa, lakini kwa sababu lengo lao lilikuwa ni dogo zaidi sisi tutaamini kuwa hiki ndicho kilichokusanywa. Kwa hivyo hii tabia ya kuvuka lengo naona mimi sio nzuri sana, ama hawakujipanga vyema wanakisia kidogo ili watangaze kikubwa tuone watu kuwa ni wafanyakazi bora ambapo mimi hii siungi mkono. Pamoja na kuwa imezoweleka katika serikali yetu, kila siku watu wanavuka lengo asilimia mia moja mara nyengine wanavuka mpaka asilimia mia mbili au mia tatu sijui wanavuuka vipi wenyewe ndio wanaojua wanavyovuuka.

Mhe. Naibu Spika, nije katika mazao ya biashara na niuzungumze huu mkarafuu ambao ni mmoja katika zao letu la biashara. Hapa kila unapoona pameoneshwa kuwa kuna miche milioni moja, milioni moja, milioni moja, haiongezeki wala haipungui. Mhe.

Naibu Spika, wakati fulani nilikuwa niko katika jimbo langu wakaja watu wa kilimo kuandikisha watu wanaohitaji miche ya mikarafuu mimi nilijisajili na wakaniuliza idadi ya miche ninayotaka nikawaambia, hadi hii leo ninaposema hapa hata mche mmoja sikupewa lakini kila kitu wanavuka lengo wao. Kwa hivyo, hii ndio hali ya mambo yetu yalivyo tunavuka lengo lakini watu mahitaji hawapati.

Mhe. Naibu Spika, hali hii bado haijaridhisha katika utendaji wetu, mkarafuu unaolelewa na kilimo katika maeneo yetu mengi unapooteshwa nitumie Kiswahili cha kwetu unapopandwa, baada ya muda mfupi inakufa kuliko ile ambayo wakulima wanaing'oa porini na kuiotesha. Ningewaomba wataalamu wa kilimo wakafanya utafiti kwa nini ile yao isiwe bora ambayo inalelewa kuliko mboni ya jicho, lakini matokeo yake haistahamili hali ya nchi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, hii sisemi kwa kubahatisha kwa sababu mimi natoka maeneo ambayo hapo zamani mikarafuu ilikuwepo leo haipo tena, lakini ile miche yake inayopandwa kutokana na wataalamu wa kilimo miche wanayochukua katika nasari zao na wale wanaong'oa misituni basi ya misituni inanawiri zaidi kuliko hii iliyolelewa vizuri. Kwa hivyo, hapa ipo haja ya wizara hii kufanya utafiti wa kutosha kwa sababu bado karafuu pamoja na kuwa utalii upo lakini na karafuu bado ina mkondo wake katika uchumi wa taifa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na maongezeko mengi yaliyotajwa narudia tena kuna matatizo makubwa ya maradhi katika mazao yetu mbali mbali, mbali na matunda kama embe na mengineyo lakini kadhalika kuna wadudu waharibifu wa mihogo hata ndizi. Migomba zaidi ya mtwike ambayo yanalimwa sana Pemba baada ya kutoa ndizi mingine unaona kama unaanza kufa na ndizi inaanza kuwiva na bado iko changa. Hii imeathiriwa na wako wadudu weupe kwa jila la kitaalamu siwajui wanavyoitwa ukienda katika shamba wanakuingia katika virago vyako ulivyovaa. Lakini sina hakika kwa maeneo mengine, lakini katika eneo langu hakuna utafiti wowote wa kitaalamu uliofanyika kuhusu tatizo hili la migomba, migomba ikiwa ni moja katika zao linalozalishwa sana katika visiwa hivi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, iko haja tena ya Wizara ya Kilimo kufanya utafiti kwa mazao yote tunayopanda katika nchi hii na kuhakikisha kuwa tunapata mazao bora na wakulima wetu iwe hawapotezi nguvu zao bure.

Mhe. Naibu Spika, katika msimu wa kilimo uliopita Jimbo la Mtambile pamoja na kuwa wizara imevuuka lengo hakuna hata nusu ekari Mtambile au Kangani iliyopata huduma ya kilimo yaani kulimwa kwa trekta, watu tumelima kwa kijembe kongoroka nikutie mbanio, lakini bado tumevuka lengo. Sasa lengo tungelivuka zaidi kama tungeliwalimia wakulima wetu wote. Mhe. Naibu Spika, bado wizara hii haijajitanua nchi nzima, huduma zake bado hazijaenea kwa kila mkulima, elimu yake haijamfikia kila mkulima, hivyo niseme bado kwa Wizara ya Kilimo haijafanya kazi yake kama inavyohitajiwa ifanye. Nataka ijue kwamba wao ndio maisha ya Wazanzibari kwa sababu maisha ni chakula na wao ndio wanaozalisha chakula.

Mhe. Naibu Spika, mimi hata hizo dakika 20 ulizonipa sitaki nizimalize niseme tu kuwa mbali ya kuangamiza kunguru kuwa ni maadui, hawa wadudu wengine wa matunda mihogo, maembe, mpunga na kadhalika ni maadui zaidi kwa sababu wanashambulia vile vyyakula

tulivyovitegemea kama vile mahindi, mihogo, ndizi, mkazo wetu katika kupambana na uharibifu tungelitilia mkazo katika mazao haya ya chakula na hawa kunguru tukawaangamiza kwa sababu waangamizaji hawa wamekuwa wawili, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ikawaangamiza kunguru wakija wao hakuwasemea leo na Wizara ya kilimo pia itawaangamiza kunguru lakini mimi naomba wizara hii iangamize wadudu waharibifu wa mazao ya chakula. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipa wakati huu kuweza kuchangia kilimo uti wa mgongo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Assaa hapa alisema kuwa wizara hii kwa kweli hatujaitendea haki na hasa kutokana na mafungu yake tunayompa ni kidogo mimi nakubaliana naye tena namuunga mkono Mhe. Asaa asilimia mia moja. Tunaendelea katika kuchangia utakuta hali halisi huko mbele.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia ukurasa wa mwanzo kwanza katika ukurasa wa 1.3 nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutetea vyema Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2010/2015 kwa kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhini ya adui maradhi njaa na umasikini kwa mafanikio.

Mheshimiwa naendelea sasa ukurasa wa 21 kilimo. Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni nilikuwa mimi mwenyewe msimamizi mkuu wa kilimo katika jimbo langu la Kitope ili kuona namna gani jinsi harakati za kuweza wananchi wetu kuondoa umasikini kwa kupitia kilimo cha mpunag. Lakini kwa masikitiko makubwa sana nisikitike na wakiri wizara kuwa kwa kweli ni muda ambao wa kuwapelekea matrekta wananchi wamechelewa, hilo moja naomba sana wakiri. Katika kuchelewa kwao kumewapelekea wananchi kuanzia bonde la Kilombero, Pangeni, Upenja na maeneo mengine Mtomchanga wapi huko mote, hawakupata mpunga, wengine wamechelewa kupata mbolea, wengine kupata dawa za kuuwa magugu.

La kusikitika zaidi Mhe. Naibu Spika, wengine hata zile pesa zao walizopeleka za kupatiwa trekta hawajalipwa. Mhe. Waziri kifungu nakizuwia mimi hiki. Sababu zilizonifanya nikizuwie ninazo sababu mbili kuu, kwanza naiomba wizara ije kunambia wale wananchi watapewa fidia ya kucheleweshwa mpunga wao wakaukosa wameingia umasikini sasa hivi hata ile mbegu hawana. La pili, kwa nini pesa zao wasirejeshewe angalau wakenda kununua hayo mapembe yaliyolazimika wende wakanunue.

Mhe. Naibu Spika, walijitahidi sana wizara kuleta mambo ya pembejeo kwa wakati lakini wamechelewa kwa sababu ukileta pembejeo wakati huna trekta basi inakuwa *nothing* tu, haiwezekani ikafanyika ile pembejeo kwenda kwa wakati kwa sababu hakuna kile kitu cha msingi.

Juzi mimi nilikaa kwenye televisheni Mhe. Naibu Spika, kwa uchungu sana na nilitoka machozi kule Bara tuseme kwa huku kwetu niseme wao kule wana kata sisi tuna wadi huku, masafa itakuwa ni makubwa kutokana na kata na wadi lakini tuchukue kesi moja na hiyo haina tofauti anakabidhiwa Diwani matrekta mengi sana si chini ya matrekta 50 wakati sisi hapa matrekta 50 wanapewa mkoa mzima au Zanzibar nzima. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, inasikitisha san asana. Kwa nini inakuwa hivyo jibu nitakuja kupewa, sasa kweli tunaidhamiria wizara hii.

Lakini la kushangaza pale tunaambiwa kuwa serikali imechukua sehemu nayo katika mkopo kuilipia. Serikali ya Jamhuri ya Muungano inasema imechukua sehemu kwa kupitia na wao mkondo ule wataweza kulipia lile deni. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hatujawa tayari. Wananchi wa Kilombero na Pangeni wanakufa na njaa wamejitutumua, wamepoteza nguvu zao, wamepoteza na mali zao kwa kuuza ili kujitayarisha na kilimo cha trekta. Waheshimiwa kwa kweli inasikitisha sana hii nakusudia kupeleka ujumbe najua waziri wangu ni mpya, waziri aliyejiandaa hayupo wakati ule kaja kumwachia mzigo Mhe. Suleiman Othman Nyanga nimshukuru na nimpe pole kutokana na kuwa wizara hii ni nzito sana sio ya mchezo. Sasa naomba sana kama nilivyoyaeleza hayo.

Vile vile nimshukuru sana Mkurugenzi wa Matrekta niseme kwa kweli alifanya kazi kubwa sana alijaribu kuweka muda zaidi alipandisha muda na mwengine alijaribu kuweka ili watu waweze kufanya nini, mafundi wake waweze kupewa, lakini sijui kama potisha walipata katika wizara hiyo siwezi kujua. Lakini namshukuru alijitahidi sana tu, tukawahi angalau kuwahi lakini sio vile nyakati zinavyoeleza. Kwa kweli pongezi zake pamoja na mafundi wote lazima haki yao wapewe kama kuna mambo ambayo hawafikishiwi sasa namuomba Katibu wa wizara hii awafikishie, kama kuna vijiposho na mambo mengine.

Lakini pia niwashukuru hao hao tena na mkurugenzi wangu wa kilimo naibu kwa jitihada zake nao kuniona siku hiyo nahangaika akaweza kunambia Mheshimiwa chukua trekta hili hapa lakini ujitolee binafsi ili uweze kuokoa wananchi, hilo moja nilifarajika sana na tulitengeneza na tulifanya kazi, naomba wanipe tena kwa wakati huo wakulima wa kunde ili nikatengeneze wananchi waweze kulima Kilombero na Pangeni, aendelee na moyo huo huo na Mwenyezi Mungu amzidishie ili tufike pahali panapotakiwa. Sasa tujitolee na sisi waheshimiwa kwa kuisaidia serikali kutengeneza yale matrekta ambayo yaliyokuwa mzigo mzito ili tuokoe wananchi wetu nao wapate kulima kwa wakati. Nalo hilo nalipongeza sana na niko pamoja na wao.

Mhe. Naibu Spika, katika kuendelea kwangu niingie katika Idara ya Misitu. Kwa kweli hawa watu wakiongozwa na Mkurugenzi wao jamadari wake nimsifu sana Mheshimiwa huyo na hasa kwa koti alilovaa leo kuwa ni zuri sana na ni moja katika kuonesha ishara nzuri ya utendaji wa kazi. Kwa sababu unapojinadhifu wewe mwenyewe ukawa mzuri ukajitengeza afya yako basi na utekelezaji unakwenda vizuri vile vile. Lakini nimpe pole kwa wakati huu wa Mwezi wa Ramadhani ndipo misitu yetu inapoteketea, mkurugenzi kaza uzi usisikie gari ya Makame Mshimba, gari ya Juma ya nani usizitoe fuata sheria.

Kipindi hiki Mhe. Naibu Spika, msitu ndipo unapolia wa Kiwengwa, unalia hasa msitu nisamehe, nisamehe, niache, niache na hii yote ni kuoneana haya kwa sababu wakikamatwa wananchi wetu sisi waheshimiwa tunakwenda mbio mkeketa, mheshimiwa hilo suala usilikubali bwana fuata sheria. Mkurugenzi tuko pamoja na wewe fuata sheria usiache kabisa, na sisi Wahehsimiwa tunachangia humo humo tuseme ukweli ulivyo ndio maana baadhi ya wakati tunawapa mzigo mzito watendaji wetu, tunawapa kazi kubwa sana simu inafanya kazi pale gari yangu nambari 3 au 4 mmeikamata na pengine kumtishia amani, mtu anataka kazi atafanya nini, ataiachia tu.

Lakini hivi karibu Mkurugenzi wangu kanifurahisha amepiga faini ikiwa gari ya nani au ya nani shilingi laki tatu na kuendelea, hongera sana Mhe. Mkurugenzi na uzi huo huo usirudi nyuma na sisi watu ambao tumo mle kwenye maeneo ya misitu tutakusaidia kupambana na hao wahalifu wa kutukatia misitu yetu bure.

Pia ninawaomba sana wizara idara hii tuisaidie kwa mafao yake mbali mbali kwa sababu wale watu unapowazuia wasikate msitu wapewe na shughuli za kuweza kufanya, ninaomba sana watafutiwe fedha za kuwaongezea *community* walinzi wazuri na vifaa vyao waongezewe kupewa ili msitu wetu uendelee kunusurika angalau tuwe na historia hiyo.

Mhe. Naibu Spika, misitu tuliobakia nayo ni mitatu tu, Jozani, Ngezi na Kiwengwa. Mhe. Waziri watendaji wake anao wazuri akiwemo na mwenyewe na watendaji wake kwa kweli wamejipanga vizuri sana.Wana mashirikiano mazuri, wana *special day* ya mikutano jinsi gani ya kufanya. Hata kwenye mazingira namshukuru anajitahidi sana kupanga programu nzuri ya uchimbaji wa mchanga, anao utaratibu huo sasa hakuna utaratibu wa kubabaishababaisha sasa wanakwenda vizuri. Lakini nataka kuongezea taaluma hapa kidogo, namuomba sana Mkurugenzi ahakikishe wale watu wanaochimba aidha kifusi au mchanga wakimaliza tu awalazimishe wapande miti, asiwaachie hata kidogo aweke kama ni sheria, kama hakuna sheria iwekwe sheria iwe ni lazima.

Mhe. Naibu Spika, aweke hivi, anapotaka kutoa kibali kwanza yule mtu amwambie masharti yetu moja, mbili ndio tutakupa kibali, vyengine vyovyote Mheshimiwa ardhi yetu inakwisha. Bumbwini huko kote kushamalizika ardhi yetu kuchimbwa na watu wanaendelea kuishambulia kuchimba huko. Mkurugenzi tena kusimamishwe huko Bumbwini, watu wamechimba Donge mpaka kukatoka maji sasa wanaelekea Bumbwini, Bumbwini kwenyewe zamani kumekwisha na sasa hivi wanaimaliza tutafute na maeneo mengine yenye mchanga twende kwa utaratibu ndio anavyofanya Mkurugenzi huyu simlaumu. Lakini wanaacha mapengo ya kutopanda miti ili rutba ikaja tena.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala la umwagiliaji ambapo hapa kwa leo itakuwa ndio mwisho wangu wa kuchangia, kama alivyosema mzee wangu, kaka yangu, wizara yake ndio kwanza mpya na yeye sitoweza kumtikisa sana, lakini ajiandae tu buti mbili tatu za kumuonesha yeye kocha wangu wa mpira kuwa mimi mchezaji wake ni mahiri.

Sasa niende kwenye Idara ya Umwagiliaji maji. Mhe. Waziri tulifanyiwa *study* katika eneo langu kule Kilombero na Pangeni kuwa bado kukamilika utafiti, lakini uko mwaka utafanyika mpunga wa kumwagilia maji. Lakini sijui imeishia wapi mpaka leo hii naona kimya sasa hayo ndio matatizo yetu serikali. Tunaandaa programu nyingi katika bajeti zetu, miradi mingi lakini *finishing* yake inakuwa *poor*, ndio maana tunasema serikali bora ichague mradi mmoja tu ihakikishe unakwenda nao sambamba hata ukija kwenye bajeti nyengine unaendeleza hivyo hivyo. Lakini ukiangalia kwenye mabuku humu wanakwambia kuna nini, sijui na nini hakuna *activity* yoyote inayoonesha sasa haya ndio matatizo yake.

Lakini nawashukuru sana Waheshimiwa wa *back bencher* wote maana ya *MTEF* sasa hivi wanaujua, wanauchambua kwa kila kitu. Sasa naomba sana suala la kumwagilia maji mpunga Mheshimiwa tusiende kule tukamdanganya Rais tu kwenye kibango chetu kitita, mimi siku zote husema jamani tusimdanganye Dr. Ali Mohammed Shein, ameweka programu nzuri bango kitita

kwa sababu kupunguza makali humu kwenye Baraza, lakini tunakuta manyago humu tofauti na kule. Kwa sababu kule wanampelekea zile *activities*, na *activities* zenyewe hazikamiliki za kule sasa utashangaa ndio *MTEF* huo! Ukija huku unakuta tofauti kabisa masuala kama yale.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana hebu tuwe *smart* kabisa tunalolieleza kwa Rais na huku kwenye Baraza lazima tulieleze vizuri, vyenginevyo wananchi wetu wanakasirika jamani, wanakasirika mambo mawili, wanakasirika tumemdanganya Rais na wanakasirika mahitaji yao hawayapati hasa kwenye kilimo. Mimi nina wasiwasi pengine Rais kaambiwa tumekwenda na wakati mara hii mpunga tunao.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna kitu kimoja nimefarajika hiki hapa, wameleta mashine sasa hivi ya kuvunia mpunga, serikali hongereni sana tu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanziba kupitia Ilani yake ya Chama cha Mapinduzi imeleta mashine. Mhe. Naibu Spika, mimi sijapata kuona katika kutembea kwangu lakini naiona Zanzibar sasa hivi hapa, basi wamesema ukweli. Lakini nataka kumwambia Mhe. Waziri Upenja tuna mpunga mwingi sana wa JKU leteni mashine hii wallahi kabla kuathiriwa. Naambiwa sijui gari kubwa bovu tukakodi injini wenzetu wamelima hawa JKU mpunga mwingi tuwapelekee na wao hili mashine wakaonje ule utamu na mimi niende nikalione. Naomba sana Mhe. Waziri jitihada hii wanaichukua sisemi uongo, wanakwenda vizuri maafisa wako kitengo hiki cha kilimo wanafanya kazi vizuri, lakini wanashindwa na kupata ile *track*. Sasa sijui kama wameshapata na katibu naye anakwenda mbio kushughulikia suala hili, lakini hapa sijapata jibu naomba jibu lipatikane hapa shimoni kuonekane kwamba watendaji wanafanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika namalizia, naomba sana Bonde la Kilombero, Pangeni, Upenja nipewe ratiba ya kuwa mwaka wa kesho bajeti tutalichimba kwa kupata mpunga wa kumwagilia maji. Halafu hiyo *NERICA* ndio itakuja hapa kwa sababu *NERICA* yenyewe mpaka leo sijaiona, nimeona pale Bambi kwa kupita njia tu ki-*plot* kidogo. Sasa mimi naomba sana sana Mheshimiwa, Wallahi leo nasikitika kuwa Mhe. Waziri sitaki nikuongezee mambo mengi kwa sababu ni mgeni na wizara hii, na ninakujua kocha wangu na mimi umenifundisha vizuri nimefikia kuwa mchezaji mzuri. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nimwambie tena kwa kumalizia kitengo cha elimu kwa wakulima kiendelee vizuri.

Lakini la mwisho maafisa tubadilishiwe katika vituo wasikae pale wakaota sawasawa na ile ardhi ya pale, hebu fanyeni mabadiliko. Vituo hivi vinavyohusika kwa mfano Kilombero, Kibokwa sijui wapi na hasa Kilombero tunaomba sana tubadilishiwe maafisa pale tuletewe maafisa wengine. Hilo naliomba sana Mhe. Waziri sitaki nikupigie buti lakini nakuomba sana hilo, ukija kunijibu nambie tayari afisa ameshabadilishwa wananchi imekuwa kero kubwa sana.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, mara nyingi sana nakuwa siungi mkono mimi masuala kama hayo, lakini nakuunga mkono Mhe. Waziri asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *(S.W)* aliyetujaalia uhai, uzima tukakutana hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Lakini pia nikushukuru na wewe kunipatia

nafasi hii ya kutoa na mimi mchango wangu katika wizara mama hii ambayo wanaitegemea Wazanzibari wengi.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kumpongeza Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, lakini pia nimshukuru Katibu Mkuu na watendaji wake. Mhe. Naibu Spika, nianze na kumshukuru Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein. Nakumbuka wakati wa ufunguzi wake wa Baraza hili katika hotuba yake mara ya kwanza kabisa, basi alisema kwamba; katika awamu yake kutakuwa na Mapinduzi ya Kilimo na Mapinduzi ya Uvuvi. Hatma ya hayo mabadiliko yaliyokuja tulileta sheria hapa ya uhakika wa chakula na lishe, nadhani ni mashahidi juu ya hili.

Mhe. Naibu Spika, sasa baada ya utangulizi wangu huo nami nianze mchango wangu katika ukurasa wa 21 kwenye Idara ya Kilimo. Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Wazanzibari, lakini pia wanawake wengi hujipatia riziki zao kupitia sekta hii ya kilimo. Hivyo basi, Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba dhana ile Rais alipoitangaza wakulima wengi walijenga matumaini na wakisubiri kwa hamu kubwa kabisa kuona Mapinduzi ya Kilimo vipi yatawafikia. Sote ni mashahidi baada ya hotuba ile wakati wa kuichangia tulisema ile ndio dira ya kutuonesha tunakoelekea.

Mhe. Naibu Spika, katika sekta hii ya kilimo hususan katika kilimo hiki cha mpunga kulijengwa mikakati katika mwaka wa fedha 2011/2012, na kulikuwa na punguzo la asilimia kubwa kabisa ya pembejeo za kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana wananchi wengi matarajio yao yalikatika matumaini baada ya kutotekelezeka upatikanaji wa mbolea kwanza ni matrekta ya kulimia kwa wakati wake. Hivyo basi, wengine walilazimika kulima kijembe kongoroka, wengine waliwahi kutoa hata fedha zao lakini hawakuwahi kulimiwa, wakisubiri mbolea ilikuwa inapatikana kwa tabu sana na pia haikuwafikia walengwa wote kama ilivyokusudiwa. Ilipatikana kwa tabu sana na wengine wakihangaika huku na kule lakini niseme kwamba naamini kuwa watendaji wa juu walilitekeleza hili kwa kina kwa kadiri Mwenyezi Mungu alivyowawezesha, lakini ni dhahiri kwamba sehemu ambazo zilisambaziwa hizi mbolea upatikanaji wake basi kulipita mambo ambayo hayakuwa mazuri katika mgawanyo wa mbolea hii.

Kwa sababu Rais katika nia yake ile alifanya kwamba wananchi waweze kumudu kuweza kununua hizo pembejeo, na asilimia kubwa Rais alisema italipwa na serikali na ile ndogo ndio wananchi ili waweze kuneemeka. Lakini kilichokuwa kikitendeka mbolea hizo zilifikia kwa watu wachache na wengine wakizizuia wakifanya ni biashara, tuna uhakika, tumewaona tulifanya *research* katika kuona hilo. Hivyo niombe basi, kwamba utaratibu huu ambao umepita niiombe wizara iandae utaratibu maalum kwa ajili ya mgawanyo wa pembejeo za kilimo ili ziende kwa utaratibu unaokubalika na kuwafikia walengwa bila ya kuingia mizengwe. Wakulima wengi walikuwa wakinung'unika sana hata upatikanaji wa dawa ya kuulia magugu ilikuwa ni tatizo.

Nadhani Mhe. Naibu Spika, tuliingia kwa haraka haraka katika huu mfumo bila ya kujipima, nadhani hakukuwa na utafiti wa kuwajua wakulima ni wangapi na tunahitaji tani ngapi kwa ajili ya mbolea, tunahitaji mbegu kiasi gani, hivyo niwaambie wizara wajipange na wafanye hilo kuwahakiki na kuweza kuwaelewa wakulima wake na kujua ni ukubwa wa ekari ngapi na

pembejeo hizo ni kiasi gani. Kufanya hivyo ndiko kutakakowezesha kuona kila mmoja anapata haki yake.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kulikuwa na mbegu ambazo tulizifanyia majaribio ya uzalishaji wake ya *NERICA* na *KIFICHO*. Naomba Mhe. Waziri atapokuja kufanya majumuisho anieleweshe basi tulipata mbegu hiyo kiasi gani kwa mwaka jana wa fedha 2011/2012, na mbegu hiyo ipo imehifadhiwa na je, imekuwa ni mbegu bora ambayo itawafikia wakulima katika mwaka huu wa fedha wa ukulima.

Baada ya hayo sasa niende katika ukurasa wa 26 katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Mhe. Naibu Spika, utafiti wa kilimo ndio suala lenyewe hasa lenye kubeba mzigo na dhamana nzito, ardhi yetu ni ndogo sana lakini pia inahitaji tuelewe kwa wakulima wale wa mpunga, tuliambiwa *NERICA* na *KIFICHO* inakubali hata ardhi ya juu. Je, tumefanya majaribio imekubali, nadhani tuelewe kwamba ukulima wa mazao mengine pia tunauhitaji lakini ardhi yetu ni ndogo hebu tuangalie ardhi zile za uwanda zinakubali mazao gani na gani, kwa sababu wananchi wetu hawana taaluma katika hili. Nadhani wizara hii itakapofanya tafiti na kuwaelimisha wakulima kuweza kujua matokeo ya tafiti hizo basi tutajipanga vizuri na kuona kwamba tunalima kwa wakati unaotukubali na pia tunalima kwa tija.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Chuo cha Kizimbani, chuo hiki lengo letu kuu nadhani ni kuzalisha wataalamu. Ni dhahiri kwamba wataalamu wetu ni wachache tunakosa mabwana shamba wa kila eneo, na mara nyingi wakulima hukosa ushauri wa karibu kabisa na mara nyingi huharibikiwa mazao yao na kupelekea kula hasara au kufa njaa.

Mhe. Naibu Spika, nikiacha idara hiyo sasa niende katika ukurasa wa 31 katika Idara ya Misitu na Maliasili. Mhe. Naibu Spika, kiukweli kabisa sasa tumefikia visiwani kuona kwamba hata hiyo misitu yenyewe imekuwa tatizo. Hili linatokana na uchimbaji wa mchanga unapohitaji kuchimba mchanga unahitaji uondoe miti iliyopo juu ya ardhi hilo ni la kwanza kabisa. Kwa hivyo, huondolewa miti ile bila ya utaratibu maalum na hatimaye huchimbwa mchanga, lakini pia mchanga huo hauna kima maalum kwa wale ambao wanafanya kazi ile kuambiwa labda ikifika kima fulani iwe basi wewe kuchimba mchanga huo, na badala yake huchimba tu mpaka wakaona basi, sasa hakuna tena linalofanyika na miti haipandwi. Moja katika Wilaya ambayo imeathirika na uchimbwaji wa mchanga na ukataji wa miti ovyo ni Wilaya ya Kaskazini ‘B’ Unguja.

Mhe. Waziri nakuomba tuondoke pamoja ukaone hali ya mazingira ilivyochafuka kwa uchimbaji wa mashimo ya mchanga, kukatwa miti ovyo, misumeno inafanya kazi, hali hii hatujaelewa kwamba nchi yetu ni kisiwa, ardhi yetu ni ndogo na tunaihitaji kwa mambo mengi zaidi, tuna shughuli nyingi za msingi zaidi tukiacha kilimo, tunahitaji viwanda na mambo mengine kabisa kwa ajili ya kupata maendeleo ya taifa letu. Lakini ni ukweli kabisa usiofichika hatuitumii vizuri ardhi yetu kwa sababu tafiti zetu hazituelekezi.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba imetiliwa mkazo sana upandaji wa mikarafuu na upandaji wa miti, lakini mimi ningependa kusema hebu turudi kidogo tuangalie historia ya Zanzibar ilikuwaje. Nadhani wale walionitangulia ni mashahidi kuona kwamba nchi hii ilikuwa na miti mingi sana ya matunda, ilikuwa na mishokishoki, midoriani, mishelisheli, mifenesi, miti hiyo

yote imekatwa kwa kutumia misumeno na hatimaye wananchi wametumia kwa ajili ya mbao na pia bado kabisa serikali haijatilia mkazo upandaji wa miti ya aina hii. Hii ndio miti ambayo inaweza kuhifadhi na kurejesha ile hali ya ardhi yetu na kuweza kuhifadhi maji ambayo ni muhimu kwa shughuli mbali mbali na shughuli zetu za kilimo.

Kwa hivyo, ningeiomba wizara iangalie kwa kina utaratibu huu wa kurejesha ile miti yetu ya asili; ambayo pengine ingefanyiwa utaratibu maalum hili zao lingekuwa la biashara kwa matunda haya kwa ajili ya kusafirisha kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nije sasa kwenye hii Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Mhe. Naibu Spika, hii imebakia kuwa dhana na nasema kwamba inaweka tu kumbukumbu zake. Lakini imani yangu kwamba serikali inapojipangia kuwa na uhakika wa chakula na lishe ni kusema kwamba inaongeza nguvu zake za uzalishaji katika sekta tofauti zinazoonesha kwamba mchanganyiko wake ndio hupatikana hicho chakula na lishe kwa wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, hatukumudu mpunga mwaka huu hali si nzuri, matunda, wadudu wapo tele wameingia. Mhe. Naibu Spika, uvuvi wa uhakika imekuwa tatizo; chakula na lishe kitakuwepo, familia nadhani zitaendelea katika hali ile nadhani tulifika kusema kuwa tunahitaji kuwa na maghala ya kuhifadhia. Tulilizungumza hilo katika ile sheria yetu ya uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Naibu Spika, umefika wakati sasa tusiletewe maneno bali tunahitaji vitendo ili tuweze kuona na kufuata ile dhana nzima ya Rais wa Zanzibar anayetaka kuwaletea mabadiliko ya kweli Wazanzibari ili waweze kuondokana na hali ngumu ya maisha. Ni ukweli usiofichika kwamba wananchi wanajituma kwa nguvu zao zote lakini serikali haijatilia maanani hasa kuona kwamba wananchi washike wapi ili waweze kukwamuka katika zoezi hili zima la shida na maisha. Vyakula vyote tunaagizia zaidi kutoka nje jambo ambalo wakati mwengine linahatarisha afya za watumiaji.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Baada ya kusema hayo ningeomba na mimi nielezwe na Mhe. Waziri atakapokuja hapa jinsi ya Wilaya yangu ya Kaskazini ‘B’ ilivyopata pembejeo kwa mwaka uliokwisha, ili nijenge matumaini ya kuunga mkono hotuba yake hii kwa ajili ya kuwajengea imani wanawake wenzangu ambao ndio wavuja jasho wakubwa katika Wilaya ya Kaskazini ‘B’.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, siwezi kuunga mkono hoja hii mpaka nitakapoelezwa majibu ya kina na hatimaye naweza kuunga mkono. Ahsante sana.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa vile muda ni mdogo mengine nitayaacha nitazungumza machache tu. Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu basi nianze kitabu hiki katika ukurasa wa 45 Mhe. Waziri alitoa shukurani kwa wakulima ambao wanalima kilimo kwa mazingira magumu. Lakini nimwambie tu Mhe. Waziri, shukurani hizi zinatosha, shukurani hizi hazitoshi kama alivyosema kwamba wakulima wanalima vilimo

kwa mazingira magumu na sote ukulima tunaujua. Kwa hivyo, ipo haja wakulima kuenziwa, kuonewa huruma na kuwekewa mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, kuna kesi moja hapa ninayo kesi ya wakulima ambao walikuwa wanalima Bungi katika eneo la kilimo. Eneo lile pana wakulima ambao wamelima ukulima wa kila aina kama vile viazi, mihogo, lakini pahala pale baada ya kwenda kujengwa mnara Wizara ya Kilimo ikaenda kufanya tathmini ili kuwalipa wakulima vile vipando vyao, kilichotokea cha kusikitisha Mhe. Naibu Spika, kuna makisio ya Wizara ya Kilimo hii, hii imefanywa na Wizara ya Kilimo wamekisia shilingi milioni sabiini ili wakalipwe wakulima wale, wamerudi wakapeleka makisio haya yakarejeshwa mara ya pili yakaletwa shilingi milioni kumi na tano. Kinachotia uchungu katika malipo haya kuna watu humu wana visiki vya muhogo viwili basi wamelipwa shilingi laki moja hamsini elfu, unamkuta mtu ana visiki mia sita analipwa shilingi laki mbili.

Kwa hivyo unakuta haya malipo kila mmoja hayakumridhisha hata kidogo. Hivyo kuna malalamiko makubwa ingawa Mhe. Waziri umerithi hii wizara lakini naomba nije kupatiwa majibu juu ya makisio haya yaliyofanywa kwa wakulima hawa. Kwa sababu tunawashajihisha wananchi walime, na kama ulivyosema kwamba watu wanalima kwa mazingira magumu kwa hivyo hii hatari. Kuna Baniani mmoja alisema kwamba, Mungu tupe balaa ikisha utuondoshee balaa, lakini leo wakulima hawa wameletewa balaa halafu wakazidishiwa balaa. Kwa sababu walikuwa na kilimo chao pale washategemea wengine wamelima mazao ya biashara pale pale wamekwenda kusagiwa mihogo yao wamelipwa hawakuridhishwa.

Mhe. Naibu Spika, muda hautoshi lakini hizi ningezisoma zingetupa ufafanuzi mzuri. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri katika wizara yako tupate majibu mazuri ya kuwaridhisha hawa wananchi. Kwa sababu leo inapigwa tathmini ya mwanzo shilingi milioni sabiini, ya pili inakuja shilingi milioni kumi na tano pana nini hapa shilingi sabiini milioni kuripuka mpaka 15 milioni. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri uje unipe ufafanuzi wa suala hili ili wananchi wale wa Bungi waridhike juu ya kadhia hii iliyowakumba na wana kilio kikubwa kwa suala hili.

Jengine moja kwa moja niingie katika Idara ya Misitu. Idara hii niliwahi kuchangia bajeti iliyopita kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wa idara hii mara nyingi wanatizamwa waliokuweko maofisini tu, wafanyakazi wa wilayani hawashughulikiwi, *hansard* ipo nilizungumza bajeti iliyopita hawashughulikiwi, hawatizamwi, naomba Mheshimiwa suala hili hebu waoneeni huruma hawa wana kazi kubwa. Utamkuta mfanyakazi mmoja ana shehia tano, shehia tano ataziranda vipi kwa miguu, tunasikitika misitu inakatwa lakini leo mfanyakazi huyu hakupewa kitendea kazi chochote wakati wa mvua atakwendaje msituni, msitu unakatwa. Kwa hivyo, tuwaonee huruma wafanyakazi hawa na tuwajali, tuwatizame kwa kuwaonea huruma.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuna suala la umwagiliaji maji, bado serikali haijalipa umuhimu suala hili la umwagiliaji maji. Naomba Mhe. Waziri aje anieleze Cheju umeme upo kitu gani kilichokwamisha kusiwe na huu mpango wa umwagiliaji maji. Sasa naomba atapokuja Mhe. Waziri aje anieleze kitu gani hasa kilichokwamisha Cheju. Umeme upo nadhani ni suala ambalo sijui lina ugumu gani kwa eneo hili la Cheju.

Jengine kama nilivyosema kuwa mengine nitayaacha lakini nitazungumzia sasa habari ya kilimo. Kila mmoja aliyesimama hapa amesema kuwa wakulima safari hii wamepata mtihani mkubwa.

Mwaka jana nilisimama hapa nikapongeza sana lakini mwaka huu maeneo yote ukija Cheju ukija wapi watu amepata hasara ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la utoaji wa mbolea alilizungumza Mhe. Ashura Sharif hapa, ufuatiliaji ulikuwa haupo itakuwaje leo mbolea inatolewa ikisha unakujasikia iko majumbani watu wanauza wanavyotaka wenyewe, dawa wanauza watu wanavyotaka wenyewe. Sasa naomba watu wasikae ofisini tu, wasikae ofisini wateremke.

Mwaka jana nilimpongeza sana Mhe. Waziri aliyekuwepo Mhe. Mansoor Yussuf Himid ulikuwepo ufuatiliaji, sasa safari hii ufuatiliaji ulikuwa hapana hata kidogo, mbali na ucheleweshwaji wa kuchimbiwa hili tatizo wakulima wamejitolea kulima tunapiga kelele wananchi walime wanalima. Kwa hivyo, hili ni tatizo ambalo lipo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo zima kwamba wakubwa wanahodhi konde au mashamba sehemu kubwa. Utamkuta mkubwa ana eka 30 mnyonge akalime wapi, kwa hivyo na hili naomba litizamwe. Unamkuta ana eka 30 ndipo yanapokuja matrekta yale kwanza yanafukuzia kwenda kulimia wakubwa wewe mnyonge huna haki. Tufanye haki sawa kwa wote, tunataka wananchi wetu tuwasaidie, kwa hivyo na hili Mhe. Waziri lionekane. Tunapokaa hapa tukazungumza tusimtizame aliye juu tumtizame aliye chini vipi tunamsaidia huyu sasa hili tulioneni ni suala ambalo linaleta matatizo kweli. Wewe kama Katibu Mkuu au nani una konde 30, huyu huku mnyonge anahangaika akalime wapi, tuone hili jamani serikali kama kweli tuna nia ya kuwasaidia watu wetu tuwasaidie watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuchangia haraka haraka mengine nayaacha mimi nasema bajeti hii siiungi mkono mpaka nije nipate maelezo haya ya kilimo cha wananchi wa Bungi nini matarajio yao ya kilimo walichokwenda kupoteza nguvu zao pale, hatimaye inakuja kufanywa tathmini hairidhishi halafu watu wanapewa makisio ambayo hayaridhishi hata kidogo Mhe. Naibu Spika. Utamlinganishiaje mtu ambaye ana visiki vya muhogo 600 ukamlipe shilingi laki mbili na huyu mwenye visiki 200 ukamlipe shilingi laki tisa, inauma hakubali mtu yoyote, hii inauma.

Mhe. Waziri nitakuba hizi karatasi uzione ukisha tukae pamoja na ninakuomba hasa Mhe. Waziri kwa kutaka kuwaridhisha wananchi hawa tufuatane mimi na wewe tuwakusanye wananchi wale tukakae nao pamoja uzungumze nao tujue tunafikia wapi juu ya hatima ya wananchi hawa. Kwa hivyo naomba hili uje unieleze wala usinifumbie macho ukaona mwanamke yule kachangia, naziweza buti mimi sasa.

Mhe. Naibu Spika, siungi mkono mpaka nipate masuala yangu hayo nijibiwe kwa ufafanuzi uliokuwa mzuri. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano mazuri ya kuweza kuipitisha asubuhi Wizara ya Mifugo na Uvuvi na tukasoma Wizara ya Kilimo na Maliasili na tayari tumeshachangia wachangiaji saba wamebakia 10. Nategemea tuje kuchangia kesho na tuimalize Wizara hii. Baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao hiki hadi kesho Jumatano, tarehe 01/08/2012 saa tatu asubuhi.

(Saa 9:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi

tarehe 01/08/2012 saa 3:00 asubuhi)